ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni

19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyagen
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi - Tarehe 29 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 6.

Uchakavu na Ubovu wa Barabara za Ndani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar imeleta faraja kubwa kwa wananchi kwa kushuhudia mabadiliko ya maendeleo katika Sekta ya Usafiri wa Anga, Baharini na Miundombinu, lakini barabara za katikati ya mji ni chakavu na zina mashimo ikiwemo barabara ya Forodhani wakati ndio sura ya Mji wa Zanzibar.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuzifanyia matengenezo barabara hizo ili kuondoa kero kwa wananchi.
(b) Kwa nini Mfuko wa Barabara unashindwa kuzifanyia matengenezo kwa wakati muwafaka njia za ndani wakati vyombo vya usafiri vinatozwa kodi mbali mbali kila mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, barabara nyingi za Mji wa Zanzibar zilijengwa baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 kwa kiwango cha lami. Kutokana na ukongwe wake, mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na ongezeko la magari, pamoja na matukio ya uchomaji wa barabara kwa makusudi, barabara hizo zimekuwa zikifanya mashimo kutokana na kuchakaa kwa lami hiyo na hivyo kusababisha usumbufu kwa watumiao barabara hizo.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imekuwa ikichukua juhudi ya kuziba mashimo hayo pamoja na kuzifanyia matengenezo makubwa barabara hizo hatua kwa hatua. Aidha, serikali imekuwa ikichukua juhudi za kuzijenga upya barabara nyingi za Mji wa Zanzibar na zinazoingia kwenye mji huo kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo mbali mbali, ambapo kwa hivi sasa tayari upembuzi yakinifu na zabuni *(tender documents)* ya kiasi cha 78km za barabara zinazoingia Mji wa Zanzibar imeshakamilika na serikali iko mbioni katika kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

Majibu. Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imekuwa ikizifanyia matengenezo ya kawaida, (*routine maintenance*) ambayo yanajumuisha uzibaji wa mashimo (*potholes patching*) barabara zote zinazojengwa kwa lami pamoja na barabara alizozitaja Mjumbe ili ziweze kupitika kwa urahisi wakati wote wakati zikisubiri matengenezo makubwa ya kuzijenga upya, kama tulivyoeleza awali huo mradi tunaoutegemea.

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Barabara wajibu wake ni kukusanya fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zote husika. Aidha, chini ya utaratibu wa *PA* (*Performance Argument)* Wizara yangu ndio inayosimamia utekelezaji wa utaratibu huo. Hata hivyo, tunaamini pamoja na upungufu wetu wa zamu unaotukabili na uchakavu wake bado kasi tunayofanya inaendana na mahitaji halisi ya ukarabati wa barabara hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri na ya kuvunja moyo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mji Mkongwe ni kivutio cha Watalii nchini kwetu, barabara zake kuwa na mashimo na wakati wa mvua watembea kwa miguu wakiwemo watalii wanapata kero kubwa sana. Je, tunatangaza vipi nchi yetu katika utalii wa kimataifa.

(b) Mbunge wa Mji Mkongwe kama miaka miwili amechangia wizara yako au serikali karibu shilingi 40 milioni za Mfuko wa Jimbo kwa barabara zake za Hankil, Mwembetanga, Mtendeni hadi Vikokotoni pamoja na *Barclays Bank*. Je, miaka miwili hiyo ni lini mtachukua jitihada hizi angalau kuzifanyia matengenezo wakati Mbunge keshachangia karibu shilingi 40 milioni kwa barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali la msingi la Mhe. Mjumbe alikuwa anaulizia masuala ya mashimo katika maeneo ya Mji Mkongwe. Kama maelezo yetu ya awali yalivyoeleza, kwamba tunakiri kuwa barabara zetu nyingi ni kongwe, lami imeishi muda mrefu na *life span* ya barabra zile nyingi zimepitwa na wakati. Kwa hiyo, maharibiko haya tuyategemee kuwepo kuendelea na wajibu wetu sisi ni kurekebisha. Mimi ninachomthibitishia Mhe. Mjumbe kwamba maeneo ya Mji Mkongwe yote ambayo yana matatizo haya ya kufumka barabara ama mashimo, wizara yetu itahakikisha inachukua juhudi za makusudi kuona kwamba tatizo lile tunaliondosha, ili kujenga taswira nzuri na haiba ya mji wetu wa Zanzibar, kwa wanaokuja na waliopo waweze kutembea vizuri kwa kuondokana na usumbufu huo wa kuweko mashimo katika barabara zetu.

Swali la pili ameulizia mchango wa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe. Ni kweli kwamba tunakiri kupokea fedha hizo shilingi 40 milioni na tunamuahidi Mhe. Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe kwamba fedha zao hizo zitatumika kwa ujenzi wa barabara hizo zinazoingia Mtendeni, Mwembetanga na kwengineko. Lakini jitihada za serikali ziko pale pale, pamoja na kwamba fedha hizi hatujazitumia, lakini serikali imechukue jitihada na juhudi za kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mkunazini mwanzo hadi mwisho kwenye Benki ya *CRDB.*

Kwa hivyo, jitihada za serikali tutaendelea kuungana mkono na viongozi wanaotoa michango yao kuhakikisha kwamba huduma hizi tunazipeleka vizuri zaidi kwa wananchi wetu, kwa sababu sote tunajenga nyumba moja hatuna sababu ya kugombania kitu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, natumia kifungu cha 37 cha Kanuni za Baraza, "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, isipokuwa kwamba, swali alililoulizwa waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Naibu Spika: Sema tatizo lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tatizo langu swali langu hakunijibu Mhe. Naibu Waziri, ni lini baada ya Mhe. Mbunge kuwa miaka miwili zimetolewa hizo pesa, kuna dalili au harufu gani inayotaka kujengwa barabara zile. Nataka anijibu ni lini zitashughulikiwa barabara zile, kiswali kidogo sana.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika nakushukuru. Kwanza naomba nimjuilishe Mhe. Mwakilishi aliyeuliza hili swali (b) la shilingi 40 milioni, hili swali tulikwishalijibu mara mbili humu ndai ya Baraza kwamba, utaratibu uliotumika kupelekwa hizi fedha ulikuwa sio sahihi. Kwa hivyo, zilikaa bila ya kujulikana mpaka zikafanyiwa uchunguzi wa kina kwa wataalamu wetu kwenda benki na kufuatilia mpaka wakaiona ***transaction*** iliyotiwa, ilitiwa katika *account* ya wizara bila ya kuelezwa maelezo yoyote yale. Kwa hivyo, hakukuwa na kielelezo wakati fedha hizi zinaingizwa.

Baada ya kujulikana kwamba fedha hizo zipo ndani ya mwaka huo 2013, Katibu Mkuu ameshazungumza na Mbunge mwenyewe kumhakikishia kwamba kwa kupitia Mfuko wa Barabara barabara hizo zitashughulikiwa katika bajeti hii tuliyonayo ya mwaka 2014/2015 bila ya matatizo yoyote. Lakini utaratibu ulioingizwa fedha hizo mpaka ikachukua miaka miwili ulikuwa sio sahihi kwa kuingiza fedha za kiserikali na hizo zilitolewa sio na Mbunge moja kwa moja, zilipitia Halmashauri au Baraza la Manispaa kwa sababu ndio fedha zao Wabunge zinakopitia. Kwa hivyo, hawa walioingiza pesa waliingiza katika njia iliyokuwa sio ya utaratibu na ndio maana ilichukuwa miaka miwili. Lakini uhakika kuwa kazi itafanywa upo uhakika, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mimi nichukue nafasi hii kuipongeza sana *UUB* kwa kuweza kuifanyia ukarabati barabara ya Kwa Hajitumbo - Gulioni, lakini mbali na ukarabati ule kuna sehemu ya Gulioni ambayo hawajaimaliza. Vile vile kuna barabara ya Mitiulaya - Hospitali yaMwembeladu. Je, ni lini barabara hii itamaliziwa pamoja na kufanyiwa ukarabati barabara ya Mitiulaya Mwembeladu ambayo Mwakilishi kupitia Mfuko wa Jimbo aliweza kutoa fedha kuweza kufanyiwa ukarabati barabara hizo.

Mhe. Naibu Spika: Swali mama lilikuwa linahusu barabara ya Mji Mkongwe lakini Mhe. Waziri unaweza ukajibu kwa manufaa ya Baraza letu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba uongozi wa Jimbo la Rahaleo uliweza kushirikiana na Idara yetu ya *UUB* katika kusaidia mchango wao katika kuimarisha huduma za maendeleo likiweko suala la ujenzi wa barabara.

Hata hivyo Mhe. Mjumbe ameelezea barabara mpya ambayo anataka ijengwe, lakini yeye mwenyewe anakumbuka kwamba tulivyofanya mazungumzo na mchango ambao amechangia barabara ambayo ametuomba tumeshamaliza kujenga. Sasa anatuuliza lini tutaingia barabara ya pili hatuwezi kuji-*commit* kwa tarehe, na tunahakikisha kwamba tukipata nguvu barabara ile ni wajibu wetu kama serikali kujenga tutatimiza wajibu wetu huo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linazungumzia kung'arisha miji yetu ya Zanzibar hasa kwa miundombinu ya barabara, na kwa kuwa Mji wa Chake Chake ni miongoni mwa miji mashuhuri sana katika visiwa hivi vya Zanzibar, na kwa kuwa barabara ile inayoteremkia kule sokoni Soko Kuu la Qattar mbovu na haipitiki na ni aibu. Je, Mhe. Naibu Waziri ana mpango gani wa kuifanyia japo hatua ya dharura hasa katika kipindi hiki cha mvua ile barabara iweze kutoa huduma vizuri kwa watu wengi wanaokimbilia kwenye Soko la Qattar.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, swali lilikuwa la Mji Mkongwe wa Zanzibar, lakini kwa kuwa na Pemba uko mji naomba Mheshimiwa atoe maelezo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kumuonea huruma naona bora tumjibu. Mhe. Naibu Spika, barabara hiyo anayoizungumza haizidi mita 300, lakini ni pahali pabaya tafauti na inavyoonekana chini kuna maji mengi sana ardhi yake ni tope tope. Kwa hivyo, ujenzi wake umeshapangwa lazima ichimbuliwe chini ijengwe upya, haiwezekani kufanywa ***lay-out*** kama vile ilivyofanywa katika sehemu nyengine za Mji wa Chake Chake. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 52

Kuimarisha Michezo Katika Idara Maalum

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 70, 80 na hata 90 timu zetu za vikosi (KMKM, JKU na MAFUNZO) zilikuwa zikifanya vizuri katika tasnia ya michezo kama vile mpira wa miguu, riadha, mpira wa pete na kadhalika, jambo lililoleta sifa kwa vikosi hivyo na Taifa kwa ujumla.

(a) Ni kwa kiasi gani wizara yako pamoja na wizara inayohusika na Idara Maalum, mmekaa pamoja na kufanya tathmini ya kuteremka kwa hamasa na uwezo wa timu zetu za vikosi katika mashindano ndani na nje ya nchi.
(b) Ni kwa kiasi gani wataalamu wa wizara yako wanaweza kuinua hamasa za uwezo wa timu zetu za vikosi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika miaka ya 1970, 1980 na 1990 timu zetu za vikosi zikiwemo KMKM, JKU, Mafunzo zilikuwa zikifanya vizuri katika tasnia ya michezo ikiwemo mpira wa miguu, riadha, mpira wa pete na michezo mingine, jambo hili lilivipa sifa vikosi hivyo na Taifa kwa ujumla. Lakini naomba pia nimwambia Mwakilishi kiwamba bado timu za vikosi zimekuwa tishio katika mpira wa miguu hapa Zanzibar na hasa timu zao za Mafunzo na KMKM zimekuwa zikichukua ubingwa katika ligu kuu ya Zanzibar.

(a) Pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia vyama vya michezo kwa usimamizi wa Baraza la Taifa la Michezo, wamekuwa wakishirikiana vyema na timu zetu za vikosi zinazoshiriki michezo mbali mbali. Aidha, vikao vya mara kwa mara katika kuendesha na kuimarisha mashindano ya michezo hiyo vinafanyika. Bado timu zetu za vikosi zinaendelea kufanya vyema na vinachukua nafasi kubwa ya kutuwakilisha katika mashindano ya nje ya nchi. Kwa mwaka huu kama nilivyosema awali, Timu yetu ya KMKM ndio mshindi wa ligi kuu ya Zanzibar na itatuwakilisha katika mashindano ya klabu bingwa Barani Afrika.
(b) Mhe. Naibu Spika, wataalamu wetu wanaendelea kushirikiana vyema na vilabu na timu zetu za vikosi pamoja na timu za kiraia, mfano Timu ya Shaba katika kuwapatia mafunzo wakuu wa michezo na waamuzi wa michezo mbali mbali kwa lengo la kuinua hamasa ya michezo nchini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa amesema serikali inashirikiana nao vyema katika kuwapatia wataalamu katika masuala ya soka hizi timu zetu za vikosi, na kwa kuwa ni dhahiri kwamba wataalamu wa nje ni makini zaidi na husaidia sana timu zetu kupata ushindi katika mashindano ya nje ya Kimataifa, pamoja na kwamba michezo ya ndani vikosi vyetu vinaendelea kufanya vizuri, lakini kwa michezo ya nje bado tunaendelea kusuasua.

Je, ni lini serikali itaandaa utaratibu wa kuzipatia makocha wa kimataifa hizi timu zetu za vikosi ili ziendelee kufanya vizuri sio tu, hapa ndani ya nchi lakini hata katika tasnia ya michezo ya kimataifa.

Pili, Mhe. Naibu Spika, jambo moja ambalo linaonekana kwamba vikosi vyetu pamoja na kufanya vizuri ndani lakini nje havifanyi vizuri ni suala zima la ukosefu wa fedha. Ni lini serikali itapanua bajeti ya vikosi vyetu, ili kuweza kupata nguvu ya kufanya vizuri katika mambo haya ya michezo na kuiletea sifa nchi yetu ndani na nje ya nchi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, mafunzo haya ambayo tunayatoa ambayo yanafanyika hapa nchini huwa mara nyingi yanaendeshwa na walimu kutoka nje. Hivi karibuni mwalimu kutoka Uingereza alikuwepo ndani nchini akiwafundisha makocha wetu mbinu bora za kuendesha mafunzo kwa timu zetu. Kwa hiyo, hili tunaliendeleza.

Suala la kwamba tutafute kocha kutoka nje ushauri wake tunauchukua, lakini tumeona ni vizuri kwanza tuwafundishe makocha wetu wa ndani mbinu bora za kuhakikisha kwamba wanakuwa na uwezo na mbinu za kisasa za kuweza kuzifundisha timu zetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Mwakilishi aelewe kwamba mjenga nchi ni mwananchi mwenyewe, kwa hiyo ni vizuri tuwaamini makocha wetu na tuwape mafunzo ya kutosha ili waweze kumudu mbinu bora za kuwafundisha timu zao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu bajeti ya Wizara inayoshughulikia vikosi hili siwezi kulizungumza lakini naamini kwamba Wizara hii ipo makini sana na wakati wowote hali ya kifedha ikiruhusu basi itaongeza fedha katika masuala ya michezo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, mpira wa miguu sasa hivi kwa wenzetu ni ajira na sio kuwa ni michezo tu. Na kwa kuwa wenzetu wachezaji wa mipira aghlabu wanakuwa matajiri kwa sababu ya fedha wanazozipata katika michezo yao ya mpira. Kwa kuwa sasa hivi timu ya KMKM ndio bingwa hapa Zanzibar na inataka kutuwakilisha katika michezo kimataifa. Na kwa kuwa makampuni yaliyopo hapa Zanzibar hayana utaratibu mkubwa zaidi kujiingiza sana kwenye mchezo huu wa mpira kuwasaidia timu zetu za mipira.

(a) Je, Mhe. Waziri anatoa wito gani kwa makampuni yaliyopo Zanzibar kusaidia timu yetu ya KMKM kwa ajili ya kutuletea ushindi wakati wanaposhiriki katika mashindano nje ya nchi.

(b) Je, kwa kuwa mchezo huu ni ajira sasa hivi Wizara yake inajipanga vipi kuwasaidia wachezaji wetu ili waone wanakuwa na ajira wafanye vizuri zaidi na kuinua vipaji zaidi vya wachezaji wetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba mchezo wa soka ni ajira kubwa sana ulimwenguni. Na ni kweli kwamba timu zetu hazina wadhamini wa kutosha. Sasa mimi wito wangu ni kwamba kampuni za kibiashara ziliopo hapa Zanzibar zishirikiane na Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar *(ZFA)* kuangalia utaratibu wa kuzipa udhamini timu zetu ili ziweze kufanya vizuri zaidi. Katika hilo timu hizi kampuni ambazo zitadhamini tutapata nafasi ya kujitangaza zaidi kibiashara na kwa hiyo na wao pia watapata faida kwa njia moja au nyengine.

Kuhusu suala la pili Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa sasa haina mpango wa kuwasaidia kifedha wachezaji ili waweze kushiriki vizuri katika michezo ya kimataifa. Tunachofanya sisi ni kwamba sera na sheria zilizopo zinaruhusu mchezaji ambaye anataka kucheza katika mchezo wa kulipwa nje ya nchi basi ruhusa inatolewa kupitia Baraza la Michezo na Serikali kwa jumla. Lakini kunambia kwamba niweke bajeti maalum ya kuwapa fedha vijana watakaokwenda kucheza mpira nje ya nchi, hilo Mheshimiwa kwa uwezo wa kibajeti wa Serikali litakuwa ni gumu siwezi kuliahidi mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Mara nyingi katika Baraza la Wawakilishi kuna lawama kwamba *ZFA* imeshindwa kuendeleza mpira wa miguu.

Je, Wizara yake ni lini itasimamia kuondolewa kwa viongozi wabovu walioshindwa kazi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, Chama cha Mpira wa Miguu ni chama ambacho cha kujiamini zaidi. Viongozi wake wanapatikana kwa mujibu wa katiba yao. Na ni wapenzi wa mpira wa miguu ndio ambao wanachagua viongozi wao. Wizara kwa utaratibu uliopo sasa haiwezekani kisheria kujiingiza katika kuweka au kuondoa uongozi wa chama chochote kile cha michezo. Ni jukumu la wanachama wa mpira wa miguu kama uongozi wa *ZFA* uliopo ni mbovu basi warekebishe wenyewe, sio Wizara au Baraza la Michezo.

Katika hili, sheria haikatazi kwamba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa viongozi wa *ZFA*. Kwa hiyo kiongozi yeyote Mjumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Salma Mohammed Ali nae akitaka kuwa kiongozi wa *ZFA* basi taratibu zipo wazi. Naambiwa kwamba Disemba mwaka huu watafanya uchaguzi, basi ingieni katika uchaguzi huu na muwe viongozi kama alivyofanya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Riadha hapa Zanzibar, ili muweze kusaidiana katika kuendeleza mpira wa miguu hapa Zanzibar.

Nam. 13

Kuanzishwa kwa Matibabu ya Haraka Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hivi karibuni Wizara ya Afya Zanzibar imeruhusu utaratibu wa malipo kwa matibabu ya haraka *fast track* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

(a) Je, kuna sera au sheria yoyote inayoelekeza au iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi juu ya matibabu hayo.

(b) Je, kuna utaratibu gani mgonjwa atahitajika kuufuata ili apate huduma hiyo.

(c) Malipo yanayotozwa kwa huduma hiyo yanakwenda wapi.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, napenda nianze kwa kusema ni matumaini yangu kwamba sote tunafahamu Sera ya Afya mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964 ndio sera za mwanzo iliyoeleza kwamba Zanzibar matibabu bure. Bado sera hiyo ipo na itaendelea kuwepo mradi tu uwezo wa Serikali upatikane. Na ndio maana Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein, Mungu amuweke alipoanza alisisitiza kwamba shughuli zote zinazohusiana na uzazi bure ili kupunguza vifo vya kina mama na watoto katika kutekeleza sera hiyo. Sera hiyo ilitekelezwa kwa kipindi lakini ilifika wakati ambapo uchumi wa nchi yetu ulipodorora na uwezo wa Serikali ukapungua na wakati huo huo mahitaji yakiongezeka. Hayo yakaongezewa nguvu na wale wasioipendelea mema nchi yetu walipopita kuwaambia wafadhili wasiisaidie Zanzibar kwa maslahi yao binafsi. Na hilo ndilo chimbuko la sera ya uchangiaji huduma za afya kukabiliana na hali ilivyo.

(a) Mgonjwa yeyote mwenye Bima ya Afya anayehudumiwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja anapata huduma kupitia *fast track*. Lakini pia mtu yeyote mwengine ambaye hana Bima akitaka huduma hiyo ya *fast track* anaruhusiwa kupata, mradi tu afuate taratibu zifuatazo:-

(i) Mgonjwa apitie Idara ya Wagonjwa wa Nje yaani *OPD* na aombe huduma hiyo na nafasi iwepo kwenye wodi.
(ii) Au ikiwa mgonjwa kalazwa katika wodi ya kawaida na akaamua kwa khiari yake kutaka kuhamishiwa *fast track*, anachotakiwa kufanya ni kuwaeleza wafanyakazi wa wodi alipolazwa, nao watawasiliana na *fast track* ili kuhakikisha kama kuna nafasi ili waweze kumhamishia huko.
(b) Malipo yanayotozwa kwa huduma hiyo yanakwenda Wizara ya Fedha katika utaratibu wa fedha zinazokusanywa na Wizara ya Afya kupitia Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, tangu kuanzishwa mpango huu Wizara imekusanya kiasi gani cha mapato ya fedha zinazopatikana na kuingizwa Hazina au zinatumika kuimarisha huduma za afya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Vile vile huduma hii ya *fast track* ina vyumba vingapi na vitanda vingapi, hilo moja.

La pili, kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inasema binadamu wote ni sawa wanayo haki ya kupewa fursa haki sawa. Kwa nini wagonjwa wengine wanalazwa katika *fast track* na wanapata uangalizi mzuri wa daktari na wengine kulazwa wodi ya kawaida. Kitendo hiki si cha uvunjaji wa Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ilipoanzishwa *fast track* mwanzo walikuwa wanakusanya pesa Mnazi Mmoja na wakawa wanatumia Mnazi Mmoja. Lakini baadae Wizara ya Fedha ikawafahamisha kwamba pesa zinazokusanywa pale ni za Serikali, kwa hiyo inabidi ziende kwanza Wizara ya Fedha halafu ndipo watakasimiwa wao za kutumia. Kwa hiyo kwa miaka mitatu ambapo Mnazi Mmoja imeanza kupeleka fedha Wizara ya Fedha , mwaka 2011/12 walipeleka milioni 176,682,779/=, 2012/13 ni 221,829369/=, lakini mwaka huu bado hawajamaliza. Lakini mpaka Machi walikuwa wameshakusanya milioni 184, 250,270/=.

Jibu (b) *fast track* ina vyumba 7, vitanda 14, kila chumba kina vitanda viwili. Suala la wao kwa nini wanapata huduma za haraka na wengine hawapati. Kuna wodi za kawaida ambapo kila mtu analazwa. *Fast track* madhumuni yake ni kulipa kuisaidia Mnazi Mmoja, kwa hiyo atakayelipa atapata huduma ya haraka haraka kwa sababu daktari anaitwa wakati wowote. Lakini haimaanishi kwamba anayelala wodi ya kawaida hapati huduma ya haraka kwa sababu madaktari kule saa zote wapo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Katika jibu la msingi la Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kuna watu wale wasioitakia mema Zanzibar, walipita katika mataifa mbali mbali na kuanza kuwataka wasiisaidie Zanzibar yakiwemo mpaka madawa. Je, watu hawa ni Wazanzibari au ni wageni. Na kama ni Wazanzibari hatua gani Serikali iliwachukulia. Na kama haikuchukua hatua. Je, Serikali ipo legelege au ina tatizo gani hata isiwachukulie hatua watu hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, watu hao ni Wazanzibari na wanajifahamu na wanajua. Wamekwenda wamefanya walichokifanya, Serikali ilichokifanya baada ya kuona kwamba hawasaidiwi na kwa

sababu yao ikaanza kutayarisha huo utaratibu wa kuchangia. Na sio kama Serikali ni legelege kwa kuwa haikuwachukulia hatua, isipokuwa tuliwaona wapuuzi tukawadharau, tukaendelea na shughuli zetu. (*Makofi*).

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa malengo ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ilikuwa ni kuwapatia wananchi wa visiwa hivi matibabu bila ya malipo, lakini kwa kuwa sasa kuna hii inayoitwa *fast track* inaanza kupenyezwa penyezwa humu. Je, hii inatokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Na kama ni ilani ya Chama cha Mapinduzi. Je, Ilani ya Chama cha Mapinduzi sasa inataka kwenda kinyume na malengo ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nimesema hivi kwamba ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza sera ya kwamba matibabu bure na yataendelea kuwa bure pale uwezo utakapokuwepo. Lakini kama uwezo haupo lazima kutafutwe mbinu mbadala. Kwa hiyo Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuifanya ifanye kazi vizuri, mbinu mbadala iliyokuwepo ikaona kwamba ianzishe *fast track*. Na hilo sio kwamba ni jambo geni, hospitali zote ulimwenguni *fast track* inakuwa nazo ili sasa kile kitakachopatikana kihudumie Mnazi Mmoja.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/15 - Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na mchango wetu tulioanza jana na tunategemea mchana tumalizie michango hii ili jioni tumwite Mhe. Waziri atoe majumuisho na baadae tupate nafasi ya kupitisha vifungu. Nina wachangiaji sita, wa kwanza ninampa nafasi Mhe. Hija Hassan Hija, wa pili ni Mhe. Mahmound Muhammed Mussa na wa tatu Mhe. Bikame Yussuf Hamad.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na asubuhi hii tukiwa katika shughuli hii muhimu ya wananchi kwa ajili ya kutetea bajeti ya Ofisi ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, aidha nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma kurudi katika hali yake ya kawaida ya afya. Tunaomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na aendelee na kazi zake kama alivyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu kwenye suala zima la uchambuzi wa bajeti. Wenzangu walizungumza jinsi bajeti ya Wizara hii ambavyo inaendelea kushuka siku hadi siku. Mwaka jana 2013/2014, Wizara hii iliidhinishiwa bajeti ya 7.9 bilioni ikiwa 7.2 bilioni ni fedha za kawaida na milioni 700 fedha ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, bajeti ya mwaka huu Mhe. Waziri ametuomba tumuidhinishie fedha za jumla bilioni 9.9 ambapo ukiangalia kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka huu, bajeti ya maendeleo imeshuka kwa asilimia 53. Kwa maana ya kwamba mwaka jana ilikuwa ni milioni 700, mara hii ni milioni 325.

Mhe. Naibu Spika, bajeti ya maendeleo ya mwaka huu imeshuka kwa asilimia 53. Ni kusema kwamba hiki ni kiashiria tosha kuwa hakuna la ziada la maendeleo kwenye Wizara hii badala ya watu kulipwa mishahara kama ilivyo kawaida. Hatuwezi kushusha bajeti ya maendeleo kwa asilimia 53 baadae Serikali ikajigamba kwamba kuna maendeleo yatakayopatikana kwenye Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini makusanyo mwaka jana yalikuwa ni bilioni 820 makisio, mara hii Mhe. Waziri ametwambia anakusudia kukusanya milioni 251 ikiwa ni punguzo la asilimia 69.4. Kwa hiyo hata yale makusanyo ambayo Mhe. Waziri mwaka jana aliyatenga yana upungufu wa milioni 569 kama asilimia 69.4.

Kwa hiyo ikiwa Wizara haina uwezo wa kukusanya, na makusanyo ya Wizara hii yalikuwa yanategemewa zaidi kwa wafanyakazi. Lakini Wizara imekiri kwamnba makusanyo yatashuka kwa asilimia 69, ni dhahiri kwamnba ufanisi wa Wizara hii kwa kweli umekuwa mdogo sana. Sababu ni zipi, Mhe. Waziri lazima atueleze kwa nini hata matarajio ya makusanyo yameshuka kwa asilimia 69. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri hili atueleze kwa nini fedha ya makusanyo imeshuka wakati vyanzo vya makusanyo haya bado vinaendelea na vinaendelea kushughulikiwa kama ambavyo Mhe. Waziri amesema.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine niende kwenye maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba ufafanuzi mwaka jana Serikali ilitwambia hapa ilitenga bilioni 17 kwa ajili ya nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi wa Zanzibar. Naomba kujua bilioni 17 zile ambazo zilitengwa kwa ajili ya nyongeza za mishahara ngapi zimetumika hadi sasa na ngapi zilibakia. Lakini pili, ni nani hasa aliyefaidika. Niliwahi kuwaambia walimu fulani hivi kwamba hii nyongeza nyinyi hamumo. Nyongeza ambayo ilitengwa na Serikali wafanyakazi wa kawaida iliwafikia kwa asilimia 25. Pamoja na kwamba wafanyakazi wote wa kawaida walipewa elfu 25 lakini ukiangalia mahesabu haya bilioni 17 ndio ningeomba kujua, hizi bilioni 17 za nyongeza nani hasa aliyefaidika. Ni wafanyakazi wote wa Zanzibar au ni wanasiasa na viongozi wakuu wa Serikali kama inavyosemekana. Kwa hiyo naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi huo ili niweze kujua hii bilioni 17 iliyotengwa ni nani waliofaidika.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye hoja ya unyanyasaji wa wafanyakazi, bado tumekuwa tukisema kwamba Kampuni ya *Zantel* inaendelea kuwanyanyasa wafanyakazi wa Zanzibar. Hili limezungumzwa miaka mingi ingawa hakuna hatua inayochukuliwa. Hivi sasa Zantel imeamua kupunguza wafanyakazi, lakini wamekuwa na malalamiko kwamba yale maslahi ambayo wameyafanyia kazi kwa miaka 10 au 15 walitaka kupewa fidia ambayo kwa kweli haistahiki. Mtu miaka 15 tumeambiwa kwamba atapewa fidia isiyozidi milioni moja na laki mbili. Kwa miaka 15 ametumikia Zantel leo anastaafishwa kwa kupunguzwa kazi lakini fidia yake ni milioni na laki mbili. Kwa kweli Mhe. Waziri naomba hili suala tupate majibu. Utaratibu wa ajira za wafanyakazi hawa na utaratibu wa kustaafishwa kwa nini maslahi yao yanakuwa madogo sana kwa muda wa miaka 15 ambao wamefanya kazi.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni wafanyakazi kunyanyaswa mimi nina mfano hai. Kuna mfanyakazi wa Chama cha Wafanyakazi alikuwa anafanya kazi Pemba, alihamishwa kuja Unguja kama zilivyo taratibu za kazi. Baada ya kufika Unguja akadai mafao yake gharama zile za kuhamishwa. Suala hili Mhe. Naibu Spika, limemchongea na jana kapewa barua ya kuachishwa kazi. Kwa hiyo mfanyakazi anahamishwa Pemba kuja Unguja, anadai haki yake kwa mujibu wa sheria anaambulia barua ya kufukuzwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, nitampa barua Mhe. Waziri baadae ili aone kwamba haki inatendeka. Ni kwa nini mfanyakazi anadai haki zake hatimaye anaambulia kufukuzwa kazi wakati Wizara ipo, kuna Idara inashughulikia maslahi ya wafanyakazi hakuna hatua inayochukuliwa mtu huyu anapata adhabu kwa kudai maslahi yake baada ya kuhamishwa kihalali kabisa. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, huu si utawala bora na hii sio kazi hasa iliyokusudiwa juu ya Wizara hii kwa ajili ya kufanya kazi hizi.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la E-Government. Mhe. Naibu Spika, ni kweli Serikali wametwambia kwamba mradi huu wa *E-government* ulitumia dola milioni 21 ambapo ni sawasawa karibu na bilioni 32. Mwaka jana hapa Barazani ilikuwa Kamati yangu yaFedha mimi ni kama Makamu Mwenyekiti, Baraza waliridhia Kamati iende ikafanye uchambuzi wa kina juu ya matumizi ya bilioni 32.

Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha niseme kabisa kwamba hatujafanya kazi hiyo ya uchambuzi wa fedha hizi. Kwa nini, kwa sababu gani, naomba liulizwe Baraza. Sisi kama Kamati hatujawezeshwa kufanya uchambuzi wa bilioni hizi 32 za matumizi ya mradi wa *E-government*. Kwangu mimi kama Mwakilishi wa kawaida niliamini kwamba hatuwezeshwi kufanya kazi hii kwasababu matumizi haya ni dhahiri kwamba yalitumika ambavyo si halali.

Kwa hiyo Kamati ilipokuwa inahoji matumizi haya ilikuwa kuna dharura nyingi, leo huyu hayupo, huyu kasafiri, subiri kidogo. Sasa hakuna uchambuzi ambao Kamati walifanya uchunguzi wa matumizi haya na kwa hiyo Wajumbe wakichangia wasije wakalaumu Kamati kwamba imefanya uchunguzi. Mimi kama sehemu ya Kamati hiyo hatujafanya uchunguzi wa fedha hizi ni lazima Serikali waturidhishe bilioni hizi 32 zilitumika vipi. Ninavyoamini mimi kwamba mradi huu wa E-*government* umefeli kwa kiasi kikubwa na ndio maana leo kila Wizara hapa wamewekewa portion maalum kwa ajili ya kusimamia E-Government. Ukiwauliza E-*government* wenyewe hiyo fedha ya jumla iko wapi, ufanisi wake hauonekani, lakini fedha imetengwa kila Wizara kiasi cha kuwaziba macho Wawakilishi tu kwamba waone kuna mradi wa E-*government.*

Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa ambazo tunazo Kamati ambayo imetembelea Kituo cha E-*government* pale Mazizini hata kompyuta 4 ambazo zimo mle ndani ya kituo ziliazimwa siku ile ambayo Kamati inakwenda kuona. Sasa mradi wa bilioni 32 kompyuta za kuwaonesha Kamati zinaazimwa siku ile hadi wananchi waambiwe kwamba mradi huu umeleta ufanisi. Mhe. Waziri leo anatwambia kuna E-*service* haiji kama hakuna hiyo E-*governmen*t. Tuambiwe kwanza hiyo E-*governmen*t yenyewe iko wapi, na nini ufanisi wake.

Mhe. Naibu Spika, mradi huu fedha hizi ni za mkopo kama ilivyo mikopo mingine Wazanzibari wataendelea kubeba mzigo huu wa deni lakini kwa kweli ufanisi wa mradi huu ni mdogo na Mhe. Waziri mwalimu wangu nadhani alipewa gunia ambalo ndani yake mna mambo ambayo hakuyafungua. Siwezi kumlaumu kama Mhe. Haroun Ali Suleiman lakini kwa kweli alipewa gunia ndani yake pengine mna bangi au mna mambo mengine ambayo hakuyafungua. Lakini hakuna mradi wowote wa E-*government* ambao ufanisi wake ulikuwa unaonekana.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala zima la ajira. Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie wazi wazi kuna suala la ajira kwa maana ya ajira rasmi na isiyokuwa rasmi, na kuna suala zima la *income* ambazo husaidia mapato. Sasa isijekuwa hizi shughuli ndogo ndogo za kiuchumi za kuuza maandazi, nyungo, kadi za simu Zantel zile ndio wenzetu wanaziita ajira na ndizo ambazo wanatusifia kwamba Zanzibar tumeajiri watu 2000.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 ya makaazi, sensa ambayo ni halali kabisa imepitishwa na Wazanzibari wamehojiwa. Zanzibar kwa sekta ya ajira ni asilimia 12.5 tu ndio ambao wameajiriwa. Kwa mujibu wa sensa hii ya 2012 asilimia 61 ni wakulima wa kijembe kongoroka, asilimia 19 wamejiajiri kwa shughuli ambazo sio za kilimo, kwa maana ya uvuvi na kuuza maandazi na mkaa, na asilimia 7 ni shughuli za kifamilia za kiuchumi.

Sasa unaposema kwamba umeajiri watu 2000 kwa mwaka najiuliza ni wepi walioajiriwa. Ni wale wanaouza nyungo barabarani, ni wale wanaotembea na vikoti vya Zantel kuuza kadi, ni wepi hasa. Na kama wameajiriwa hawa nini hatma yao. Kwa hiyo muajiriwa mzuri hasa ni yule ambaye hatma yake akifika umri wa kustaafu anapata maslahi ambayo yatamsaidia katika umri wake wa uzeeni. Hawa ambao wameajiriwa na Wizara hii ambao leo tumeambiwa wanaajiriwa kwa asilimia kubwa ni wepi hao. Ni wale ambao siku ya mwisho ya kustaafu kwao watapata maslahi, au ni wale ambao wanauza maandazi barabarani na kuuza nyungo. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atupe ufafanuzi, lakini kwa takwimu za sensa ambazo zipo bado suala hilo Zanzibar ni gumu sana na sababu ambazo zipo ni sababu ambazo kwa kweli lazima Serikali watuwekee wazi utaratibu wa ajira ambao Wazanzibari watapata maslahi kama Wazanzibari halali.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla alizungumza kwamba wananchi wetu wanaopelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kuajiriwa kwa kweli wamekuwa wakipata tatizo kubwa, mengine hatuwezi kuyasema hapa hadharani lakini wamekuwa wakilalamika sana kwamba wanakwenda kule kwa msingi wa kuajiriwa hatimaye wanakimbia ajira hizo kwa sababu kuna mateso makubwa ambayo yanawapata.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri afanye utafiti na awasikilize wafanyakazi wale waliopo nje ya nchi. Je, kweli wanafanya ajira zile kama ambavyo Serikali imekusudia au inakuwa ni sehemu ya kuwadhalilisha wale watu wanaokwenda nje ya nchi. Sehemu kubwa ya watu wetu wanaokwenda nje ya nchi kwa kweli wamekuwa wakilalamika kwamba ajira zinazopatikana kule ni ajira ambazo zinawakandamiza. Mhe. Waziri nikuombe sana ufanye utafiti pengine uwaite wale ambao wamerudi upate maelezo yao kwa kweli yatakusaidia jinsi gani huko wanapata tabu pale wanapokwenda nje ya nchi kwa ajili ya kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuna haja ya kufanya kazi ngumu ya kuchunguza mradi wa E-*government* wapi umefikia. Mhe. Haroun Ali Suleiman hata tukamsagasaga hana majibu ya kina juu ya mradi wa E-*government.* Amepewa Wizara juzi, watu wameshaharibu, huo ni ukweli. Na kama hakujaharibiwa mtu na aseme hakujaharibiwa. Watu wameharibu mradi mzima leo anatoa maandishi ambayo lazima aseme kama Waziri hamna kitu. Kwa hiyo Wawakilishi kama tupo makini kweli bilioni hizi 32 za dola milioni 21 ni fedha za Wazanzibari ambazo zimekopwa.

Mimi nasema mara zote kwamba jambo hili limekuwa ni tatizo kwa sababu Wawakilishi wenyewe ndio sisi, tumekuwa hatujali kusema kweli, watu wanaharibu fedha ukisema hapa basi mtu huyo anaonekana huyu ni adui, na yule asiyesema ndio anaonekana mtu halali kabisa. Kwa hiyo Mhe. Waziri hata tukamchambua kama karanga hapa hana majibu ya mradi wa E-*government.* Fedha imepondwa na hakuna ambacho kimefanyika ndio leo Mhe. Waziri anatuandikia ana mradi mpya wa E-*service*.

E-Service Mhe. Naibu Spika, lazima kuwe na E-Government ambayo imekamilika. Kwa kweli haikukamilika na kama imekamilika Serikali itupe maelezo vipi mradi huu ufanisi wake umefanyika.

Ninachoamini mimi Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wameendelea kupewa deni kubwa la mkopo huu bila ya ufanisi kama ambavyo watabeba deni la mradi wa Uwanja wa Ndege na miradi mengine ambayo Wazanzibari wameshuhudia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi niseme kwamba nitaunga mkono hii hoja. Kwa sababu naona hata nikiikataa Mhe. Waziri nitampa tabu bure, hana majibu ya ziada, jambo ambalo yeye mwenyewe hakulifanya huwezi kumhukumu. Kwa hiyo naunga mkono hii hoja nikitegemea kwamba atanipa uchambuzi wa jambo moja tu la matumizi ya bilioni 17 ya nyongeza za mishahara ambayo Serikali waliitenga. Nijue ni nani ambao walifaidika. Ikiwa wafanyakazi wa kawaida walipewa hiyo 95, hizi bilioni 17 zilikwenda kwa nani. Ni Wawakilishi, ni Wakurugenzi au nani walipewa bilioni 17 naomba kujua hivyo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu katika hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, sina budi pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri, lakini vile vile na kumuombea dua kwa Mwenyezi Mungu ili azidi kupata afya njema na aweze kushirikiana nasi zaidi katika kuendeleza maendeleo ya kuisaidia nchi yetu na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo nina mchango katika sekta moja tu ndani ya kitabu hichi. Wenzangu wamekwisha kutangulia wakazungumza mengi katika maeneo mbali mbali. Lakini mimi nakuja katika ukurasa wa 29 kifungu cha 52 Idara ya Ajira.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nakuja hapa kutaka kuja kuchangia hoja hii nilianza kufanya tafiti katika vitabu vilivyopita. Mhe. Naibu Spika, naomba unipe fursa ili tujikumbushe hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ya mwaka 2011/12 naomba kunukuu.

"Mhe. Spika, Idara hii ni mpya na ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa sera ya ajira, mpango wa kuzalisha ajira, pamoja na kubuni na kusimamia mipango na taratibu za soko la ajira zitakazohakikisha fursa za ajira zinapatikana kwa usawa na kwa wote wanaohitaji. Pia Idara hii ina jukumu la kufanya tafiti kwa ajili ya kuendeleza sera, mikakati na mipango mbali mbali ya ajira, kuanzisha na kusimamia mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na uwekaji wa taarifa za soko la ajira na kusimamia ajira kwa wataalam wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini Zanzibar."

Mhe. Naibu Spika, juzi nilikuwepo kitini hapo nilikuwa na hamu sana ya kuchangia katika Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, lakini kutokana na majukumu mengine ambayo ilikuwa umenipatia ikanibidi nichangie kwa maandishi. Katika Wizara ile Mhe. Naibu Spika, nilitaka kufahamu nini maana ya utawala bora, lakini pia nilitaka kufahamu misingi ya utawala bora. Kwa bahati nzuri Mhe. Waziri alipokuja kufanya majumuisho alitusaidia baadhi ya tafsiri na akatusaidia muelekeo halisa wa malengo na madhumuni ya utawala bora.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi napata kigugumizi kidogo kuna baadhi ya mambo ninapoyaona. Matarajio na muelekeo wangu ni kwamba inapokuja kusomwa bajeti ya mwaka huu na kupitia mapitio ya mwaka uliopita, ni matarajio kuona kwamba mwaka uliopita Serikali ilijikita kufanya moja, mbili, tatu. Na mwaka unaofuata ni kuweza kupata kwamba tulifanikiwa kufanya tatu, nne, tano lakini sita, saba, nane imebakia matarajio yetu tunatarajia labda kumaliza hili, lakini tuna mpango wa kufanya tisa, kumi, kumi na moja katika mwaka unaofuata.
Nashindwa kufahamu ninapoona kwamba mambo yale ambayo yamepita katika siku za nyuma ni yale kwa yale yanakuwa yanajirudia na kujirudia. Hapa mimi nakuwa napatwa na mashaka.

Nilijaribu kufanya utafiti zaidi nimesoma kitabu hichi cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2013 na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar 2013/14 kitabu cha kwanza. Hapa pana maelekezo Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu;

"Kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2013/14 katika hiyo sekta ya ajira. Kufanya ukaguzi kwa taasisi 240 ili kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ikiwemo kupambana na ajira ya watoto. Kununua gari moja kwa ajili ya shughuli za ukaguzi, kufanya mkutano mmoja wa wahusika ili kupitia taarifa za utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO). Kushiriki katika mikutano na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mikutano na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani. Kukusanya mapato kutoka kwenye vibali vya

kazi na mikataba ya kazi. Kuandaa na kurusha hewani baadhi ya vipindi. Kuanzisha na kuendesha shughuli za usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kikazi. Kufanya mikutano minne ya bodi na mambo mengine. Kufanya mikutano miwili ya utatu, kufanya mikutano miwili ya kamati ya wataalamu na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba vijana wetu Zanzibar wamekuwepo hapa muda mrefu wakihangaika wanatafuta sehemu za kuweza kufanyakazi, ili waweze kujiendeleza kimaisha. Mhe. Naibu Spika, lakini bado mimi sijaona mipango na utaratibu makini wa kuweza kuwasaidia vijana wetu wa Zanzibar, hususan wale ambao wamemaliza elimu zao ikiwemo elimu ya msingi katika kutengeneza utaratibu ulio bora na makini kuwasaidia, ili waweze kupata ajira sehemu za kazi maeneo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia katika kitabu hiki nakuta kwamba serikali ilikuwa na mpango wa kufanuya ajira 2,000 kwa mwaka ambao unamalizika sasa. Tumefanikiwa kupata ajira 1600 na zaidi kwa vijana wetu ambao walikuwa wamekwenda kuomba kazi katika maeneo mbali mbali. Kinachonishangaza na kunisikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hizi takwimu zinanipa mashaka kidogo, nikitizama katika kitabu hiki cha mpango wa maendeleo, nimekuta utekelezaji halisi. Mwanzo katika kitabu chetu hiki cha bajeti kulikuwa kuna mpango wa kuweza kuzifanyia utaratibu taasisi 240 kwa mwaka uliopita. Lakini zilizoweza kutekelezwa ni taasisi 60, ambapo ni chini ya asilimia 50 ya malengo ambayo serikali ilikuwa imejipangia.

Sasa je, Mhe. Naibu Spika ni nini kilichosababisha kutokufikiwa kwa malengo ya haya mbao yaliyokuwa yamepangwa na taasisi hii, juu ya kuhakikisha kwamba utekelezaji wa sheria hizo unakwenda sambamba nakuweza kutoa tafsiri na kuondoa matatizo ambayo yanawakabili wale waajiri na waajiriwa katika sekta zetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo na kwenda katika eneo la vijana hasa. Katika kitabu hiki cha mpango wa maendeleo, ukurasa wa 129 vijana 37 wanaotafuta kazi wanawake 11 na wanaume 26 wameorodheshwa kwa ajili ya kuunganishwa na ajira. Kati ya hao vijana 13 wenye ngazi ya shahada ya kwanza wameunganishwa na Kampuni ya Tigo.

Vile vile vijana 168 wanaume wamepata fursa ya kufanyakazi katika kampuni ya mabaharia ya DANAUS. Aidha, vijana 273 wamepata nafasi ya kazi nje ya nchi katika nchi za Djibouti, Oman, Qatar, Saudi Arabia, *UAE* kwa kupitia mawakala binafsi. Sasa Mhe. Naibu Spika, nikiangalia takwimu hizi ambazo zinatoka katika mpango wa maendeleo, nikiangalia na maelekezo ambayo yamo katika kitabu chetu cha bajeti. Mimi naanza kupata mashaka na naona kwamba ile *seriousness* ya kuwasaidia vijana katika kupata ajira ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar hapa inakosekana.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu cha bajeti, huku kuna vijana waliopatiwa ajira na 410, wakati katika mipango huku kuna 168, hapa kidogo naanza kupata mashaka. Hawa ni watu ambao wamefanyiwa utaratibu katika Kampuni ya DANAUS, 410 lakini 168 katika kitabu cha mpango wa maendeleo. Halafu vijana 859 wamepata nafasi katika nchi za nje, wakati huku kuna vijana wako chini ya kiwango hicho, huku kuna 273. Sasa ukiangalia hivi vitabu vyenyewe vinagongana, sasa sijui huu umakini wa kuweza kuwa na imani kwamba vijana hawa watasaidiwa ili waweze kupata kazi inakwendaje. Hapa mimi naanza kupatwa na mashaka.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona kwamba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie hasa na atufahamishe mikakati ambayo itakuwa inaweza kuleta matumaini ya kuona kwamba vijana wetu wanasaidiwa na wanapata kufahamu utaratibu mzima wa kuweza kupata kazi katika maeneo haya.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu mimi kila siku ya Mungu kinanipa matatizo. Pale tunapokuja kupitisha miswada yetu hapa ya sheria hapa ya sheria katika sekta ya kazi na hususan pale tunaposema kwambwa ili uajiri ufanyike basi upatikane uzoefu wa miaka mitano ndipo mtu aweza kuajiriwa. Kusema kweli kipengele hiki katika miswada na sheria zetu ni kipengele ambacho mimi nahisi ni kikwazo, katika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaweza kupata ajira katika nchi yetu.

Kama hiyo haitoshi, vile vile Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hapa naomba atusaidie katika utaratibu mzima unaotumika juu ya utaratibu wa kuweza kuongeza vipindi vya kazi, baada ya muhusika kumaliza kipindi chake cha kazi na kuweza kupewa nafasi nyengine ya kujaza mkataba mpya wa kazi na kuendelea na shughuli za kazi.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, na kwa namna ambavyo Mhe. Waziri atakapo kuja hapa na kuweza kunijibu maombi yangu, maswali yangu pamoja na hoja zangu, nitaendelea kuunga mkono hoja ya wizara hii kwa asilimia mia na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu, vile vile tutapitisha bajeti hii kujibiwa mambo ambayo nilikuwa nataka ufafanuzi wake. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa na mimi fursa hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma.

Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia afya njema na uzima na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili. Pia napenda nichukuwe fursa hii kumuombea dua Mhe. Waziri kwa maradhi yaliyompata kidogo, Mwenyezi Mungu amjaalie amzidishie afya yake, ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kama vile tulivyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nimpongeze waziri na watendaji wake kwa juhudi kubwa wanayochukua katika kuona wizara hii kwa kiasi fulani inafanikisha majumu yake waliopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi naanza kusema kwamba naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia na nawashauri na wajumbe wenzangu waiunge mkono hii hotuba ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nikianza na mchango wangu mimi, sitokuwa na mchango mkubwa sana, kwa sababu ni miongoni mwa wajumbe wa kamati tunaosimamia Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma. Kwa kutilia mkazo tu nitaweza kutoa mchango wangu mdogo.

Kwanza nianze na Idara ya Mipango Sera na Utafiti katika utekelezaji wa malengo yao, walizungumzia suala zima la mfuko huu wa bima ya afya. Katika kifungu cha 4 hiki walisema;

> "ripoti ya usarifu wa awali ya mfuko wa bima ya afya imeandaliwa, ripoti hiyo inajumuisha mapendekezo ya makundi yatakayofaidika"

Kwanza niwapongeze kwa hatua hizi wanazochukua, lakini kwa faida ya wananchi na faida ya Baraza hili naomba watupe ufafanuzi kidogo ni makundi gani haya yatakayofaidika na mfuko huu wa bima ya afya, kwa sababu hili suala limeshakuwa la muda mrefu mpaka kufikia watu kutoa matumaini kuwa halishughulikiwi. Sasa watakapotupa mchanganuo kidogo kwa faida ya wananchi wetu na wajumbe wa Baraza hili basi wataweza kufaidika na maelezo haya.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili ni suala la mishahara. Suala la mishahara halijawa na mfumo madhubuti na ndio maana ikapelekea watu kuwa na mashaka katika ulipaji ya mishahara. Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo ambalo limejitokeza kwenye taasisi za serikali, kuhama watenedaji wa serikali kuhamia mashirika mengine.

Mhe. Naibu Spika, suala hili lipo na watu zaidi ni kutafuta maslahi. Mhe. Naibu Spika, tukumbuke kuwa mtu yule anapoajiriwa pale, serikali inachukua gharama ya kumsomesha mtu yule ili aweze kuwa na ufanisi zaidi katika kazi zake. Baada ya kuona maslahi yaliopo pale ni madogo basi huweza kuondoka na kwenda kwenye taasisi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti yetu ya kamati, sio taasisi binafsi tu, lakusikitisha zaidi ni mfanyakazi yule kuondoka kwenye taasisi ile ya serikali na kwenda kwenye shirika, lakini ni lile lile la Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sasa hili ni tatizo, kuwa unapokuwa kwenye taasisi ya serikali na mtu anapokuwa kwenye shirika la Serikali hii hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, pengine elimu zao ni moja lakini mishahara yao inapishana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili ni tatizo na inatakiwa serikali iliangalie kwa makini sana, ili wizara isipate tabu ya kusomesha watu halafu wakaondoka na kwenda kwenye mashirika mengine kwa kufuata maslahi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine katika idara ya uendeshaji na utumishi, malengo ya mwaka 2013/14 lengo la pili ni kuimarisha usalama wa majengo na mazingira yanayoizunguka wizara. Mhe. Naibu Spika, niwapongeze ni kweli

kuwa majengo yanayolizunguka jengo lile pale kwa asilimia kubwa ni mabovu. Lakini wasije wakageuka wale ngariba wa Chambani, kwa sababu na jengo lao na wao ni bovu, kwa hivyo waweze kulifanyia ukarabati.

Tulipokwenda kwenye kamati mara moja tuliibaini ile ngazi pale inapasuka, kwa hivyo majengo ya pale takriban yote yana matatizo. Kwa hivyo, wasiyafanyie matengenezo majengo yaliyoizunguka wizara tu, lakini pia waangalie na wizara yao.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni kuhusu Idara hii ya Nyaraka kama tulivyosema kwenye ripoti yetu, Mhe. Waziri atueleze kuwa ni taasisi au ni idara ya nyaraka. Bado katika idara hii changamoto zipo na moja katika malengo yao ya mwaka 2013/14, lengo moja ilikuwa ni kununua mtandao wa *CCTV* pamoja na kulifanyia matengenezo madogo madogo ya jengo. Katika malengo ya mwaka huu bado sijaona kuwa chombo hiki tayari kimenunuliwa au hakijanunuliwa. Pia ufinyu wa bajeti katika taasisi hii umekuwa ni mkubwa kiasi ambacho kinaondoa matumaini, na kwa sababu taasisi hii inajukumu la kusimamia idara nyengine za serikali zote, ili kufanikisha lengo la kuweza kuweka kumbukumbu katika taasisi za serikali.

Mhe. Naibu Spika, taasisi nyingi za serikali zina matatizo ya utunzaji wa kumbukumbu. Sasa ikiwa Mkurugenzi huyu hakuwezeshwa katika idara yake au taasisi yake, sidhani kama atakuwa na uwezo wa kufikia hilo lengo tunalokusudia.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna agizo ambalo tulilitoa kwenye maagizo ya kamati namba 5, kupatiwa usafiri ili kuweza kumpunguzia kazi Mkurugenzi huyu kwa kutembelea wizara nyingi katika kufanya utafiti wa ukusanyaji wa kumbukumbu. Wizara walituambia kwamba shauri hili limepangiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/15, lakini ndani ya kitabu hiki sijaona eneo lolote ambalo linazungumzia kuhusu ununuzi wa gari hii. Mhe. Waziri nakuomba kwa sababu idara hii ya nyaraka ina jukumu kubwa la kuweza kutoa taaluma kwa Unguja na Pemba.

Kwa hivyo, iwapo idara hii itakuwa na ufinyu wa bajeti kama tulivyoieleza katika ripoti yetu, basi itakuwa hakuna kitakachoendelea na bado tutaendelea kusumbuka wakati tunapotafuta kumbukumbu katika taasisi za serikali na kumbukumbu zile zikawa hazionekani.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya Ajira. Kwanza nichukuwe fursa hii kuwapongeza kwa kuweza kuwapatia vijana 410 fursa ya kupata kazi kwa kupitia kampuni mbali mbali, kama walivyoeleza katika kitabu hiki.

Mhe. Naibu Spika, hizi ndizo kazi ambazo vijana wetu kwa wingi watapata ajira. Tukitegemea kuwa sote tuajiriwe na serikali hii basi hili litakuwa ni tatizo na tutakuwa hatufikii malengo yale tunayokusudia. Ni lazima kuwe na ajira nyengine ili wanachi wetu au watoto wetu waweze kupatiwa ajira hizo. Kubwa ni kuwa na mikataba ambayo itawalinda mikataba ile. Huko wanakokwenda kufanyakazi ikiwa ni nje ya nchi au ikiwa ni ndani ya nchi, kwa sababu wengi ajira wanazozipata ndizo hizo hizo.

Mhe. Naibu Spika, tuchukuwe mfano mmoja wa kampuni hizi zinazokuja, kampuni hizi tuseme zikija kama hapa Zanzibar, basi watu wengi kampuni hizi zinapokwenda kufanyakazi popote wao wanajua kuwa kampuni hii imekuja hapa kufanyakazi, lakini wananchi wetu kwa sababu hawana taaluma basi wanajua wasimamizi wakuu ni serikali au inayofanyakazi hapa ni serikali.

Tatizo lililopo, kampuni hizi badala ya kuhatilifiana na wananchi pengine kukosa kulipwa mafao yao kwa zile kazi ambazo wanafanya, basi serikali au wizara inashindwa kusimamia wananchi wale kuweza kupatiwa haki yao. Wizara wanakataa au hawawatendei haki wananchi kwa kusema kweli Mhe. Waziri mimi nataka nitoe mfano mmoja ulio hai kulikuja kampuni moja ya NGOGO iliyokuja kujenga soko pale Tumbe, hatimae kwa sababu wananchi wetu na siku zote tunalizungumza suala hili ni watu wanaotafuta rizki kila upande wakashirikaiana na kampuni ile. Kampuni ile haikuja na wafanyakazi pale isipokuwa wafanyakazi walikuwa wanatoka pale maeneo ya kijiji kile walichokwenda, lakini hatimae walifika hadi mpaka leo wakashindwa kuwalipa pesa zao walizofanyia kazi.

Wizara ya Uvuvi ndio waliokuwa wakijua jukumu hili na kampuni hiyo waliileta wao lakini walishindwa kusimamia Wizara wananchi wale kulipwa haki zao, kwa hivyo hii hawatendei haki wananchi na watu wengi si kwa sababu wana taaluma ya kujua kuwa hawa ni wakandarasi wanakuja hapa, lakini wao wanalipwa na Serikali sisi watulipe wao kwa hivyo lazima tuwekeyane mikataba wao hawajui hiyo.

Serikali au ile Wizara inayohusikana wao ndio wanaokijua kile sasa wajibu wao waendelee kuwashughulikia wananchi wale, ili kupata haki yao, lakini Mhe. Waziri hilo linashindikana na halifanywi na wananchi wetu kwa kweli wanasikitika, likija likitokea tokeo hapa pengine wananchi wale kuchukua hasira kwenda vunja jengo lile au kusema jengo hili hapafanywi chochote hapa sasa wao wataonekana kama wavunja amani nchi hii. Lakini kumbe wao Serikali haiwajali kwa sababu kama inawajali wao Wizara haikushindwa kuwasimamia kampuni ile kuweza kuwalipa haki zao. Kwa hivyo Mhe. Waziri mikataba ni kitu kizuri ili wananchi wetu wasiweze kutumwa kiholela.

Jengine ni Kamisheni hii ya Kazi, Mhe. Waziri amesema hapa katika kupunguza ajira mbaya za watoto jumla ya watoto 631 wametolewa katika ajira mbaya na kurejeshwa skuli na kupatiwa vifaa vya masomo, nalo pia niwapongeze kwa sababu watoto waliomo katika ajira mbaya ni wengi na kuna Mawilaya yamezidi kuwa na watoto hawa, sasa hili Mhe. Waziri kwa faida ya wananchi na kuomba watoto hawa 631 uje unieleze.

Kwa sababu Wilaya yangu inaongoza kwa watoto wenye ajira mbaya kwa hivyo naomba uje unieleze katika Wilaya yangu ni watoto wangapi waliotolewa katika ajira hizi mbaya, lakini pia wazazi wao mumewaandalia mpango gani ili watoto wale si ile tu kupewa sare na kurudi skuli. Wale wazazi wao wanatakiwa na wao wawezeshwe ili kuweza kumudu wale watoto wao na kuweza kuwahudumikia ili wasije wakarejea tena katika ajira hizi mbaya.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache narudia tena kusema kuwa naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia nakushukuru Naibu Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kimsingi mimi leo sina maneno mengi isipokuwa natia tia nyalio tu. Kwanza nitumiye fursa hii kumpa pole Mhe. Waziri kutokana na ugonjwa ambao ulimpata katika kipindi kilichopita kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi, tunakupa pole sana, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akuimarishie afya yako, kusudi tuendelee kuwa nawe hapa.

Sisi katika Baraza hili Mhe. Waziri tunakuchukulia kama zizi kwa sababu ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokotea zizini kusaidiwa, kwa msaada tunaoupata kutoka kwako mara nyingi tunakuhesabu ni kama zizi la wawakilishi wengi tuliomo humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hilo nimpe pole vile vile Mhe. Waziri kutokana na hii Wizara aliyopewa hii, hii Wizara uliyopewa Mheshimiwa kwa kipindi kirefu ilikuwa na mambo mengi ambayo kwa kweli kuwepo kwake inaweza kuchafua taswira nzuri na utendaji wako makini ambao unao kwa kipindi kirefu, lakini niwaambie tu waheshimiwa Wawakilishi kwamba mara nyingi dhahabu thamani yake haibadiliki kwa kuiweka kwenye tope. Naamini Mheshimiwa utajitahidi kupapatua kusudi ili hii Wizara tuione inyooke kama tulivyoiona Wizara ya Elimu siku zile.

Mhe.Naibu Spika, nianze kuhusiana na muundo mzima wa utumishi katika nchi yetu muundo wa utumishi sio rafiki kwa wazawa hata chembe, yaani muundo huu katika muundo uliopo sasa katika nchi yetu sio rafiki kwa sisi wazawa, inasikitisha sana kuona muundo wa utumishi katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa unanufaisha sio kwa kiasi kikubwa lakini kwa kiasi fulani wageni zaidi kuliko sisi wazawa, tofauti sana mimi nimefanya kazi hizi katika nchi kadhaa na mwenzangu hapa Mhe. Salim tulikuwa tunafanya utafiti katika nchi kadhaa duniani zikiwemo zile za Ulaya, zile la Amerika, na hata hizi nchi zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara pamoja na zile UAE *cantries*, tukaona kwamba katika mtandao mzima wa ajira katika nchi zao mwelekeo mkubwa unalengwa kwa wazawa wa nchi, kabisa kabisa Mheshimiwa.

Mimi juzi juzi pale Oman nilikuwa katika tafiti zangu hizi hizi, nikaangalia Muoman ambaye sasa yupo lakini alizaliwa pale Viotngoji Umangani, lakini mama na baba yake walipohama huyu wakamchukua, lakini alizaliwa Vitongoji pale Pemba Umangani akaenda zake Oman baada ya kufika yule mzee akazaa mtoto mwengine kule Oman, kwa kutumia mama yule na baba yeye. Lakini katika suala la ajira yule waliyemzaa Vitongoji na kumpeleka pale Oman alikuwa hapati fursa, alikuwa sio mtwana na badala yake alikuwa ni mgeni na alikuwa hapati *facilities* anazozipata yule aliyezaliwa pale ingawa ni mama na baba mmoja.

Sasa tuone jinsi ya wenzetu wanavyothamini uzawa na bado hii nimeona ki- *country* je, katika hizo *democratic* tuangalie sana Mhe. Waziri katika hili, leo inasikitisha sana kwamba soko la ajira katika nchi yetu wananufaika zaidi Wakenya katika mahoteli pale. Sisi unamkutia Mkenya ni Hotel *Administrator* wakati sisi kuna Mvitongoji, kuna

Mtumbatu ana *Masters* au *Degree* ya mambo haya ya *Hotel Management* na mambo mengine hachukuliwi anakwenda kuchukuliwa Mkenya.

Aidha, unamkuta mfyeka majani pale kachukuliwa Tanga, kachukuliwa Morogoro wakati Mtumbatu yupo anaweza kukata majani na Mpemba yupo pale anaweza kukata majani hapati ajira hii, ni tatizo. Sasa Mhe. Waziri hebu utakapaokuja hapo nielezee ni nini kipo. Mimi nilikuwa nadhani katika wawekezaji wanavyokuja ile wanaiita MU *Memorandum* of *understanding* ya kila *project* inayokuja hapa basi ilibane zaidi soko la ajira, ili ajira zao ziwanufaishe vijana wetu.

Hii itaisaidia sana Serikali kupunguza wimbi hili la vijana kufuata mambo haya, kwa sababu wakishakuwa hawana kazi hawa wanajiingiza katika madawa ya kulevya, wakishajiingiza katika madawa ya kulevya hawamalizii hapo wanajiingiza katika mambo yanayoweza kupelekea mambo ya ukimwi, jambo ambalo hata Dk. Sira Mamboya anaweza kupata matatizo kufikia pale 0.3, Dk. Sira Mamboya ambae ananiangalia kwa jicho la husuda.

Mhe. Mwenyekiti niendelee Mheshimiwa kwamba ikiwa hatukuwa makini katika hili basi acha na vijana wetu kuwa na ajira, acha kuwa na matatizo mengine lakini tutapata tatizo hili nililolisema kwamba vijana wetu watajiingiza katika mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nije katika maslahi ya Watumishi, Mheshimiwa maslahi ya watumishi katika nchi yetu mara nyingi hutegemea uzoefu wa kazi, kiwango cha elimu na nyongeza inayotolewa na *headache state.* Kiongozi wa nchi pale katika hafla mbali mbali, maana sisi hapa mara nyingi kiongozi wa nchi katika sherehe za kuadhimisha mambo yetu haya ya Mapinduzi hutoa *statement* ya nyongeza ya mishahara. Anapotoa agizo Rais sioni kama kuna pingamizi ya kamisheni gani sijui kudharau dharau kabisa kabisa amri ya Rais. Leo nasikitika kwa taarifa nilizokuwa nazo Rais alitoa agizo la Wafanyakazi wa nchi hii kuongezwa mshahara, lakini mpaka jana nafuatilia fuatilia kuna Wizara hii hawa jamaa wa ZBC kule Pemba au sijui ni ZBC wote, lakini kule Pemba hadi leo hii hawajapata ile nyongeza aliyosema Rais. Sasa Mkuu wa utumishi wewe ndio tunaambiwa ndio kila kitu pale, utatueleza nini utakapokuja hapa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo jengine na usumbufu mkubwa unaopatikana hapa kwa watumishi wa Serikali ni pale wanapomaliza elimu ya juu kwa jaili ya kurekebishiwa maslahi yao, hawa wana tatizo kubwa Utumishi mna tatizo mimi sijui ni chombo hasa pale Pemba sijui ni chombo cha Ofisi yako ya Pemba Mheshimiwa Waziri, au ni hasadi tu au uadui au roho mbaya za watumishi wake kuna Mheshimiwa katika Ofisi yako pale Pemba kuna kijana Ali Khamis yeye ni *Cashier* katika Wizara ya Elimu ana *Mastars Degree* ya mambo ya *management of finance* huu ni karibu mwaka kafanya mambo hayo katika chuo kimoja hapa Dar es Salaam sijui ni IFM hapo Dar es Salaam, Mhe.Waziri Afisa Mdhamini aliyekuwepo Pemba hajamrekebishia huyu mfanyakazi wangu maslahi yake, ameshapata elimu hii.

Mhe. Waziri nataka nikuulize hii ni hasadi, huu ni uadui, au hii ni roho mbaya ya watumishi wako pale Pemba. Kama ni uadui basi naomba upambane nao Mhe. Waziri wewe una *high qualities* kama ni ujinga basi nadhani hawastahili kuwatumikia wananchi waliopo katika visiwa hivi, waondoshe.

Mhe. Waziri ni tatizo sana Ofisi yako ina roho mbaya vibaya sana, ile Ofisi uliyopewa mara hii kuna walimu wa *TAP Teachers Advancement Programme,* ile waliyopata mafunzo kule, *Wallahi laadhimu* huu ni mwaka wa tano nimesema Mheshimiwa humu nimewatetea walimu wenzangu. Mimi ni mwalimu tena sio mwalimu kama nakwenda kusomesha tu ni mwalimu *by profession* katika masuala ya *Biology, Chemistry with education*. Nimewatetea walimu wenzangu humu mpaka nikaumwa, nikalazwa Al-Rahma hapa kwa kupiga makelele humu ndani. Siku kadhaa nimekwenda Al-Rahma kutokana na kwamba serikali haisikii nikatetea wee, nikatetea wee mpaka nikapata matatizo ya sukari, nikalazwa Al-Rahma hapo.

Mheshimiwa mtatuua nataka leo unambie kwamba barua imeshapelekwa huu ni mwaka wa ngapi katika Ofisi yako Mhe. Waziri, na hadi leo hii walimu wa *TAP* wale waliosoma *TAP* na wale wakufunzi sijui ni walimu vile vile waliowasomesha wale walimu hadi leo hii mafao yao hawajalipwa. Hapa leo katika jambo ambalo sithubutu kufanya mie ni kukuzuilia kifungu nakuheshimu sana mwalimu, nakuheshimu sana sio kosa lako hili lakini umebeba jeneza ambalo huku nje ni zuri lakini ndani mna maiti.

Umemebebeshwa jeneza sasa Mheshimiwa utakapokuja nakuheshimu sana na wala maneno haya nisingependa niseme kwa sababu hivyo ukiniangalia mimi naona haya nimeinamia chini, lakini nalazimika niseme, "lisilo budi hutendwa".

Sasa Mheshimiwa ikiwa walimu hawa hawakulipwa basi bajeti hii leo itakuwa ni jino kwa jino hapa nitaizuia Mheshimiwa, au unipe lugha itakayoniridhisha. Nakuheshimu Mheshimiwa usiniangalie nakuonea haya, uje uniambie niridhike ni kwa nini hawa walimu mnawasumbua, hawa walimu wamesoma kipindi chote hiki hamjawalipa *justice delaying justice denied* haki ikichelewa kutolewa Mhe, Naibu Spika, ni sawa sawa na kwamba haikutolewa kabisa, mwaka wa tano hawa mnaendelea kuwadhulumu nataka *reason behind* ya hilo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwanza niipongeze Serikali kwani katika ukurasa wa 44 wa hiki kitabu naomba Mheshimiwa uniruhusu nikinukuu, ukurasa wa 44 katika ibara ya 73(1) kwa heshima kabisa Mheshimiwa naomba uniruhusu ninukuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14 Kamisheni imetekeleza malengo yafuatayo, sasa nanukuu hiki kifungu kidogo 73(1) *" ilifanya mikutano 22 iliyojadili na kutoa uamuzi kuhusu masuala mbali mbali katika utumishi wa umma na kuidhinisha miundo ya utumishi mitatu ambayo ni taasisi ya Karume ya Sayansi na Techonologie, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na Idara ya Mahakama".*

Kwa hivyo nataka kwanza nije hapa kwenye Idara ya Mahakama na kwanza niipongeze Serikali Ofisi yako kuweza kupeleka huu muundo katika Idara ya Mahkama ambapo ni miongoni mwa mihimili mitatu ya nchi, katika hili Mheshimiwa niwapongeze kwa kuweza kuinua mafao hasa ya hawa majaji na mahakimu wetu katika ngazi za Wilaya na Mikoa, lakini mumesahau wafanyakazi wa chini wa mahakama hususan hawa matarishi, hawa madereva, pamoja na makarani. Hawa mumewasahau nataka ukumbuke kwamba Jaji ambaye maslahi yake yametononoka vizuri hawezi kufika akakalia kiti chake cha ujaji kama hajaendeshwa na dereva, kama hajapelekewa mafaili na karani, kama kesi anataka kuhukumu haijasomwa na karani. Jaji hawezi kufanya hivyo mpaka asomewe kesi namba, faili namba, isomwe kesi ndio aisikilize.

Inasikitisha sana kwamba mtu wa sampuli hii karani wa Mahkama hamkumuangalia tena kwa kuanzia ya mwanzo mpaka Mahkama ya Wilaya naona hali ni mbaya sana ya kimaisha Mheshimiwa inasikitisha sana. Kwa hivyo mimi nadhani katika muundo mlioutoa musiwaangalie hawa mahakimu na majaji tu, tarishi, ili hakimu aweke *court order* lazima ile *order* yake ichukuliwe ipelekwe kwa mlengwa anayepeleka ni tarishi, ili hakimu *court order* isibu pale anapopataka lazima apewe tarishi.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Hizo zitanitosha Mheshimiwa. Sasa inaoenekana matarishi mumewasahau, makarani mumewasahau, *this is a biasness* Mheshimiwa musiwe *bias* katika kuendesha nchi. Nchi hii ni yetu sote bila kujali taaluma, kiwango cha elimu au mtu alipo, hawa makarani, hawa matarishi wa mahkama, hawa wakata majani wa mahkama nao ni watumishi na ni wazanzibari na wao wapeni maslahi yao.

Mheshimiwa, niangalie katika kitengo kila cha uhasibu, huku ndio mmebagua zaidi. Mheshimiwa Mhasibu aliye na digrii ya mwanzo ambaye yuko Wizarani na Mhasibu mwenye *Master Degree* aliyeko kwenye Idara, basi huyu mwenye *First Degree* au *Diploma* anamshinda, hawa waliopewa kwenye Wizara wana 1.53 milioni yaani 1,530,000 wanapokea kwa mwezi. Huyu aliyekuwa Idara nitoe mfano ili wanasiasa wenzangu wanifahamu, kwa mfano hii Wizara tuliyoko sisi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, yule Mhasibu aliyepo pale Ofisini ndio anaye-*enjoy influence* ya 1.53 milioni. Lakini Mhe. Spika, Mhasibu hapa wa Baraza la Wawakilishi ana digrii mbili yule kule ana digrii moja tu, huyu wa Baraza la Wawakilishi hazidi laki tano Mheshimiwa *what does it mean*? Utakapokuja hapa unifafanulie kwa kina Mhe. Waziri ni kigezo gani mlichotumia nyinyi serikali, watu wa kada moja *same profession* wakawa wametofautiana katika madukhuli.

Ni sababu gani ya kimsingi au ni katika ubaguzi baguzi tu hivi. Na hii Waziri ukija nataka unieleze hili agizo alilitoa nani la kwamba hawa muwalipe 1,500,000, hili lilipita hapa Barazani au mlikaa mkaamua huko au ni Waziri wa Fedha tu alisema, nataka hapo tueleze. Na likija toleo mtuletee ili tuweze kujua, maana yake mnatuumisha kichwa sana.

Mimi nilikuwa ninaishauri serikali sana Mhe. Waziri katika hili, ili tusije tukapoteza watalaam wetu, basi hii *national cake* iwe *equally distributed according to the academic performance* na mambo mengine kama vile uzoefu. Lakini mkisema nyinyi mnatoa fungu mnampa huyu, huyu hamumpi huo ni ubaguzi uliobobea na mimi katika hili sitounga mkono hata siku moja.

Nadhani kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ushaanza kuniangalia angalia muda umemalizika nitaunga mkono hili, mpaka pale mwalimu wangu, Mwalim Haroun atakapokuja kunijibu ni kwa sababu gani watu wa CAG wale ambao ni *external auditors,* wana *Degrees* nyingi kuliko hao wahasibu wake wapate laki tano na wale wapate 1,5000,000, aje anieleze CAG *auditors* ambapo ni *watch dog* wa *public fund* wapewe hela ndogo, hawa wapewe hela nyingi hawa makarani wa kawaida, uje unieleze.

Vile vile nyie mnapopelekewa ofisi zetu Mhe. Waziri mnapopelekewa maombi ya wafanyakazi kwamba Wizara inataka wafanyakazi, basi muwajibu haraka haraka hizi wizara kwa mfano pale *CAG Office* wana mwanasheria huyu mmoja tu kama ulimi, akiumwa mwanasheria mmoja huyo hawawezi tena kwenda mahkamani kutetewa, na wameshapeleka maombi ya kutaka waajiriwe wanasheria mpaka leo hii hamjawajibu. Hiyo si jeuri hiyo! Na si hao tu Wizara ya Elimu wanataka walimu, mmekaa kimya, Wizara ya Afya inataka madaktari kimya, hii jeuri.

Ahsante Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nitakuja kuunga mkono baadae baada ya kufafanuliwa na mwalimu wangu pale, mwalimu Haroun vizuri. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi hii kupata nafasi ya kutumia muda mchache kutoa pia mawazo yangu machache juu ya kitabu hiki cha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi nha Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii kutuleta hapa katika kazi zetu za kawaida. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, nimpongeze waziri na nimtakie heri Mwenyezi Mungu amrudishie afya yake ili aendelee kulitumikia taifa kama kawaida yake.

Mhe. Naibu Spika, Wizara tunayoijadili leo kulingana na ratiba niliyonayo mimi hii ilikuwa tuijadili kuanzia tarehe 2 na tarehe 3. Leo ilikuwa tujadili Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Kwa hivyo tuko mbele sana ya ratiba. Na kwa nini tukawa mbele kwa sababu zile siku za mwanzo mwanzo pale mlitubana. Watu wamepeleka tunaambiwa aliyekuwa hajaleta tuzungumze kwa maandishi. Sasa mmetufanya tuwe mbele sana, kwa hivyo kwa sababu tupo mbele kama wakiangalia watakua wao wapo hii iendelee kuchangiwa ili ule muda wetu ambao umeshatangulia tuweze kuu-*cover* wenyewe. Isiwe jioni ifungwe na wachangiaji wapo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitawale kidogo hiki kitabu kwenye ukurasa wa 4 pale ambapo Wizara ilipangia kukusanya pesa kidogo zile shilingi milioni mia nane na ishirini na wakakusanya waliokusanya milioni mia moja na hamsini na saba sawa na asilimia 19. Kama nilivyosema katika Wizara moja iliyopita kama huu ingelikuwa ni mtihani hii ni (F) maana yake wamefeli. Kipi kilichowafelisha sikijui.

Katika maombi ya mwaka uliopita serikali iliomba au Wizara hii iliomba bilioni saba na milioni kadhaa. Kati ya hizo ambazo zilifanyiwa kazi na serikali hizi zilizosemwa matumizi mengineyo hizi ndio ambazo zimetumika kwa ajili ya kazi kwa kipindi kilichopita ambao ni shilingi bilioni moja, milioni mia saba na kidogo ambao ni sawa sawa na asilimia 6. Kwa hivyo kazi ya serikali katika Wizara hii kwa miezi 9 iliyopita, imefanyika kwa kiwango hicho. Kama ingelikuwa wanafanya mtihani na hili (F).

Sasa Mhe. Naibu Spika, serikali inatwmbia kuwa uchumi umekuwa, lakini watoto wa serikali ni hizi wizara zake. Tujalie mimi nijigambe nina pesa chungunzima lakini wanangu nyumbani wanalala na njaa ndivyo serikali hii ilivyo, inasema uchumi umekua lakini kazi za serikali kasma inayopelekwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi ni ndogo mno, sasa ukuaji huu tutauonaje wakati ambao huduma ziko duni. Ziko duni si kwa sababu pengine ya ubadhirifu tu wa watedaji wako ata ziko duni kwa sababu hakuingiziwa pesa, sasa kazi hizi ilikuwa azifanye vipi? Kwa hivyo uchumi uliokuwa umekulia wapi?

Kwa kweli kujitangazia kuwa uchumi umekuwa lakini huduma za serikali hazipo sijui huu ukuaji ukoje kwa kweli siujui. Kujitangazia tunavyojitangazia lakini utendaji wetu au uingiaji wa pesa katika kazi ukawa uko katika hali hiyo. Mheshimiwa hali hii si nzuri na haipendezi na inadunisha utendaji wa serikali. Itakuwaje Wizara ambayo

imepangiwa bilioni saba, lakini ile iliyofika kwa huduma za jamii katika Wizara ile ni bilioni moja pekee na kidogo kwa miezi 9 iliyopita. Je, kwa mitatu iliyobakia hiki kilichobaki kitaweza kutumika. Ilivyokuwa haiwezekani kwa miezi 9 pia hakitowezekana kwa miezi 3, ni hatari kubwa kweli kweli. Maneno yetu hayendi pamoja na vitendo vyetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitazame huvi viambatanisho tu ndio mchango wangu kwa leo, sina lolote la kusema. Nitizame ile *column* tu ya matumizi mengineyo ambayo ndio hasa matumizi ya serikali, katika idara zote za Wizara hii. Kuna mipngo Uhusiano na Utafiti ilitarajiwa kupata fedha zile ikapata hizo ni asilimia 31.7 kama ni mtihani (F) wamefeli.

Inayofuata asilimia 38 (F), iliyofuata asilimia 4, kama ingelikuwa kuna nyengine zaidi ya (F) ingekuwa wapewe hiyo. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, katika miezi 9 iliyopita Idara au Taasisi nzima ya Serikali imetiliwa pesa ambayo ni sawa na asilimia 4 tu ya yale makadirio yao. Hapa kweli nitumie lugha ya Profesa Mshimba serikali iko *serious*?

Mhe. Naibu Spika, hii hali ni mbaya na sijui Mhe. Waziri atakuwa na hoja gani ya kutujibu ingawa hana kwa sababu kubwa atasema ndio pesa hakutiliwa na pengine ni kweli. Inayofuata ni asilimia 15 ni (F) hivyo hivyo, 23.7 ndio hivyo hivyo mpaka mwisho, kuna moja tu ina asilimia 64 hiki ni Chuo cha Utawala wa Umma sijui kwa nini kikaongezwa pesa mpaka ikafika hivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika uingizwaji huu wa fedha katika Wizara mbali mbali serikali inakusudia nini? Inakusudia hii serikali ifeli au Wizara zifeli na zikifeli tumlaumu nani? Kauli yetu uchumi umekuwa utendaji wetu uko hivi na ni mambo mawili ambayo hayakubaliani.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo mimi nije kwenye Idara ya Nyaraka na Makumbusho, ambayo karibuni iliundiwa Kamati Teule ya kwenda kuichunguza. Dr. Mshimba hapa alitaka hiyo kamati itoe jibu mimi mjumbe lakini si msemaji wa kamati kwa hivyo itakuwa sina jibu lakini kamati hiyo ilitangazwa na Spika imebakia hivyo hivyo Spika kaitangaza tu basi, haijafanya chochote chengine zaidi ya kutajwa wajumbe wake imemalizia hivyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nmeshangazwa kuwa nyaraka na kumbukumbu maalum katika sehemu hii zinatoweka. *Professor* Mhe. Ali Mzee Ali pale anaishinda hii taasisi kwa kumbukumbu. Kwenye Bunge tulikuwa kamati moja katoa katiba ya uhuru wa 1963 ya Zanzibar pengine ingelikuwa kule ingekuwa haipo tena lakini *Professor* Ali Mzee anayo. Leo taasisi nzima ya serikali inashindwa na raia kwa kutunza kumbukumbu.

Mhe. Naibu Spika, mimi si msemaji mkubwa sana lakini niliwahi kupita skuli siku mbili tatu kusoma na wengine niliposoma mimi walikuwa hawajazaliwa. Mhe. Naibu Spika, mimi mpaka leo mabuku yangu ya *form I* ninayo yana miaka arubaini na iliyopita nyuma lakini watoto wa leo lile la *form II* ya mwaka jana leo yuko *form III* hanalo tena. Hawa watoto wetu wanakwenda sambamba na hizi taasisi za serikali, hawana utunzaji, serikali haina utunzaji.

Mhe. Naibu Spika, hii ni aibu kweli kweli kuwa taasisi ya serikali inapoteza kumbukumbu muhimu na nyaraka muhimu za nchi. Mimi niliyekuwa sina chochote sina madawa, mabuku yangu yapo wala hayajaliwa na mende wala kurasa hazijagandana, nilisahau tu ningechukua moja nikaja kuwaonesha.

Mhe. Naibu Spika, Idara hii kwa hivyo inahitaji wafanyakazi wake wapatiwe mafunzo ya kutosha ili wawe waaminifu na wawe watunzaji wa kumbukumbu na nyaraka muhimu za serikali. Vyenginevyo itafika siku historia na kumbukumbu za kale za nchi yetu ambazo zinatunzwa hapo zitoweke. Nchi ambayo haina kumbukumbu ni hatari tena hatari kubwa kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, niguse kidogo kwenye hii Idara ya Ajira ambayo iliingiziwa pesa sawa na asilimia 4 tu ya mahitajio yake. Ajira kwa vijana ni tatizo, ajira imekuwa ni jambo sugu katika Visiwa vyetu hivi. Serikali ajira kubwa iliyoko hivi sasa pale inapotokea ni katika Vikosi. Mhe. Naibu Spika, kwa jinsi tunavyoajiri vijana katika vikosi vyetu iko siku kila raia kumi watakuwa wana kijana mmoja wa vikosi kuwalinda, kama ingelikuwa ni vikosi ya ulinzi. Kwa sababu hii ndio ajira pekee kubwa iliyobakia, nyengine zote ni za kuokota okota tu. Lakini kwenye vikosi takriban kila mwaka kama si mara moja au mara mbili tunawaajiri. Kwa hivyo, hii ndiyo ajira kubwa iliyobakia nyengine zote zipo na zinasuasua. Sasa sijui serikali haina hizo kazi za kuwapa vijana wetu au hao vijana wa kuwaajiriwa hawapo, sijui inakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, na hao waliokwishaajiriwa maslahi yao ni mepesi mno, katika hali ya nchi yetu tunavyoishi kumlipa mfanyakazi kima cha chini tunachowalipa ni hatari. Mhe. Naibu Spika, mfanyakazi anavyotakiwa kazi anayoifanya imuendeshe, imlishe, imvike, imtibu kama ana watoto awasomeshe, sisi tunamlipa mtu hata kijio cha siku kumi mshahara wake wa mwezi mzima hakifiki. Je, mfanyakazi kama huyu kama anatumikia pahala ambapo chakudokoa kipo hatageuka paka chume akafunua kawa akachukua bila ya kupewa. Mwaka huu ndiyo serikali imetangaza hakuna chochote kabisa isipokuwa wamesema kwamba watawafanyia marekebisho kwa wale ambao hawajafanyiwa, lakini Mhe. Naibu Spika jinsi serikali ilivyofanya marekebisho kwa wafanyakazi ndipo wanapoongeza tatizo jipya, yale marekebisho pia badala ya kuwa ni marekebisho yanazaa tatizo jengine jipya.

Mhe. Naibu Spika, kuna watu zaidi walimu ambao wameshatumikia miaka mingi wamefika sehemu fulani basi marekebisho yalipokuja hawakuongezewa kitu, lakini kuna watu ambao pale walioajiriwa miaka hii miwili mitano nyuma anarekebishiwa kumpita yule aliyezuiwa kuwa asiende mbele tena. Marekebisho haya ni marekebisho gani? Kwa huyu inaonekana ni *mark time* kaa hapo hapo anakuja mjukuu wa kielimu mwenye elimu kama yake huyu uliyemzuia anabakia pale huyu anakwenda mbele kuliko huyu aliyezuiwa, wana elimu moja lakini wanatofautiana sana kwa miaka ya kazi na uzoefu wa kazi.

Kwa hivyo, jinsi serikali ilivyojaribu kufanya marekebisho ndiyo pia inapozaa tatizo jengine jipya, pale ambapo serikali huko miaka ya nyuma haijakuwa na wataalamu kama leo ilikuwa mambo yanakwenda vizuri kweli kweli. Kila *increment* ya mwaka anaongezewa, aliyetangulia hafikwi na aliyeko nyuma.

Mhe. Naibu Spika, leo tuna wataalamu kwa lugha nyengine kibao lakini mambo yanakwenda kibao, je, baadhi ya wataalamu wanai-*sabotage* serikali? Kwa sababu haiwezekani Mhe. Naibu Spika, mtu aliyefika miaka 30 keshokutwa anastaafu halafu ashindwe na mtoto wake aliyemzaa mwenyewe, ana elimu kama yake kwa malipo, sijui ilikuwaje marekebisho haya yanavyokwenda. Hapo anapomaliza sasa anapotayarishiwa hicho kiinua mgongo chake kupitia huu mfuko wa hifadhi inasemekana anachukuliwa mshahara wake aliyomalizia wanarudi miaka minne nyuma wana-*top up* halafu wanatafuta *average*, wanapotafuta *average* ya miaka mitano ule mshahara ambao aliondokea haufiki tena. Kwa hivyo, anatayarishiwa mafao yake kwa *average* ya miaka kadhaa wala hachukuliwi pale ambapo kwa miaka aliyostaafu. Hapa baada ya kuwa mtu anastaafu yakumnnyanyua akaishi vizuri tunampiga nyundo ya kichwa.

Mhe. Naibu Spika, sijui mambo haya yakoje, serikali inayofuata sheria, katiba na utawala bora ikiwa mambo yake yanakwenda kwa aina hiyo yenye wataalamu chungu mzima. Mhe. Naibu Spika, lengo letu ni kuwatetea na kuwatumikia watu hasa utumishi wetu uwe na lengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi Tume yake ya Utumishi na watumishi wake bado hawajatendewa haki, kwa hiyo ningeliiomba serikali kwa sababu hiki ni chombo kimoja katika nguzo tatu kuu za serikali cha kutunga sheria, serikali yenyewe na mahakama. Sasa kwa nini Tume ya Utumishi ya hapa Barazani ambayo ni moja katika mihimili mitatu ya serikali ikawa inapigwa danadana.

Mhe. Naibu Spika, watu wa nchi hii au serikali ya nchi hii hakuna wafanyakazi wazuri duniani kama wafanyakazi wa Zanzibar, kwa sababu mambo wanayofanyiwa na serikali yao ingekuwa nchi nyengine ama wangaligoma ama wangaliandamana. Lakini kwa ajili ya upenzi wa nchi yao na pengine pia kwa hofu isijekuwa maana nikigoma nitafukuzwa kazi, lakini tunawaonea huruma kwani watu wanafanya kazi katika mazingira magumu, maelezo yetu ya vitabu vyetu na midomo yetu tu pia iende katika utendaji halisi wa shughuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, tuwape imani watumishi wetu ili wafanye kazi ya kuwatumikia watu kwa moyo mkunjufu, haipendezi, haifurahishi wala haielekei kumuona mfanyakazi miaka michache au mwaka mmoja tu baada ya kustaafu ana haha lakini anahangaika, anataabika, anasumbuka na ni jana tu kaacha kwenye utumishi wa taifa lake.

Mhe. Naibu Spika, bila ya watumishi serikali ingelikuwa haipo, mwalimu wangu mmoja aliniambia kuwa uendeshaji wa shughuli yoyote ni *chain process*. Kila kiungo ni muhimu sawa na kingine. Mhe. Naibu Spika, kama ingelikuwa hakuna mchangiaji wa pale Manispaa Mjini basi Mji ungelinuka kuliko vile unavyonuka leo. Lakini kwa sababu kuna mtu anayesafisha pale basi ile harufu mbaya inaondoka. Kwa hivyo, mtu huyu na yeye ni kiungo sawa na mimi niliyekuweko huku, sisemi kuwa tulingane kwa maslahi, lakini na hayo maslahi yake afanyiwe ili aweze kuishi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa bado dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: ...na yeye apangiwe maslahi yake aweze kuishi, siyo anaondoka kazini akifika nyumbani hata chumvi hakuna.

Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kuwa inatwambia kuwa uchumi umekuwa hivyo huu ukuaji wa uchumi uonekane ndani ya utendaji wa serikali katika taasisi zetu, usiwe katika vitabu tu.

Mhe. Naibu Spika, jinsi tunavyojitangaza mtu aliyeko nje ya Zanzibar au nje ya Tanzania atazisikia hotuba zetu nzuri tunazozitoa ataona kwa Zanzibar wako kwenye pepo ya dunia na aje aone ni hatari sana.

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba sana serikali hii hali ya uingizaji wa fedha katika taasisi zake uuone na ione kuwa *OC* ndiyo fedha ambayo inayoendesha wizara kwa hiyo ziingizwe kulingana na walivyopangiwa tena kwa wakati kwa vile uchumi wetu umekuwa wa kima kikubwa. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, asubuhi hii ya leo na mimi kunipa fursa yakuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na machache tu sina mengi kwa leo hii nitachangia kidogo tu, lakini kwanza naomba nichangie hapa kwenye hii utumishi wa umma kuhusu suala la ajira.

Mhe. Naibu Spika, suala la ajira ni muhimu sana kwa nchi yetu na kwa vijana wetu, Mheshimiwa kama wenzangu walivyozungumza kwanza kama tuna vijana wetu wengi wanaosoma wengine wana Diploma, wengine wana degree lakini wengi hawana hizi ajira. Sasa hizi ajira zilizopo katika nchi yetu basi Mhe. Waziri angezisimamia vizuri tukaona kama hawa vijana wetu ambao wamesema hizi ajira zilizopo chache basi zinakuwa zina-*balance* vijana wetu wa Zanzibar wanakuwa wanapewa kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Saleh ametoa mfano hapa kama Oman kule wazawa ndiyo wanapewa kipaumbele hata mishahara ya wale wazawa katika nchi ya Oman basi na wale waliokuja ambao hawakuzaliwa pale hawalingani mishahara yao. Wale wazawa wanakuwa na mishahara mikubwa zaidi.

Sasa Mheshimiwa ajira zetu zilizopo katika haya mahoteli yetu ni ajira, lakini wengi wamepiga kelele kama wale wazalendo wanakuwa chini zaidi kuliko wale wageni wanaokuja katika nchi hii. Kwa mfano, wa Kenya na siyo wa Kenya tu wanakuja wengine wanatoka nchi nyengine, lakini wapo hapa wamepata ajira siyo mbaya. Sawa, wamepata ajira kutokana na utaalamu wao na hata nchi nyengine za wenzetu wataalamu wakija wahawawezi wakawafukuza kwa sababu mtu kama huyo ana utaalamu wake anapata kazi kutokana na utaalamu wake.

Hata sisi wazanzibari tunao ndugu zetu ambao kuwa wanafanya kazi nchi za watu lakini kutokana na utaalamu wao walionao. Kwa hiyo, siyo vibaya lakini wale wazawa walitakiwa wapewe kipaumbele.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala hili la ajira namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie sana na alisimamie aone kama sekta hizo za utalii basi wanawapa kipaumbele wazawa.

Suala jengine kuhusu huku mahotelini ni suala ambalo kila siku tunalipigia kelele kuhusu waajiri kwamba hawawatendei haki waajiriwa wao ambao wengine hawapewi mikataba na inakuwa ni rahisi kuwafukuza na wakiwafukuza wanakosa haki zao. Mhe. Naibu Spika, hili suala tumeshalipigia kelele sana hivyo namuomba sana Mhe. Waziri apitie katika mahoteli na akija atueleze kama ni wafanyakazi wangapi ambao wamepewa mikataba waliowasimamia, na ni wangapi bado hawajapewa mikataba. Pia ni mahoteli gani ambayo yanakuwa sugu kuwapa mikataba wafanyakazi wao.

Suala jengine Mheshimiwa ajira sasa hivi zote zinapitia utumishi wa umma, wizara zote zinaleta barua zao utumishi wa umma, na utumishi wa umma inatakiwa ndiyo sasa itoe barua za kuwapa *go head* zile wizara zenyewe. Amezungumza Mheshimiwa kuhusu Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kama wana mwanasheria mmoja na wameshaleta ombi, kwa hiyo namuomba Mheshimiwa hili alisimamie aone kama ile idara hii ni muhimu sana.

Kwa hiyo, kuwa na mwanasheria mmoja si kuwatendea haki kwa sababu mwanasheria mmoja anataka mwenzake washauriane.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, kuhusu hizi ajira mimi ningeomba sana kama watu wanachukuliwa kutokana na vigezo vya elimu yao, lakini Mheshimiwa nafasi hizi zinatangazwa kwenye magezeti, zinatangazwa kwenye maredio, zinatangazwa kwenye televisheni. Lakini Mheshimiwa siyo watu wote kama wanapata habari kwenye televisheni na kwenye redio, ningeomba Mheshimiwa hata kama inayoajiri ni utumishi wa umma lakini hizi ajira zingegaiwa kutokana na Wilaya, Mikoa, Majimbo kwa sababu kama zitakwenda Majimboni au Wilayani basi wataenea watu ajira. Lakini kutokana na kutangaza wanaopata zaidi ni watu waliopo Mjini hata kama wameshaangaliwa elimu na vigezo, hiyo elimu na kule vijijini iko.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nilitaka kuzungumza ni suala la wafanyakazi wanapostaafu. Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi hawa wanapostaafu sheria yetu ile kila siku tunazungumza kama sheria ile inawabana wafanyakazi. Kwa sababu mtu anaweza akastaafu sasa anatakiwa afike umri wa miaka 60 ndiyo alipwe kiinua mgongo chake kile.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwingine mtu anaweza akastaafu ana miaka 55 bado miaka mitano mbele, hivyo anapostaafu kama ana miaka mitano mbele mtu huyu anakuwa anahangaika sana hajapata pesa zake. Kutokana na kuwa ameshafanya kazi muda mrefu badala ya kufaidi zile pesa zake ambazo amezifanyia kazi pengine anataka ajenge, anataka afanye kitu kingine cha kumsaidia katika maisha yake inakuwa pesa zile hazipati mpaka ule umri wa ile miaka 60 inayotakiwa ndiyo apate zile pesa zake.

Kwa hiyo, naomba hii sheria ifanyiwe marekebisho, kwa sababu wengine wanakufa bila ya kufaidi matunda ya jasho lao walilolitoa. Sasa hii inawabana sana wafanyakazi wanapostaafu na wengine wanakuwa hawafaidi zile pesa zao, pesa zile zinakuja kurithiwa yeye mwenyewe hayupo kabisa. Kwa hivyo, naomba na sheria hii ifanyiwe marekebisho ili mtu anapostaafu tu asisubiriwe mpaka afike miaka 60 kuwa akamilishe ile miaka 60 ndio apewe pesa zake, apewe mapema ili zimsaidie kuweza kujiendesha na maisha kwa sababu anakuwa hayumo tena kazini.

Mhe Naibu Spika, suala jengine ninalotaka nilizungumze, kama nilivyokwambia leo nina machache tu ni hili suala linalozungumzwa la Utumishi; Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi. Suala hili tushapiga kelele sana na kipindi kilichopita Mhe. Salmin Awadh Salmin alipiga kelele kweli kweli kwa suala hili, kwa nini unakuwa uzito watumishi wa Baraza la Wawakilishi wanaingizwa katika Tume ya Utumishi wa Umma iliyoko kwenye serikali, wakati Baraza la Wawakilishi lina Tume yake ya Utumishi. Naomba sana, hii Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi ipewe haki yake na iweze kufanya kazi zake bila ya kubanwabanwa.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi, lakini pia nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kuwa katika hali ya afya njema.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpa pole sana Waziri ambaye alipata matatizo lakini huo ni utumwa wa Mwenyezi Mungu, na nimuombee dua Mwenyezi Mungu amjaalie na amzidishie afya ili tuwe naye katika kujenga Taifa letu. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao walimsaidia kuandaa kitabu hiki chenye malengo mbali mbali ili kumuwezesha aweze kutuelezea mambo mbali mbali katika michangio yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na mambo lakini mafupi mafupi, kwanza nitakuwa na wastaafu. Wastaafu nakusudia ni wastaafu wote kwa jumla, lakini hasa ni wastaafu wa vikosi. Naomba sana wastaafu hawa waangaliwe lakini si kuangaliwa tu, hata pencheni zao kwa kweli ni ndogo.

Lakini nikija katika wastaafu hawa wa vikosi nije hasa na wafanyakazi wote ambao wamestaafu. Naiomba sana serikali katika mambo yote lakini watu hawa waliijenga na wao nchi hii kwa namna moja au nyengine. Sasa naomba pencheni iongezwe, mtu pencheni anayopata haifanani kabisa na kazi aliyoifanya kama miaka 50, 45 mpaka 30. Hivyo serikali tujaribu kama tunavyoweza ili kuwasaidia wastaafu wetu hawa ambao na wao wameitumikia nchi hii na ndio tukaweza kufika hapa ni pamoja na wao. Hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nitamuomba Mhe. Waziri kwa sababu hii wizara amepewa hivi karibuni, namuomba sana aipitie upya wizara hii, aangalie ni wapi na wapi kuweza kuweka marekebisho, kwa sababu wizara hii ndio moyo wa serikali. Kwa hivyo, nitamuomba sana Mhe. Waziri na watendaji wake apitie kila kipengele akishirikiana na Waziri ambaye alikuwa na wizara hii ili aweze kuhakikisha kwamba mambo yanakaa sawa. Kwa imani yangu kwa Waziri huyu kama alivyoitengeneza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wizara hii itafanikiwa *Inshaallah*. Hilo la pili.

Lakini la tatu nije katika wastaafu wa Usalama wa Taifa. Huko nyuma Usalama wa Taifa walikuwa wanalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini baadae wakaingia katika Muungano. Naiomba serikali pale ambapo waliitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar basi zile haki zao wapewe, kwa sababu kuna haki ambazo wanazidai hawa. Serikali na hili ilitupie macho Mhe. Waziri, mukae mtafakari, mzungumze, mkubaliane na wizara husika, kwa sababu hili ni la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Wizara ya Fedha muwafikirie hawa Usalama wa Taifa ili yale mapungufu yao waliyokuwa hawajalipwa basi walipwe wala si pesa nyingi kwa kipindi ambacho wamestaafu hawa watu.

Jengine niipongeze sana serikali kwa ajira ambayo imeajiri, lakini nitoe wito kwa wasomi wote ambao hawajapata ajira, jamani kuajiriwa sio lazima uajiri wa serikali, ajira ni kisomo chako ambacho umesomea kitu fulani na kuweza kutafuta kundi la wenzako mkaweza kujiajiri wenyewe. Natoa wito kwa wasomi wote serikali hii imeweka fedha za uwezeshaji, natoa wito wale ambao hawajapata ajira basi wajikusanye kwa mujbu wa *qualifications* zao ambazo wamesomea ili waweze kujiajiri. Nina imani kubwa kwamba serikali hii itaweze kuwasaidia, tusikae tukanung'unika kwamba hatuna ajira, ajira ni yako mweyewe ulichokisomea, kama serikali haijakuajiri. Naiomba sana na nawaomba wasomi wakae, waunde taasisi yao ili kuhakikisha na wao wana taasisi yao ya wasomi waweze kujiajiri wenyewe, halafu baadae waiombe serikali kama wanataka kujiajiri ni kitu gani ambacho kitaweza kuwasaidia.

Nikiendelea nije kwenye ajira kwa watoto. Pia na hili nitoe wito kwa wazazi, sisi ndio wazazi, sisi ndio tunaolea, sisi ndio tunaosomesha. Nitoe wito kwa wazee kwamba ukitaka kumpa utajiri mwanao umpe elimu, utajiri wa mtoto kwa ulimwengu tulionao sasa hivi ni elimu, tuache kuwatumia watoto wetu wadogo kuwapotezea maisha yao, wewe umeshayapoteza yako sasa mtizame yule ambaye atakuhangaikia wewe. Mimi nasema kwa wazazi wa kike na wa kiume tuache kuwatuma watoto wetu wadogo kuwapa ajira za kufanya mambo ambayo si mazuri. Hilo la tano. *(Makofi)*

Lakini jengine nije katika Vikosi vya SMZ, ingawa vina wizara yake lakini ningeomba Mhe. Waziri vikosi hivi vifikiriwe kwa sababu wanafanya kazi kubwa. Vifikiriwe kila kipindi baada ya mwaka, najua serikali uwezo wake ni mdogo lakini hivi ni vikosi mvifikirie kupandisha mishahara, mishahara yao ni midogo kwa uwezo wanaofanya kazi.

Naiomba sana serikali pamoja na kwamba najua wanawazidishia mishahara yao, lakini naiomba serikali pamoja na yote hivi ndio vikosi ambavyo vinasaidia katika nyanja zetu mbali mbali. Pia niseme kwamba wizara yao itakuja lakini si vibaya na haya na wao wakapatiwa ajira binafsi, lakini nitakuja kuzungumza wakati wa vikosi.

Jengine ambalo nitalizungumza nimesikiliza wenzangu hapa Mhe. wa Vitongoji na Mhe. Mohammed Haji Khalid, wamezungumzia kuhusu habari ya Oman. Mimi nataka niwaambie hivi, waliyoijenga Oman ni Wazanzibari, tena wamewapata Wazanzibari *readymade* waliosomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa sababu mimi *bench* langu niliosoma nao mwaka 1964 *Fidel Castro* wote pamoja na wale ambao akina Mhe. Mohammed Haji Khalid tumebakia mimi, yeye na Mhe. Abubakari Khamis Bakary, kwa sababu sisi wazazi wetu wote ni Wazanzibari, lakini wengine wote wamekwenda Oman na ndio waliojenga huko, niwapongeze sana hili wala halina ubishi. Kwa hivyo, niseme tu kwamba, Oman huko nyuma kuanzia kwenye 1960 imejengwa na Wazanzibari na hawa wamepatikana *readymade*, walivyokwishakumaliza tu hapa *Form IV;* ya zamani sio ya leo, wamekwenda kule na wengine wamesomesha wenzao walioko kule. Kwa hivyo, mimi niwapongeze kwa hilo, niwapongeze Wazanzibari waliotoka hapa wakaenda wakasaidia watu wa Oman.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu umesema kuwa tutumie wakati niseme tu niunge mkono suala moja la watu wanapostaafu kupata mafao yao ya *ZSSF*. Kwa kweli hili ni jambo muhimu sana kwa serikali, mtu anastaafu unafika wakati wake lakini hapati ile haki yake ya kuweza kumsaidia yeye kuendesha maisha yake. Naiomba sana serikali

kama kuna sheria, kama kuna kanuni; kwa kweli suala hili tuliangalie vizuri ili mtu anapostaafu apate ile haki yake sio ameshakufa pesa zinatumiwa na watu wengine, wanafaidika wengine. Yeye ndiye aliyefanya kazi zote. Naiomba serikali hilo Mhe. Naibu Spika.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, natoa ushauri na naiomba sana serikali kwamba, tunapofanya mambo ya bajeti hebu tuige mfumo wa wenzetu Tanzania Bara. Sisi hapa tunakuwa tunajadili kwenye Kamati zetu lakini tunachokijadili ni kwamba ndio hicho hicho hakiwezi kikaongezwa. Sasa ninachoomba ni kwamba tufanye kama wenzetu Tanzania Bara ili angalau tuweke Wizara ya Fedha iwe mwisho kabisa. Tunapozungumza kama kuna jambo limejitokeza wizara imepewa pesa kidogo, basi wizara ile iweze kuongezewa fedha. Hili nalizungumza kwa makusudi kwa sababu sasa hivi tutasema tu wizara hii imenyimwa pesa kifungu hiki, kwa nini wakapewa pesa hizi, ni kwa sababu ndio mfumo tulionao hivi sasa, na hata tukifanya nini serikali haiwezi ikaongeza fedha za aina yoyote.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi leo hii, lakini kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia asubuhi hii uzima na afya njema. Pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpa pole Mhe. Waziri kwa matatizo, kwa maradhi ambayo anayo, lakini nimuombee dua kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwa na afya njema na maisha marefu ili aweze kuendelea na majukumu aliyonayo ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa niingie katika kitabu hiki, lakini pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kuwapongeza watendaji wote wa wizara hii kwa kumpa mashirikiano ya dhati Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma katika kuandaa kitabu hiki hadi kufikia leo hii kukijadili ndani ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie katika ukurasa wa 4 wa kitabu hiki; Muhtasari wa Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Serikali inategemea kupata pesa kutokana na vianzio vyake mbali mbali vya nje kwa maana ya wafadhili, lakini pia vianzio vyake vya ndani kwa maana wananchi ambao ni wavuja jasho wa Taifa hili.

Lakini pia matumizi ya serikali yanapangwa kwa kuzingatia makusanyo hayo na zaidi makusanyo hayo ni kiasi cha fedha ambazo taasisi imepanga kukusanya inakuwa imeshajipangia matumizi katika Bajeti ya Serikali. Sasa taasisi inapopanga kukusanya mapato lakini halafu inapokuwa mapato yale wakayakusanya kwa asilimia si zaidi na yale waliyojipangia kwa kweli Mheshimiwa jambo hili huwa la kusikitisha.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki wametwambia kwamba wamejipangia kukusanya mapato ya Shilingi 820 hadi kufikia Machi, 2014. Lakini kwa bahati mbaya imekusanya mapato ya shilingi 157 sawa na asilimia 19 ya makadirio. Sasa asilimia hii ni zaidi ya shilingi 600 milioni ambazo ni pesa nyingi sana katika utaratibu mzima wa serikali. Mimi najiuliza, kwa sababu naamini kwamba bajeti hii ambayo waliipanga ya ukusanyaji bila shaka ni ya vianzio vyao mbali mbali vya ukusanyaji wa mapato, lakini hatimaye mapato hayo yameshuka kwa asilimia 10. Sasa nafikiri Mhe. Waziri atapokuja hapa atuelimishe kwa faida ya Baraza hili Tukufu, lakini na wananchi ambao nje wanatusikiliza, imekuwaje kwamba mapato haya yameshuka na kufikia shilingi milioni 157.

Mhe. Naibu Spika, pia ukija katika ukurasa huu wa mwisho katika mwaka wa fedha 2014/2015 wamepanga kukusanya mapato ya shilingi milioni 251. Pamoja na ukusanyaji ambao ulipita walitwambia kwamba watakusanya shilingi milioni 820, lakini kwa bahati mbaya wamekusanya shilingi milioni 157. Sasa sio kigezo cha kwamba kipindi kijacho wakusanye milioni 250. Kwa sababu mimi naamini kwamba vianzio vyao vya mapato bado vipo vile vile, sasa si rahisi kuamini kwamba inawezekana wakakusanya mapato ya shilingi 251 milioni. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anielimishe vizuri nielewe ili niweze kumpitishia bajeti yake hii.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 14 wa kitabu hichi. Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara hii kwa namna walivyosomesha wafanyakazi wao wengi. Lakini Mhe. Naibu Spika, taasisi hii sio kuwa ndio kwanza kujitahidi kusomesha wafanyakazi wake. Tumeona katika Wizara iliyopita Ofisi ya Makamu wa Kwanza hata wao wamejitahidi kusomesha wafanyakazi wao wengi kupitia Wizara yao.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, hata Wizara ya Fedha kwa kawaida huwa inasomesha wafanyakazi wao wa ndani katika Wizara yao hiyo ya Fedha lakini hata taasisi nyengine. Sasa Mhe. Naibu Spika, nimeona kwamba hawa

wameunda Idara maalum ya kusomesha wafanyakazi. Sasa kwa mtizamo wangu sioni mantiki ya kuwepo Idara hii maalum kwa kusomesha wafanyakazi. Kwa sababu bila shaka taasisi zote za Serikali zina utaratibu maalum wa kusomesha wafanyakazi wao. Sasa hapa kuundwa Idara hii mimi naamini tunaharibu pesa za Serikali tu, basi bora pesa hizi tuzitumie kwa mambo mengine ambayo ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije katika Idara ya Nyaraka. Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Idara hii kwa kuona kwamba upo umuhimu mkubwa wa kutafuta namna, lakini pia kwa kuona kwamba umuhimu wa kuhifadhi nyaraka zetu kwa njia ya kielektroniki. Lakini hata hivyo Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba huu ndio mfumo wa sasa hivi ambao tunakwenda na wakati. Lakini mimi niombe Wizara kwamba pia tusidharau basi kutumia mfumo huu wa *manual* tuliotoka nao hapo zamani wa kuzihifadhi nyaraka zetu.

Mhe. Naibu Spika, tunaamini kwamba mfumo huu wa kielektroniki unaweza wakati wowote ukaharibika, lakini inawezekana pia kumbukumbu zikapotea. Sasa kama tutautegemea mfumo huu tu mmoja tunaweza tukapoteza kumbukumbu zote za Idara hii. Sote tunafahamu kwamba Idara hii ni nyeti, Idara hii ni muhimu sana kwa taifa letu, kwa sababu kumbukumbu zote za taifa zinahifadhiwa hapa.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, wageni wote wanakwenda hapa katika kuangalia kumbukumbu, wageni ambao wa ndani ya nchi, na pia wageni wa nje ya nchi kwa ajili ya kufanya tafiti mbali mbali. Sasa Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha sana unaweza ukaenda katika Idara ile unakuta viti vimefungwa kamba. Namuomba Mhe. Waziri aje atwambie ana mikakati gani ya kufanya ukarabati?

Lakini si hilo tu Mhe. Naibu Spika, jengo lile pia limechakaa na bovu sana. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri hili pia ni muhimu sana kuzingatia. Kwa sababu katika kitabu chake hichi ametwambia kwamba malengo yake amejiwekea kufanya ukarabati, kufanya matengenezo. Lakini taarifa hizi Mhe. Naibu Spika, hata katika bajeti iliyopita alitwambia maneno haya kwa haya.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nije katika vifaa vya *CCTV camera.* Kama tutakumbuka Waheshimiwa Wajumbe katika bajeti iliyopita Mhe. Waziri pia alitwambia kwamba ana utaratibu wa kuunga kifaa hichi. Lakini mpaka bajeti hii ndio kwanza Mhe. Waziri anatwambia kwamba anategemea kufunga kifaa hichi. Sasa sijui Mhe. Naibu Spika, *are we serious?*

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, katika Idara hii tuliambiwa kipindi kilichopita ziliibiwa baadhi ya nyaraka, na tukasema kwamba ni vizuri basi waunde Tume au watu maalum katika Idara hii hii wawe wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuepusha lile jambo lililotokea lisitokee tena. Waswahili wanasema "Ukiumwa na nyoka ukiona unyasi unashtuka". Kwa hiyo na Idara hii kwa kweli imeshaumwa na nyoka, sasa nawaomba basi wasituandikie tu kwamba tuna utaratibu wa kufanya ukaguzi. Mimi nadhani ni vizuri wangetueleza kwamba wamepanga kuwa kila baada ya mwezi au miezi mitatu watafanya ukaguzi wa ndani wa nyaraka hizi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na Idara hii sote tunafahamu kwamba nyaraka hizi zinabeba takataka mbali mbali kutokana na uchakavu wa makaratasi zaidi zinabeba vumbi. Sasa Mhe. Naibu Spika, sijui sina uhakika sana kama wafanyakazi wetu ambao wanahusiana na hizi nyaraka wanazo hizi *mask* maalum wanavaa wakati wa kupanga karatasi zile.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wale ambao wanatunza nyaraka zile kwa kweli wanaishi katika mazingira ya hatari kwa afya zao. Lakini pia lazima tufahamu kwamba wafanyakazi wale sisi ndio tuliobeba mzigo ule. Kwa hiyo naomba Mhe. Waziri kama hizo *mask* hazipo, basi aje kutueleza kwamba katika bajeti hii amejiandaa vipi kuhakikisha kwamba wafanyakazi wale ambao wanatunza nyaraka zile wanapatiwa *mask* maalum. Isiwe inatokea mtu unakwenda kucheki unaambiwa stoo *mask* zimemalizika.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Waziri kwa namna alivyowatafutia vijana wetu ajira nje ya nchi. Mimi naamini kwamba amefanya kazi nzuri sana, kwa sababu sote humu ndani ya Baraza hili tukufu tunakaa tunawaelimisha wananchi kwamba vijana wasitegemee ajira ya Serikali tu, kwa sababu Serikali haiwezi kuwapa ajira watu wote.

Lakini Mhe. Naibu Spika, sijaona humu katika kitabu chake kwamba amejitahidi kwa kiasi gani kuwatafutia vijana ajira katika kampuni zilizowekeza ndani ya nchi. Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sadaka inaanza nyumbani, na

naamini kwamba kama Mhe. Waziri ameweza kutoka nje akajipanga vijana wetu kupata ajira nje ya nchi, sidhani kwamba anaweza kushindwa kujipanga vijana wetu wakapata ajira ndani ya nchi. Matokeo yake tuna vijana wengi tu wamo katika makampuni binafsi ambao sio wazalendo, vijana ambao wa nje ya nchi. Kwa mfano Wakenya.

Sasa hii Mhe. Naibu Spika, kwa kweli haileti heshima kwa taifa letu, lakini pia haileti hadhi kwa taifa letu. Kwa sababu mimi naamini kwamba kama tutajiwekea mikakati maalum kwamba kampuni yoyote ambayo itawekeza Zanzibar lazima ifuate masharti maalum ya kuhakikisha kwamba kwanza inampatia ajira mwananchi wa Zanzibar. Naamini kwamba litawezekana, lakini pengine labda Serikali haijawa makini katika kutekeleza hili. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja ku-*wind up* atwambie amejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba vijana wetu anawapatia ajira katika kampuni ambazo zimewekeza ndani ya nchi yetu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema sote tunafahamu kwamba taasisi zetu zina matatizo ya kuajiri wafanyakazi. Na pengine Mhe. Naibu Spika, ajira nyingi zinaajiriwa katika taasisi kutokana na kada mbali mbali, lakini ukiangalia kiundani unakuta taasisi zetu za Serikali zinaajiri kada nyingi zikiwemo za Uhasibu na Wanasheria. Kwa hiyo waajiri hao, wanapokwenda katika taasisi unakuta vijana wamekuwa wengi, hata wanakuwa hawana kazi ya kufanya katika taasisi ile. Sasa mimi naomba hili nitalichangia katika Wizara ya Elimu, lakini naomba niligusie tu kwamba Mhe. Waziri basi mshirikiane na Mhe. Waziri husika ambaye ni Waziri wa Elimu kuona kwamba vyuo vyetu sasa vibadilike. Kubadilika kwamba vipunguze kusomesha kada ya uanasheria na uhasibu, badala yake tujikite katika baadhi ya kada nyenginezo ambazo hatuna watu wa kutosha kutokana na kuwa hawana taaluma ya kada zile.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano kuna kada ya utaalamu wa mazingira tuna upungufu, lakini pia kuna kada za mainjinia sidhani kama kuna vyuo ambavyo vinasomesha kada hizo. Lakini pia kuna baadhi ya kada pia sijazitaja hapa tuna upungufu wa wafanyakazi hao. Hatimaye unakuta taasisi nyingi zina wanasheria zaidi ya 20, kuna wahasibu zaidi ya 10, sasa baada ya kufanya kazi za uanasheria wanakuja kupewa kazi ambazo hazina sifa na taaluma yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango huo naunga mkono asilimia mia moja, lakini naomba Mhe. Waziri aje kunijibu masuala yangu niliyochangia ili na mimi nijiridhishe. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami nikushukuru kuniruhusu kuchangia muda huu ingawa sitokuwa na mengi lakini nitachukua kama dakika zangu 5 mpaka 7 kuzungumza kidogo lakini nieleweke.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Waziri Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na watendaji wake wote katika kusimamia majukumu haya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo bila ya kupoteza muda nianze na ukurasa wa 47. Kwa masikitiko makubwa mimi nilikuwa nikipiga kelele sana suala la Tume ya Utumishi Serikalini, naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika. "Kwa mwaka wa fedha 2012/13 Tume ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

Kuandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki ambapo ajira 1,419 zilitegemewa kutangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini."

Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha ambacho mimi nafsi yangu siwezi kukiamini watu walioajiriwa ni 568, vijana wangapi leo huko nje wana digrii bado wanaendelea kuteseka. Nafasi za ajira 568 zilipokelewa na zilitangazwa kupitia *ZBC TV* na Redio. Usaili wa nafasi 568 za ajira ulifanyika Unguja na Pemba kwa kibali cha ajira na kwa nafasi hizo kuteuliwa. Angalia Kiambatanisho namba 8A.

Tunafanya nini? Kiwango ni kidogo ambacho hakikufikia malengo. Hapa nitahitaji maelezo. Vijana wetu wengi wamesoma wamekuwa na madigrii, madiploma bado wanateseka na ajira. Na cha kusikitisha zaidi kuna wengine wazee wanaongezwa muda. Siku hizi wanachukuliwa kuongezewa muda huku wale wenye nguvu hawapati ajira.

Tuangalie hivi juzi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafikiri kateua Wakuu wa Wilaya vijana; kwa kuzingatia vijana ndio nguvu kazi ya kesho. Hii mihali itatupeleka wapi. Imekuwa Zanzibar shamba la bibi tunasomesha watu, tunawalea, wanapata madigrii baadae wanatutoroka hapa hawawezi kukaa katika mazingira kama haya.

Leo daktari akivuka tu kufika Dar es Salaam hapo sikiliza pesa anazozipata. Kitu cha kusikitisha tena hapa nitahitaji maelezo Wizara hii haraka iajiri daktari wa mifupa, hapa Unguja ninayemjua ni mmoja tu. Na hapa nitakuwa mkaidi kweli kweli. Haiwezekani Dokta Shaib peke yake pale Mnazi Mmoja. Na ukienda Mhe. Ali Salum Haji hayupo hapa alipata ajali Jimboni kwake tulikaa masaa matano kumbembeleza kutoka Fuoni kuja pale kufanya kazi. Hapa nitahitaji maelezo Wizara hii *immediately* iajiri. Hatuwezi kwenda hivi kubahatisha, kuyaweka maisha ya wananchi wetu rehani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije ukurasa wa 81 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu. Kuhusu watalii waliofika nchini tumeambiwa watu 478. Ni kweli idadi ndogo kama Zanzibar itakusanya mambo yake ya kale katika historia kuitangaza.

Kuna mambo mengi ya kujivunia hapa mfano hai Livingstone kapita tu Zambia sijui na wapi wameshamtungia *history.* Hapa tulikuwa tunae hatujautangaza utalii wake. Leo ukiuliza kaburi la Siti binti Saadi utaambiwa sijui liko wapi hapa. Kuna msanii wetu Bi Kidude amefariki kaburi hata kujengewa halijajengewa, watoto wetu watakuja kuuliza Bi Kidude ni nani katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kilio chengine ambacho Mhe. Saleh Nassor Juma alikizungumza. Tumeambiwa mapato ya Zanzibar yamekuwa, sijui yamekuwa kwa kiasi gani wakati Mahkama zetu watu wanateseka, mazingira magumu ya vitendea kazi, ma-*DPP* halikadhalika haisemeki.

Cha kusikitisha sasa hivi walimu wetu. Kuna baadhi ya Wajumbe wametuletea *messages* walimu wenye digrii mishahara kurekebishwa imekuwa ina vikwazo vikubwa. Kwa hiyo wanapendekeza bora waje huko Utumishi kuchukua mafao yao. Ualimu kazi kubwa kumfundisha mwanafunzi mpaka akafika pahala kufahamu. Na Waziri nashukuru mimi umetokea ualimu. Hayo marekebisho yafanywe haraka walimu wana mazingira magumu wanayoishi, wengine hata vipando hawana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri dakika zangu 5 zimekwisha, na vile vile nimeshafahamika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu juu ya hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, jambo la mwanzo ambalo nahitaji nilizungumze ni lile juu ya suala la mfuko wa bima wa afya. Mhe. Naibu Spika, suala hili la mfuko wa bima ya afya ni suala ambalo tumelizungumza kwa muda mrefu na inaonesha kwamba hatua bado hazijachukuliwa.

Mhe.Naibu Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri ni lini mfuko huu wa bima ya Afya utaanza kufanya kazi ili wafanyakazi wa Zanzibar waweze kufaidika na mfuko huu, kwa sababu mfuko huu ukitizama kwa Tanzania Bara tayari mfuko huu umeshaanza kufanya kazi na wafanyakazi wameshaanza kufaidika. Kwa hivyo nilitaka nijue tu Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze ni lini hasa mfuko huu utaanza kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, suala langu la pili ninalotaka nilizungumze ni maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, kutokana na kupanda kwa maisha, yaani vifaa pamoja na chakula pamoja na makaazi, kwamba makaazi yamekuwa kodi zake ni kubwa sana, na ambayo yote haya yanamsubiri mfanyakazi. Msururu wa ada za malipo. Malipo yenyewe kwa mfano mzazi ambaye ana watoto. Haya yote yanamkabili mfanyakazi alipe ada ya malipo ya skuli, ni moja katika orodha zake na yamepanda malipo ya skuli bila ya kiasi.

Haya yanawakabili wafanyakazi Mhe. Naibu Spika, pia na wananchi mambo haya yanawakabili. Hali hii kimaisha inakuwa ni ngumu sana. Yanafanya maisha ya wafanyakazi wetu kuwa duni na maslahi duni kwa wafanyakazi wetu.

Mhe. Naibu Spika, hapa kwa masuala haya ya mtiririko ya maisha magumu pamoja na mishahara, ninasema kwamba mishahara ya wafanyakazi ni midogo sana kiasi ambacho mishahara hii, hasa hasa ukianzia kwa wafanyakazi walio chini mishahara yao ni midogo sana, kipato chao wanachokipata kwa maisha yao kwa siku ni kidogo sana ambacho hakiwezi kikakidhi haja.

Mhe. Naibu Spika, mbali na hawa wafanyakazi ambao maslahi yao ni madogo lakini vile vile kwa wataalamu vile vile maslahi yao sio makubwa. Na mishahara takriban wafanyakazi hawa hayawezi kulingana hata siku baina ya sekta na sekta, kwamba sekta hii au wizara hii mfanyakazi mwenye uwezo ule ule, elimu ile ile, uzoefu ule ule na elimu ndio ile ile, lakini ukienda katika wizara nyengine aina zote za sifa utakuta zipo sawa sawa lakini wanapitana katika maslahi ya kipato chao.

Kwa hivyo kupitana kwa sekta na sekta katika masuala ya mishahara, hilo suala ambalo Mhe. Waziri anahitaji kuangalia kwa umakini kabisa; kuhakikisha kwamba hawa wafanyakazi wetu hawapitani kwa maslahi baina ya sekta na sekta. Hivyo nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri ni lini wizara yako itaandaa *scheme of service*, ili *scheme of service* hiyo itawasaidia wafanyakazi wetu kuweza kujinyanyua katika hali yao ya maisha.

Ninaamini kwamba wakati inafanywa *scheme of service* ni bora zaidi kuliko ambako kumpa mtu shilingi ishirini au shilingi ishirini na tano. Fedha hizo hazimsaidii kitu lakini *scheme of service* itaweza kuwasaidia wafanyakazi wale wenye uzoefu, wale wenye muda mrefu na elimu yao, *scheme of service* itakuwa ni kitu kizuri sana ili na wao hawa wafanyakazi waweze kujisikia vizuri sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ninapenda kuzungumza jambo jengine nilizungumze kuhusu suala la taasisi za nyaraka. Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ambayo inashughulikia nyaraka za kitaifa wana kazi ngumu sana. Kazi ambayo ili waweze kuifanya vizuri wanahitaji vifaa ambavyo vitaweza kufanya kazi yao iende vizuri. Lakini la pili zaidi ya hivyo vifaa na wao wenyewe wafanyakazi katika taasisi hii ya nyaraka wanahitaji kuwa na afya nzuri. Na muda mrefu sasa hivi wafanyakazi katika taasisi hii ya nyaraka afya zao si nzuri kutokana na hali yenyewe ya pale ambayo haina utaratibu mzuri.

Kwa hivyo utakuta wanahitaji kuangalia afya zao na vile vile wanahitaji kupata mahitaji muhimu ya kuhakikisha kwamba wanaweza kuzitunza nyaraka zile bila ya kuharibika. Kwa sababu kuna mambo ya msingi katika taasisi hii; kwenye nyaraka kunahitaji kuwa na vitu ambavyo vinaweza kusaidia kama kwa mfano vipoza hewa (*AC*). Hapa inaonesha kwamba zipo mbili lakini zipo tatu nyengine zimeharibika, hazijatengenezwa mpaka leo.

Hivyo kama ikiwa nyaraka hizi ambazo zinadhibitiwa ndani ya jengo lile, hazikuweza kupata vipoza hewa, maana yake ni nini. Maana yake karatasi zilizomo katika taasisi hii, unyevunyevu unaoweza kuingia katika karatasi zile ni rahisi sana kuziharibu karatasi hizi na kuvimba na kupoteza maelezo yaliyomo mule ndani ya nyaraka.

Kwa hivyo, hili suala ambalo tumetolea maelezo muda mrefu kwamba wanahitaji kupata vipoza hewa viwe vya kutosha. Sasa labda nimuulize Mhe. Waziri katika taasisi hii ni vipoza hewa vingapi vinahitajiwa ili kuweza kukamilisha suala zima la nyaraka, kwa sababu hatujui hasa idadi ambayo ya vipoza hewa vinavyotakiwa ndani.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine kuna suala hili la kuweka jengo hili muhimu kwa ajili ya ulinzi wa nyaraka wapate kitu kinachoitwa *CCTV*. Mhe. Naibu Spika, suala hili la *CCTV* katika kuweka fedha zake mpaka leo haijaonesha ni kiasi gani ya fedha zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa kifaa hichi. Kwa hivyo, nilitaka Mhe. Waziri atwambie, kwa sababu hakionekani kifungu chake kipo mahali gani. Tunamuomba Mhe. Waziri atueleze hichi kifungu chake cha kuendeleza kazi hii ya *CCTV* kipo wapi, mbona hatukioni.

Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ina kazi nyengine ya kutoa huduma. Huduma hii inayotoka pale katika taasisi hii inafanyika kwa wenyeji na inafanyika kwa wageni. Lakini mara nyingi shughuli zake zinasita kuendelea kutokana na mahitaji hayatimizwi sawa sawa. Kwa mfano pale yanahitajika madawa ya kuzitengeneza zile karatasi ambazo zimeharibika. Sasa kama dawa haikupatikana ina maana wafanyakazi wapo likizoni, kwa sababu hawana la kufanya, dawa hazipatikani za kutosha.

Haya ni mambo muhimu Mhe. Naibu Spika, na yanahitaji kupatikana. Kupatikana kwa zile dawa ni moja katika maendeleo ya shughuli za kazi za pale ndani ya ofisi ile. Ikiwa dawa hazipatikani, ina maana kazi ndio zimelala na maendeleo ya ile kazi hayaonekani. Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri masuala haya mpaka lini itakuwa kuna upungufu wa madawa, kwa nini madawa haya hayapatikani kwa wakati wake; vifaa pamoja na madawa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine nilitaka nilizungumze ni kuhusu usalama wa wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ya nyaraka ni taasisi ambayo kidogo ina matatizo kwa wafanyakazi. Kama wafanyakazi hawa usalama

haukuwekwa vizuri basi ipo hatari katika afya zao. Hapa kuna suala muhimu kwamba hawa kutokana na kazi zao wapate maziwa kila siku. Suala hili halipatikani. Hivyo, ikiwa suala hili halipatikani na wao wanaendelea kufanya huduma katika zile kazi ambazo katika *strong room* wanatakiwa wabakie mule na ni mahala pa hatari. Kwa hivyo kama maziwa hayapatikani afya zao zinaweza zikawa mbaya. Mhe. Naibu Spika, sasa nimuulize tu Mhe. Waziri ni lini vifaa pamoja na madawa yatapatikana katika ofisi hii. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine tumefurahi kwa upande wa Pemba kwamba na wao katika ofisi yao ya nyaraka walikuwa wanakosa jingo; ambalo jengo hilo lilikuwa sio nzuri katika kuweka huduma za shughuli zao. Lakini bahati nzuri wamepata jengo jengine ambalo kwa kiasi fulani ni zuri. Kwa maelezo tuliyonayo ni kwamba tayari jengo hili limekabidhiwa kwa taasisi hii ya nyaraka za Pemba na ruhusa imetolewa tayari ili shughuli ziweze kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, lakini ningeliomba tu Mhe. Waziri katika jengo hili ambalo tayari zinataka ziwekwe hizi nyaraka. Je, jengo hili limeshatayarishwa vizuri ili kuweka nyaraka hizi ili zisiwe *moisturized* na zikaweza kuharibika karatasi. Kwa sababu si hoja tu kupata jengo lakini shughuli ni ile ile kama iliyokuwepo hapa, na ni shughuli ni ile ile inayotakiwa ifanywe kwa Idara ya Pemba. Lakini je, ile hali yenyewe ya kuhifadhi hizi nyaraka imeshatayarishwa. Kwa kuchelea kwamba zisije zikaharibika.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo ninataka nilizungumze ni juu ya *performance based contract*. Suala la wafanyakazi Mhe. Naibu Spika, ni suala muhimu sana. Mfanyakazi ambapo anataka kupata ajira ya kuingia katika kazi, tuweze kufuata utaratibu ambao unaokubalika. Sikusudii kusema kwamba tusitoe ajira, ajira tutoe lakini wakati tunapotoa ajira kwa mfanyakazi ni lazima tufuate taratibu za ajira.

Mhe. Naibu Spika, tunamuajiri mtu lakini pengine katika ajira tunayomuajiri pengine mfanyakazi huyu hana uwezo mzuri kiutendaji, au pengine inaweza ikatokezea kwamba baadhi ya wafanyakazi uwezo wao wa kiutendaji ni mzuri sana. Sasa lakini mimi ninasema hivi, kabla ya ajira ya kudumu, yaani ile ajira ya kudumu kwamba huyu ni mfanyakazi wa kudumu katika ajira yake. Suala muhimu ni kwamba huyu mfanyakazi ni lazima apewe mkataba wa kupima uwezo, yaani *performance* yake kiutendaji.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kama hakuna kitu kama hicho tukimuingiza tu kama ameajiriwa, pengine uwezo wake katika utendaji sio mzuri au haustahiki. Kwa namna hiyo itakuwa Waziri hawezi kufanya kitu, lakini pale patakapokuwa na mkataba, pindipo kwamba uwezo wake utakuwa ni mzuri na unakubalika basi ajira yake iweze kuwa ya kudumu. Lakini isiwe tu ajira ya kudumu moja kwa moja bila ya kutizamwa *performance* yake.

Hivyo, Mhe. Naibu Spika, nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba kama vile inavyofanya Wizara ya Elimu kwamba mfanyakazi wa Wizara ya Elimu hawezi tu kuwa mfanyakazi bila ya kuwa hajapewa muda maalum wa miaka miwili kufanya kazi na baadae kuthibitishwa kwamba uwezo anao wa kuendelea na kazi.

Hivyo ningependa Mhe. Naibu Spika, atupe maelezo kwenye suala hili. Je, na hapa katika wafanyakazi wote taarifa zao ni za aina moja au ni zile tu zilizopo katika Wizara ya Elimu, kwamba wanakuwa na *probation period*, muda maalum wa miaka miwili halafu mwalimu anathibitishwa kwamba huyu tayari ni mzuri wa kuweza kuendelea na kazi. Je, katika taasisi nyengine hali ni hiyo hiyo au mtu akishaajiriwa ndio moja kwa moja anakuwa ni mfanyakazi wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ungefupisha ukapata na wenzako watatu wakapata kuchangia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante. Mhe. Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ninataka nimalizie ni kuhusu Kamisheni ya Kazi. Kamisheni ya Kazi imepanga kuhakiki taasisi kiasi 240. Lakini inaonekana sheria na sera za kazi haziridhishi hasa katika sekta binafsi. Kwenye mahoteli ambapo vijana wetu wanaajiriwa, wanapewa ajira lakini ajira wanazopewa bila ya mkataba, hazina mkataba.
Na unapomuajiri mtu humpi mkataba, ina maana wakati wowote mtu yule unaweza ukamfukuza. Kwa hivyo anapofukuzwa mtu yule, ina maana kuna mambo ambayo ya maslahi anayakosa. Kwa mfano, zipo stahiki ambazo yeye anazipata. Kwa mfano stahiki hizi zile haki za malipo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ataukosa. Moja ni hilo.

Kwa sababu unapomfukuza mfanyakazi bila ya kuwa na mkataba anakosa haki zake. Mhe. Naibu Spika, sasa ninamuomba Mhe. Waziri kwa nini sheria, sera na kazi hazifuatwi. Hilo nikitaka kumuuliza Mhe. Waziri. Sera zipo

na sheria zipo, kwa nini hawa katika mahoteli hawafuati hii sheria na sera za kazi, kwa nini? Wakati mtu unapomfukuza mara moja katika kazi anakosa haki zake nyingi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo linalowafanya vijana wetu kukosa mwelekeo wa kimaisha anapofukuzwa.

Mhe. Naibu Spika, ninaheshimu wakati wako. Ninashukuru na mimi kwa kunipa nafasi na ninaungana naye Waziri katika hoja hii asilimia mia juu ya mia.
Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa. Nafasi ninampa Mhe. Rufai Said Rufai baadae afuatie Mhe. Fatma Mbarouk Said na tumalizie na Mhe.Salma Mohammed Bilal. Dakika 15 kila mmoja.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kunijaalia mchana huu kupata nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mawazo yangu machache katika hotuba hii ya Mhe. Haroun Ali Suleiman; Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote niungane na wale Wajumbe ambao katika kuchangia kwao wamempa pole Mheshimiwa, na mimi ninampa pole ya dhati kabisa ndani ya moyo wangu. Mwenzetu Mwenyezi Mungu aendelee kumuondoshea matatizo aliyonayo na mengine yasimfike, ili azidi kupata afya njema na aweze kulisukumu gurudumu hili ili tuweze kufanikisha mambo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze ukurasa wa 11, nianze na ofisi yake Mhe. Waziri. Nimpe pongezi nyingi sana Mhe. Waziri, toka tuanze bajeti tena si rahisi Mawaziri kutoa taarifa zao, hiyo ofisi yake kama Waziri. Kwa hivyo sio mfumo mbaya ni mfumo mzuri, mwendo wa Waziri, Baraza linaelewa ziara zake, wageni wake na mambo mengine mbali mbali yanayofanyika katika ofisi yake.

Mhe. Naibu Spika, nishukuru kwamba Mhe. Waziri katika ofisi yake alipata wananchi mbali mbali kumtembelea, ni karibuni wananchi wasiopungua 907 kwa kipindi hiki cha bajeti ya mwaka 2013/14 walitembea katika ofisi yake kwa mambo mbali mbali. Kwa hivyo, nadhani shida zao walizokuwa nazo nahisi zimetatuka.

Pia alipata kutembelewa na Ubalozi wa nchi mbali mbali na ujumbe kutoka *Ras Al Khaimah*. Hawa *Ras Al Khaimah* hata hapa Barazani waliwahi kuja ni miongoni mwa marafiki wa dhati ambao wana mpango mkubwa wa kuisaidia Zanzibar katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo. Kwa hivyo, nadhani katika ugeni huu haukosi lolote la kuelezwa Mhe. Waziri kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar. Sasa katika maelezo haya ningemuomba sana Mhe. Waziri kuzidi kuwafuatilia wageni wake hao waliomfika na wananchi waliokwenda, ili kuhakikisha kwamba yale mazungumzo yenye ufanisi kwa nchi, kuweza kuyatekeleza vizuri ili tuweze kuondoka katika hatua hii tuliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije katika Idara ya Usalama na Afya Kazini. Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba Idara hii ina umuhimu mkubwa katika wizara hii. Ni kweli kwamba baadhi ya wafanyakazi wa serikali wamo katika majengo ya kizamani, majengo ambayo hali za majengo hayo kwa kweli yako hali mbaya sana.

Mfano, jengo la Utawala Bora na Mahakama ya Ardhi na maeneo mengine. Kwa kweli haya ni maeneo ambayo kidogo yako dhaifu na tukiangalia usalama wa wafanyakazi wetu uko katika hali mbaya. Kwa hivyo, ningeishauri sana serikali kusimamia suala hili ili muweze kuwaondosha wafanyakazi wetu katika hali ya hatari, ili lisije kutokea litakalotokea hatima yake tukabeba lawama ambapo sio pahala pake pa kubeba lawama.

Pia usalama wa baadhi ya wafanyakazi ambao ni walemavu, kwa kweli katika wizara mbali mbali majengo yetu hatujawawezesha wafanyakazi wale ni walemavu, ni usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi hawa. Miundombinu tuliyokuwa nayo baadhi ya maeneo mengi ni yale yale ya kizamani inakuwa ni usumbufu kwa wafanyakazi hawa, na hata wale wageni ambao ni walemavu wanakuja kutembelea katika wizara mbali mbali, basi huwa wanapata tabu sana kwenda kufikisha yale ambayo wana matatizo nayo.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuna afya za wafanyakazi. Baadhi ya wafanyakazi wanajitia vitanzi na kujiua au kujinyonga kidogo kidogo bila ya wao wenyewe kuwa na taarifa hizo. Mfano, Mhe. Naibu Spika, uvutaji wa sigara ni jambo ambalo linaathiri sana afya za wafanyakazi na za wananchi wetu. Lakini pia unywaji wa pombe, uvutaji wa bangi na mambo mengine, haya yote yanaathiri sana na yanaua sana wafanyakazi wetu.

Mhe. Naibu Spika, ulevi ni kitu kibaya na baadhi ya wafanyakazi tabia hii wanayo; ya uvutaji wa sigara na vinywaji vyengine. Kwa hivyo, mimi nitaomba sana Mhe. Naibu Spika, hii Idara ya Usalama na Afya Kazini za wafanyakazi, waweze kulisimamia inavyopasa kabisa ili wafanyakazi wetu wawe katika hali nzuri ya afya zao, wanapokuwepo makazini na pale wanapokuja kustaafu, basi wawe bado wanaweza kulitumikia Taifa kwa hali nzuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nizungumzie katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Hapa Mhe. Naibu Spika, utumishi wa umma ninaoukusudia kuuzungumza, wenzangu wamezungumzia maeneo mbali mbali. Mimi nataka nizungumzie wafanyakazi wa serikali hii wa zamani wale waliokwisha kustaafu.

Mhe. Naibu Spika, kuna watumishi wengi wa serikali wa zamani ambao wakati huo waliokuwa wakifanya kazi, mishahara yao ilikuwa ni midogo mno mpaka mtu kufikia kustaafu. Wafanyakazi wa zamani waliostaafu hapa walikuwa wakilipwa mwisho wa mwezi shilingi 20,000 huo ndio ulikuwa mshahara wake wa kazini. Lakini hadi hapa tulipo wafanyakazi hawa hazijaangaliwa zile pencheni zao, bado wanaendelea kulipwa kiinua mgongo chao kidogo mno, pencheni yao inakuwa ni ndogo zaidi ambapo kama mtu ana familia ya watu wanne basi haiwezi kumkifu anapopata hicho kiinua mgongo chake.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ni lazima hawa wametupa damu yao nyingi katika nchi hii au Taifa hili, ni vyema Mhe. Mhe. Waziri na hawa nao mkawaangalia, kwa sababu hawa ndio waliotufikisha hapa tulipo. Kwa hivyo, tusiwe kama wakulima wa migomba. Mkulima wa mgomba, mgomba wake unapotoa ile ndizi basi hutafutia jiti akausegeka ule mgomba, tunaita mwega. Basi mwega ule unakuwa na heshima kweli, lakini siku anayokuja kuchukua ndizi yake basi kitu cha kwanza atakachokidharau ni ule mwega, ndio atakaoukata mwanzo halafu ndio akachukue ile ndizi yake.

Kwa hivyo, tusiwe hivyo Mhe. Naibu Spika, hawa ni wafanyakazi wa muda mrefu wameitoa nchi mbali sana mpaka hapa tulipo. Kwa hivyo, tuwajali kwamba nguvu zao walizozifanya zimewawezesha na wengine, na sisi wengine tukafikia hapa tulipo. Kwa hivyo, naomba sana waangaliwe ili uwezo wa kuweza kuishi maisha haya tuliyonayo, basi na wao angalau tu robo ya maisha waweze kuishi na wao.

Mhe. Naibu Spika, kuna katika Kamisheni ya Utumishi kuna wenzetu hawa wanaofanyakazi katika mahoteli, maeneo mengine ya watu binafsi kama pale viwanda vidogo vidogo, Savana na maeneo mengine. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wafanyakazi hawa hawathaminiwi, baadhi yao hawajaliwi kabisa, hasa hawa wa kima cha chini, huku chini chini.

Mhe. Naibu Spika, hawana ule mkataba wanaokatibiana baina ya muajiri na muajiriwa. Mtu anaweza kufanya kazi miezi mitatu akidai kupata waraka ule wa kuajiriwa, basi hapo yule muajiri sasa anamtafutia kila sababu, ili amfukuze kazi, na wanaofukuzwa kazi sio wale wageni wanaotoka nchi nyengine mbali mbali, anayefukuzwa ni Mzanzibari *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mtu anafanya kazi pengine anakaribia mwaka, ukikaribia mwaka akidai tu basi tayari anafukuzwa, na hawa ni vijana wetu tunao wengi sana, na kila taasisi hasa hizi taasisi binafsi ambazo mpango wao ndio hivyo, basi wananchi wetu wanarudi wanaachishwa kazi zile na wala hakuna kipato chochote ambacho anakipata katika kazi ile aliyokuwa akiifanya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri wizara yako inajitahidi katika masuala mengine mbali mbali, lakini na hizi taasisi za watu binafsi, ni vyema zikafuatiliwa na wananchi wetu wakaweza kupata haki zao ambazo wanazikosa, na huu umekuwa ni mpango maalum kwa wafanyabishara mbali mbali. Akiona hapa tayari atapata wajibu wa kumlipa huyu mfanyakazi kiinua mgongo chake na mambo mengine, basi hutafuta sababu ya kuwafukuza kazi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache niliyochangia na mimi naunga mkono hoja, nasema sina matatizo nayo naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Rufai Said Rufai. Sasa ni zamu ya Mhe. Fatma Mbarouk Said, na Mhe. Salma ajitayarishe.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ili nikaweza kuchangia bajeti hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2014/15, hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma.

Pia nimshukuru Waziri kwa hotuba yake ya bajeti ambayo aliiwasilisha kwa *style* ya kipekee na imefahamika. Mwenyezi Mungu azidi kumpa mema ya uzima, kwa sababu ya uwajibikaji wake na hali yake bado haijaridhisha, lakini tokea jana tunaye hapa na kawasilisha yeye mwenyewe, Mwenyezi Mungu *Inshaallah* amzidishie neema hii.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe Wajumbe wenzangu tumsaidie Mhe. Waziri kupitisha bajeti hii kwa kukosoa na baadaye tushauri, lakini mwisho tufanye wajibu wetu wa kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, ingawaje hapa yanapita maneno ya chini kwa chini hapa, lakini mimi nasema tumsaidie Mhe. Waziri. Wizara hii ina majukumu mazito kwa kila taasisi iliomo ndani ya wizara hii. Ninachokiomba kwa serikali kuzipatia taasisi hizi fedha kama zilivyoombwa, kwani bila ya kuzipatia fedha hizo tutakuwa tunajidanganya, yale malengo waliyojipangia itakuwa ni ndoto tu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali katika ukurasa namba 13. Mhe. Naibu Spika, idara hii kama nilivyosema ina majukumu mazito, ni kwamba kuwapatia mafunzo rasilimali watu. Kwa kweli kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba bila ya elimu basi hapawezi kufanyika kitu chochote na hawa watu ambao tunawasomesha hii ndio rasilimali ya taifa. Kwa hivyo, niipongeze idara hii kwa kutoa mafunzo mbali mbali.

Pia kuandaa na kuchapisha mpango mkakati wa utekelezaji wa sera za mafunzo. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana idara hii kwa kuandaa mpango mkakati, kwani bila ya kuwa na mkakati hatuwezi tukasonga mbele.

Mhe. Naibu Spika, kuna Idara ya Utumishi na Maslahi ya Umma katika ukurasa namba 20 mpaka ukurasa wa 22. Niseme kwamba Idara hii pia ina majukumu mazito na ni lazima iyatizame na iyaangalie, kwa utekelezaji wao lazima wapate bajeti ya kutosha, kwani vile vile niseme kwamba ili utende haki basi na wewe uwatendee wenzio haki. Kwa hivyo, juu ya kuwa ina majukumu muhimu, lakini na wao vile vile wazingatie maslahi ya wenzao, kwani kama hawakuzingatia suala la maslahi ya wenzao basi na wao watakuwa hawakujitendea haki, kwa sababu hili ni jukumu lao.

Idara hiyo hiyo niipongeze kwa kufanya marekebisho ya mishahara ya watumishi wote mwezi wa Oktoba 2013. Hapa imesema kwamba watumishi wenye uzoefu kuanzia miaka 15, nimeona hapa shilingi 150,000 mpaka shilingi 225,000. Kwa kweli hili ni jambo la kulipongeza.

Vile vile kuna jambo jengine la maslahi. Tutizame maslahi ya wale wafanyakazi ambao sasa hivi wamo kazini, lakini kuna maslahi pia tuwatizame na wale wenzetu ambao wameshastaafu kazi katika SMZ. Kuna watu mpaka leo wamestaafu miaka ya nyuma, lakini anapokea labda pencheni ya 7,000, hebu tuzingatie na hili, na atakapokuja na Mhe. Waziri wa Fedha pia nitaliwasilisha tatizo hili ambalo linatukabili kwa wapiga kura wetu. Kwa kweli mtu mpaka leo anapokea shilingi 7,000, hebu tufikirie hii shilingi 7,000 inamsaidia nini mwananchi na hali yetu ambayo tunaijua sasa hivi. Shilingi 7,000 ukiwa na watoto hata kwa chai haitoshi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri pamoja na taasisi nyengine ambazo zinahusika na mambo haya, ni lazima tuzishughulikie taasisi hizi.

Vile vile nije kwenye Idara ya Nyaraka ambayo ni idara yangu ambayo niliifanyia kazi kwa muda mrefu, kabla ya kuja hapa mimi nilikuwepo pale Idara ya Nyaraka na naijua matatizo yake juu chini, chini juu.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba nilikuwa pale na nilikuwa ni Mhasibu wa Idara ile. Nilipokuwa pale kwa kweli sikuwa mgumu kwa kitengo cha *conservation*, ambacho kilikuwa kinahuisha zile nyaraka kwa msimamizi mahiri ambaye alikuwa na uchungu wa nyaraka zile, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi, wiki iliyopita ametutangulia mbele ya haki Marehemu Amour Taib Afadhali.

Nilikuwa anaponiletea kwamba anataka madawa ya kuhuisha; kwa sababu sote tulikuwa tunajua umuhimu wa nyaraka zile, basi sikuwa mgumu kutekeleza. Ningeiomba serikali ikaipa bajeti ya kutosha taasisi hii, na hasa

kifungu cha umeme, kwa sababu kama nilivyosema zile nyaraka zinahitaji kuhuishwa, basi zinahitaji zipate umeme wa kutosha ili kuziendesha zile *AC* zake ziweze kufanya kazi vizuri.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa kwenye idara ile hii Idara ilikuwa chini ya Wizara ya Elimu, tukitizama umuhimu wa elimu na mambo mbali mbali ya Wizara ya Elimu kwa kweli ilikuwa kuwekwa kwenye Wizara ile ni kama kuitelekeza, kwa sababu tunajua umuhimu wa elimu na kuiweka Idara ile kwenye Wizara nzito kama zile kwa kweli ni kuinyima haki zake, na hasa huko nyuma nakumbuka nilipokuwa mimi pale ilikuwa kuna umuhimu wa mambo ya elimu hasa wakati wa mitihani mambo mengi yanajitokeza, kwa hivyo ilikuwa saa nyengine unatizama lipi la mwanzo kulifanya na ukaisahau Idara ile.

Nashukuru huko nyuma ilikuwa fedha zinatumika Mawizarani ilikuwa hazitumiwi sana zile sheria hasa za manunuzi pamoja na sheria za fedha zilikuwa zinatupwa sana, lakini kwa sasa kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye kila mara anakuwa anatoa ripoti zake hapa, na sisi kama kamati ya PAC vile vile tukazisimamia nashukuru kwa kiwango kikubwa matumizi haya kidogo yamebadilika.

Kwa sababu nakumbuka mimi huko nyuma mimi nilipokuwepo pale hii Idara niseme ukweli ilikuwa haiingiziwi fedha kama ipasavyo, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba Idara hii ni muhimu na vile vile wenzangu wamesema kwamba; ile Idara pale kwenye Idara yenyewe kuna nyumba ya mtu, ni kwa nini kipindi chote na najua kwamba mwenyewe mwenye nyumba hii mpaka kwa jina ni la Hadadi naona, kwa hivyo yeye nahisi hana matatizo, akipatiwa pahala pengine anaweza kuhama pale na akapatoa, lakini mpaka leo hii hapajapatikana ufumbuzi wa kupewa pahala pengine hili ni tatizo, ingawaje yeye alikuwa anasaidia kwa sababu pale nyaraka wafanyakazi wakitaka maji na nini wanakwenda mule, si kama ni tatizo kwamba labda ana nia mbaya ya ile Idara; anaisaidia sana hata maji tulikuwa tunatumia kwake yeye pale. Lakini hatuoni sababu ya kwa nini mpaka leo hii ikawa hakujapatikana ufumbuzi wa kupatiwa angalau mahala pengine na yeye akakaa.

Mhe. Naibu Spika, niende na Kamisheni ya Kazi humu kwenye kitabu naona haikuelezwa majukumu yake, ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja basi anieleze kwa ufupi majukumu ya Kamisheni ya Kazi, lakini punde hivi nimepata masikitiko nimetumiwa meseji kwamba kuna mfanyakazi mmoja alikuwa anafanyia kazi Chama cha Wafanyakazi, *CHADAU;* nafikiri chama cha wafanyakazi wa Mahoteli, nimetumiwa hapa kwamba amefukuzwa kenda kulalamika sasa hivi na hii kesi sasa hivi ipo Mahkamani, hebu niulize Mhe. Waziri ikiwa chama chenyewe Chama cha Wafanyakazi kinasema kwamba ni chama cha wafanyakazi lakini pia kinakiuka yale masharti ya kazi, mimi nasema Kamisheni hii iwe inasimamia vizuri au usajili labda wa haya makampuni. Kwa sababu haiwezekani chama chenyewe ni cha wafanyakazi lakini pia nacho kinakiuka yale masharti ya kazi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niseme kwamba nimshukuru sana, niendelee kumshukuru Waziri na niwaombe wenzangu waipitishe bajeti hii. Mimi mara nyingi huwa nasema hapa bila ya mashirikiano yetu sisi pamoja na wenzetu hawa Mawaziri palipokuwa na kosa tukosoe, lakini nasikitishwa na wenzangu ambao hukaa humu tumo katika kusema maneno ya kuponda na kukejeli, na sijui kwa nini kejeli hizi zinakuja sote tupo dau moja. Nakumbuka ule mchezo wa biti Khamis na mumewe aliyemwambia kwamba tuko kizani, akamwambia twalala banda moja, kwa hivyo si vizuri tukawa kila mara tunaponda. Palipokuwa na tatizo tuseme na palipokuwa na haki, kafiri mchinjeni lakini haki yake mpeni.

Baada ya hayo nashukuru kwa kunipa fursa hii, naunga mkono hoja ya hotuba hii mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Baada ya hapo naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya, vile vile naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nakuahidi nitatumia muda mdogo tu, kwa sababu mara nyingi mtu anapofika mwisho kwenye sahani hujiona anaramba akaona ni utamu, kumbe anaramba mikono yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu kutumia nafasi hii kumpa pole Mhe. Waziri, kwa mitihani Mwenyezi Mungu aliyotwambia atatupa akiwa yeye alipewa mtihani wa ugonjwa, na vile vile namuomba Mwenyezi Mungu ampe afuweni zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nianze na Idara ya Ajira. Hii ni Idara muhimu sana katika nchi lakini utekelezaji wake wa kazi unadorora mno, vijana wengi hawana kazi na wamekata tamaa kabisa, na hakuonekani na mipango ya

Serikali kupitia Idara hii kupata ufumbuzi wa suala hili na kwa kuukosa umakini kwa Idara hii imeshindwa hadi hivi sasa kuweka taarifa sahihi ya soko la ajira na imeanza kubangaiza bangaiza.

Mhe. Naibu Spika, mfano katika ukurasa wa 31 aya ya 54 kifungu kidogo cha 3 naomba ninukuu ‘‘Ziara ya ufuatiliaji zimefanyika kwa Wilaya ya Mkoani na Chake Chake, wilaya hizi zimesaidia kuzalisha ajira 112 kupitia nafasi za biashara katika soko la Chake Chake’’ mwisho wa kunukuu.

Hapa naomba nimuulize Mhe. Waziri hilo soko la Chake Chake lililozalisha ajira 112 kwa mwaka huu analijua, hivi pale sokoni pana nafasi za biashara zinazofika 112 Mhe. Naibu Spika, mimi naona huko ni kubangaiza, ni vyema Waziri asidanganywe akaja kutudanganya na sisi, ni kweli alipata ugonjwa lakini watendaji wake wasiutumie ugonjwa wa Mhe. Waziri vibaya, ni nani atakayedanganyika kwamba pale soko la Chake Chake pana ajira 112. Sasa Mhe. Naibu Spika, ikiwa sera zinazosimamiwa katika upatikanaji wa ajira kwa wananchi isiwe mtu anakuja kuuza kombe na chaza kutoka Wesha na akapata shilingi elfu moja kwa siku ikahisabiwa kwamba ni uzalishaji wa ajira.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kidogo nigusie Kamisheni ya Kazi ingawa ndio hivyo kuramba mikono, Kamisheni ya kazi nayo inaonekana kusimamia majukumu yake lakini Serikali ilipoamua kuanzisha sekta ya utalii mategemeo yake ni kwamba Wazanzibari wapate kazi kwenye hoteli hizo. Lakini kwa masikitiko makubwa kazi kwenye hoteli hizo wengi waliopo ni wageni sio Wazanzibari, wenye hoteli wameachiliwa na Kamisheni ya Kazi wanafanya wanavyotaka, kuna waajiriwa wa mahoteli wanaleta ndugu zao kutoka kwao na kuja kuchukua nafasi za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hawa Wazanzibari wachache wanaoajiriwa wananyanyaswa na kufukuzwa kazi ovyo huku wenye hoteli wakitamba kwamba Kamisheni ya Kazi wanayo mfukoni, sasa namuomba hapa Mhe. Waziri atueleze kwa nini anaachia mambo haya ni sababu zipi?

Mhe. Naibu Spika, sasa naona nizungumzie kidogo Kamisheni ya Utumishi ya Umma ambako nako kuna mashaka mengi. Kamisheni hii imeshindwa kutoa miongozo kwa Tume ya Utumishi. Tume ya Utumishi Serikalini ilipaswa kuweka kigezo cha waliomaliza mwanzo chuo ndio wapate ajira mwanzo, lakini la kusikitisha Mhe. Naibu Spika, kuna watu ambao wamemaliza chuo tokea mwaka 2007 lakini waliopata ajira ni watu waliomaliza chuo 2013 hii sio haki. Na kwa hakika suala hili Mhe. Naibu Spika, linaashiria upendeleo, ujamaa na udugu. Serikalini haitakiwi iende hivyo, atizamwe yule aliyemaliza mwanzo, huyu aliyemaliza 2007 hajaajiriwa anaajiriwa aliyemaliza 2013 huyu aliyemaliza 2007 kakusudiwa nini? Halafu wakiondoka watu kwenda kutafuta ajira kwengine unasikia hawana uzalendo, uzalendo utapatikana wapi.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nije katika Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi. Mimi hapa sitokuwa na mchango mkubwa lakini namuomba Mhe. Waziri atakaposimama aniambie hawa wakuu wa Idara wana tatizo gani kwa sababu Mhe. Naibu Spika, 2012/13 nilichangia hapa, 2014/15 nilichangia na niliambiwa kwamba hawa wakuu wa Idara wanashughulikiwa maslahi yao, hivyo kweli Mhe. Naibu Spika, wamkabidhi mtu Idara nzima aiongoze lakini hakuna posho, wakati dereva wa Afsa Mdhamini, taarishi, wote wanapata posho ile nayo ni dhamana kubwa hebu Mhe. Waziri atwambie kuna tatizo gani hapa?

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nije katika ukurasa wa 57 katika Kiambatanisho Namba moja kuna asilimia ya mapato yaliyokusanywa ni 17. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri aniambie kuna sababu yoyote wakati mahoteli yote yana wafanyakazi wasiokuwa Wazanzibari au mapato yanaliwa, namuomba hapa Mhe. Waziri anipe jibu.

Vile vile nakwenda kwenye Kiambatanisho ukurasa wa 58 kiambatanisho namba 1(b) matumizi mengineyo kwa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa wamepatiwa asilimia 4 tu ya Makadirio yaliyopitishwa na Baraza lako tukufu, Je watendaji hawa wa Idara hii wakikosa ufanisi watalaumiwa. Namuomba Mhe. Waziri hapa anifahamishe au hii asilimia nne tu kweli itafanya nini au tuwalaumu hawafanyi wajibu wao wakati matumizi mengineyo ni asilimia nne, hapa naomba maelezo, vyenginevyo nisiporidhika nitazuia fungu la Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na kama nilivyosema nitatumia muda mdogo sana kwa sababu ukiramba utamu unaramba mkono wewe unapata utamu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kuambiwa kuwa nitamalizia jioni, kwanza nishukuru Mwenyezi Mungu. Umeambiwa “*Waidhaa maridhtu fahuwa yashifiyn*”. Mwenzetu ameumwa kafika mbali kwa matibabu nashukuru Mwenyezi Mungu kamsaidia na dua zetu, kwa hivyo tumshukuru Mwenyezi Mungu

kwa hilo, na tumuombe Mwenyezi Mungu amrejeshee afya yake kuliko ya zamani ili aendelee na kazi pamoja na Mawaziri wenzake kwa maslahi ya nchi hii.

La pili Mhe. Naibu Spika, kutokana na wakati kwanza niseme kuwa kitabu kimeandikika kimefahamika, na kwa sababu hiyo yapo baadhi ya mambo kidogo tunataka ufafanuzi, na moja kwa moja nianze kwa Kiambatanisho cha 1(c) ambacho kiko ukurasa wa 60.

Mhe. Naibu Spika, Kiambatanisho hiki kinahusiana na Muhtasari wa Mapato na matumizi ya fedha za maendeleo kwa mwezi wa Julai, mwaka 2013 mpaka Machi mwaka 2014. Hapa pana vifungu vinne tofauti; kuna ajira mbaya kwa watoto ilitakiwa kifungu hiki kiingiziwe milioni 50 lakini hakuna hata moja iliyoingizwa ni 0%. Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma milioni 100 imeingiziwa milioni 12.5 ni asilimia 13 tu, Programu ya Taifa ya kujenga uwezo ilitakiwa kuingiziwa milioni 150 zilizoingizwa ni milioni 15.493 tu sawa na asilimia 10 na ya mwisho ni *e-government* ambayo iliidhinishiwa kuingizwa milioni 450 lakini zilizoingia ni milioni 11.9835 ikiwa ni sawa na asilimia 3.

Mheshimiwa ukiangalia katika hali hii nasikitika kuwa Serikali kwa makusudi au kwa bahati mbaya lakini imeidhalilisha sana hii Wizara, sijaona kifungu hata kimoja katika Wizara zote kilichoingiziwa 0% isipokuwa Wizara hii, kwa hivyo ikiwa kuna maelezo yoyote ya sababu hiyo na fungu lote hili kuingiziwa asilimia 6 naomba nipate maelezo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni Kiambatanisho 2(a) ambacho kipo ukurasa wa 61 na hichi kinazungumzia idadi ya wafanyakazi waliopo masomoni kwa mafunzo ya muda mrefu ambao wanagharamiwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/14, jumla yao ni wanaume 8 wanawake 8 wote ni 16. Naipongeza Wizara kwa hali yake mbaya ya kifedha ilivyo ikaweza kusomesha watu wake nje kwa gharama za Wizara yenyewe.

Jengine ni Kiambatanisho 3(a) ambacho hiki kipo ukurasa wa 63 kiambatanisho hiki kinahusiana na aina ya mafunzo ya muda mfupi yaliyotolewa kwa wafanyakazi wa Wizara kwa mwaka 2013/14 yaani hawa wote wanatoka Unguja, jumla yao ni 16, wanaume 11 na wanawake 5 lakini naomba kujua tu kwamba kama kule Pemba kulikuwa hakuna haja ya watu kama hawa kupewa mafunzo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa naomba umalizie hapo utamalizia jioni. Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa ushirikiano wa pamoja tangu asubuhi hadi sasa hivi, kwa hivyo naakhirisha kikao chetu hadi Saa 11:00 jioni ya leo.

(Saa 7:00 Mchana Baraza liliakhirishwa mpaka Saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, nimearifiwa kwamba Mheshimiwa Salim Abdalla Hamad amebakiza dakika chache sana na hajakubali kuzisamehe. Karibu Mheshimiwa nimeambiwa una dakika 5 zilizobaki.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kuendelea kwa sababu ya wakati naendelea na kiambatanisho cha 3(a) ambacho kiko ukurasa wa 64 kiambatanisho hiki kinaeleza kuhusu wale waliopatiwa mafunzo mafupi nchi mbali mbali.

Mhe. Spika, nchi zenyewe zilizotajwa katika viambatanisho hivi ni India, China na Korea na tunayo jumla ya wanafunzi 120 wa aina hiyo; wanaume wakiwa 68 na wanawake 52 hili tunampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi yake, na kwa sababu ya wakati moja kwa moja twende kiambatanisho cha 8(b) 6(a) kilioko ukurasa wa 82 kiambatanisho hiki Mhe. Spika, kinaelezea kuhusu mawakala 7 wa ajira waliokaguliwa. Ninamshukuru Mheshimiwa, kiambatanisho cha 6(a) kinaelezea ajira zilizopatikana ambazo ni ajira 889 na ajira hizi ni za nchi za nje, kuna Djibout, Oman, UAE, Saudi Arabia, Qatar pamoja na Yemen. Hapa naomba kupata maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, hapo awali kulikuwa na mpango kama huu wa vijana wetu kuajiriwa katika nchi za nje, lakini Mhe. Waziri kwa kuona kwamba mazingira ya waajiriwa kutokana na vijana wetu wanaotoka hapa na ajira zilizokuwepo huko kwa wakati huo haziendi vizuri hakukubaliana moja kwa moja na wazo lile, na mimi ninalipongeza kwa sababu tunataka ajira ambayo ni ajira halali kabisa.

Lakini kwa kuangalia hivi sasa ndio tunao vijana hao 859 walioajiriwa nchi mbali mbali, mimi ningeliomba kujua kuwa je zile sababu zilizomfanya Mhe. Waziri kwa wakati ule kukataa vijana wetu kuajiriwa walikwishakata *passport* na kila kitu na sasa hivi ndio limekubalika, ile sababu tayari kwa alivyokuwa akiona yeye mambo yameshakaa sawa.

Halafu (b) tukiangalia katika ajira hizi jumla ya wanaume ni 343 tu na wanawake ni 516 kwa asilimia wanaume ni 39.9 na wanawake ni asilimia 60.1 tukiona wanawake ni wengi sana. Suala la pili, je hizi ajira za wanawake zilikuwa wengi kuliko za wanaume ndio ikawa hivi, na halafu kwa sababu ni wanawake Mheshimiwa atatwambia hadhari aliyoichukua ili isijekuwa ajira hizi zikasababisha mmong'onyoko wa maadili yetu kwa huko wanakofanya kazi.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, kwa mambo mengine ya ajira, katika nchi yetu tunayo ajira ya aina mbili. Kuna wale ambao ni wa kudumu na wanapostaafu wanapata haki zao pamoja na pencheni endelevu mpaka mwisho wa maisha yao, na kuna wale ambao tokea walipoanza kazi ni watoto hawajaoa mpaka sasa hivi, tena wengine ndio wameshafika wakati wa kustaafu na wengine wameshastaafu wamebakia kama ni wafanyakazi wa siku au wa muda; yaani tunasema *daily worker*. Hawa wanapoacha kazi kwa sababu ya kuzeeka au kwa sababu zozote ambazo zinawafanya wasiweze kufanya kazi, maskini hawana mambo wanayopata au stahiki wanazopata kama wale waliokuwa ni wafanyakazi wa kudumu.

Je, Mhe. Waziri haoni kuwa wakati umefika kwa wale walioajiriwa mpaka hivi sasa kuwa wanaendelea na kulipwa kila siku wakafanywa wa kudumu ili watakapozeeka wakati wanafanya kazi sawa sawa na wale wa kudumu na wao wapate haki hizo. Nimshukuru sana ndugu yangu Mustafa Aboud Jumbe alipokuwa katika Shirika la Bandari alikuwa ni Mkurugenzi Mkuu, kulikuwa na wafanyakazi wengi sana tu ambao ni wafanyakazi wa kutwa, lakini baada ya kumpa ushauri huu wengi aliwaajiri.

Vile vile suala kama hili limetokea katika hoteli yetu ya Bwawani lakini bado kuna taasisi. Hata huko Shirika la Bandari na Taasisi nyengine hasa haya mashirika wapo watu aina hii maskini baada ya kumaliza muda wao wanaondoka bila ya chochote. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri awajue hawa ni wangapi, awaangalie mazingira yao na ikiwezekana na wao waajiriwe kwa kudumu ili wapate haki zao wakati wa kustaafu.

Jengine Mheshimiwa niisifu Wizara kuwa inashughulikia malalamiko mengi ya wafanyakazi kaeleza humu na sababu waliorejeshwa waliokuwa wameshindwa na kadhalika, lakini ile kuyashughulikia matatizo ya wafanyakazi ni jambo kubwa sana, angalau akiona mtu kwamba amedhulumiwa au yeyote ana matatizo anajua pa kuelekea. Lakini bado kuna wengine mpaka sasa hivi maskini sijui ni kwa sababu ya uenyeji au vipi wameshindwa.

Mfano mimi kwa bahati mbaya nilikutana na kijana mmoja anaitwa Salma Ali Mussa huyu alikuwa akifanya kazi katika vyama vya wafanyakazi, alianza kazi mwaka 2007. Kwanza alikwenda muda wa miaka 4 mfululizo hajalipwa haki yake yaani ninakusudia mshahara mpaka akalipwa tarehe 4/2/2011. Ile pesa ya kuanzia mwezi wa Saba mpaka Januari 2011 mpaka leo hajaipata. Huyu mama kwa bahati mbaya kauguliwa na mtoto wake maradhi mazito ikabidi asafiri kutoka Pemba kuja Unguja, na aliaga na akafanya kazi huku, lakini aliporudi Pemba baada ya matibabu au baada ya kumtibu mtoto wake kufika kule akapata barua ya kufukuzwa kazi, na barua hii ilikuwa ni ya tarehe 13/05/2014 ni ya juzi tu. Huyu mama maskini ya Mungu ndio hajui pa kwenda hajui pa kurudi. Pengine wapo wengi wa aina hii, kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri watu kama hawa tukimpelekea wakati tunaona katika kitabu chake kuna watu wengi binafsi aliowapokea na tunashukuru kwa hilo na huyu amsikilize ili na yeye apate haki zake.

La mwisho Mheshimiwa kwa sababu nimepewa muda mdogo, nilikuwa ninashukuru kwa hapa Zanzibar inapotokea ajira huwa inatangazwa na ikishatangazwa huwa kunatakiwa sifa na watu huenda wakaomba. Lakini kutokana na hali ya mazingira ilivyo wako wale wenye sifa ambao wamemaliza hivi karibuni na kuna wengine wameshakaa siku nyingi sana bado hawajaajiriwa, lakini wote wametimiza sifa. Maajabu tunayoyaona na mifano tunayo lakini si vizuri kuyatoa hapa kwa sababu ni kumuingilia mtu katika haki yake ya maamuzi.

Kuna wengine hivi karibuni wameajiriwa lakini kuna wengine wenye sifa kama zile za muda mrefu hawajaajiriwa mpaka leo. Kwa hivyo ninamuomba pia Mhe. Waziri zaidi ya ile roho yake safi kabisa kuwa kila mtu mwenye haki yake apate; ya kutangaza mambo haya na watu wakafuatilia ni vizuri, kwa sababu anayo ile ajira ya kazi katika Wizara yake, afuatilie na huu uajiri unakwenda vipi, kwa vile tuna watu wengi sana hivi sasa wamemaliza masomo wana sifa, lakini kwa sababu ya udogo wa nchi yetu bado hawajaajiriwa.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, ninashukuru sana ninaomba kukaa kitako.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa na mimi nafasi niweze kuchangia kidogo kwa yale ambayo yanahusiana na ajira hasa katika hotuba yetu ili watu waweze kuyafahamu, halafu tuanze kufuata taratibu kwa sababu sheria ndizo zinazotutaka tuache kufanya yale ambayo tulokuwa…

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru kwa kunipa nafasi hii napenda sasa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uwezo kusimama hapa, lakini pia kwa kunipa nafasi ili niweze kumshukuru Waziri anayehusika kwa kuwa jasiri pia kwamba hali yake ilikuwa ngumu, lakini Mungu kampa uwezo wa kusimama hapa kuja kutetea Wizara yake. Sisi kama watendaji wa Wizara ya Afya tumejitahidi kwa kadri tulivyoweza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kuona kwamba tumefanikisha na leo tuko naye hapa.

Mhe. Spika, katika mazungumzo ya watu waliozungumza hapa yalitajwa kuhusu Bima ya Afya. Bima ya Afya iko chini ya Wizara ya Afya, haiku chini ya Wizara yake, na sisi ndio…

Mhe. Spika: Mheshimiwa hebu ielekee zaidi hiyo *microphone* ili upate kusikika vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nilikuwa nataka nizungumzie suala ambalo limezungumzwa hapa kuhusu Bima ya Afya ni kweli kilichosemwa kwamba Bima ya Afya kama ingekuwa imeshaanza ingetusaidia kwa kiasi kikubwa kupata fedha, na matatizo mengi ya afya yangeweza kutatuka na watu wangepata huduma zilizo bora.

Wizara ya Afya imepewa jukumu hilo na limo kwenye maandalizi na sasa hivi kuna muelekezi ambaye anakamilisha taratibu za mwisho ili waraka huo upelekwe kwa Makatibu Wakuu na hatimaye Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kupewa ruhusa ili tuweze kuletewa mswada hapa upitishwe kwa ajili ya kupitisha huduma za afya. Kwa hivyo ninaomba Waheshimiwa Wawakilishi wawe kidogo na subira, hayo mambo yanaandaliwa na tunauelewa umuhimu wa jambo hilo.

Jambo jengine ambalo ningependa kulisemea kuhusu wafanyakazi wetu. Sisi kama Wizara ya Afya tatizo letu kubwa ni wafanyakazi. Tunajitahidi kwa kadiri tunavyoweza tunamuajiri kila ambaye anastahiki kuajiriwa Wizara ya Afya kwa kufuata taratibu zilizopo; kwa kutangaza nafasi tulizonazo na kupitia kwenye Tume zinazohusika na kufanyiwa taratibu zote za ajira baadae tunaruhusiwa kuajiri.

Lakini Mhe. Spika, kwa nini imenilazimu nisimame. Kuna vitu ambavyo kama Wizara ya Afya vinatuvunja moyo, kwa sababu sisi tunaajiri wale wote wanaohusika na mabo hayo, lakini sasa hivi kila ukitizama bado unatukuta pengo halishi. Kwa sababu kwanza watu sasa hivi wanaokuja Wizara ya Afya wanaoingia Chuoni wanaingia kwa madhumuni mamoja makubwa ya kujua kwamba ukiingia Chuo cha Afya ukitoka pale kazi utapata, kwa sababu tuna *deficit* kubwa na tunaruhusiwa kuajiri. Kwa hivyo hilo linawapa matumaini lakini wakati mwengine hilo hilo sisi linatuathiri kwa sababu wakati tunapoajiri watu tunakuwa tumeshapiga hesabu kwamba kwa kiasi fulani tutakuwa tumepunguza pengo. Lakini wale wanaopita pale wanapita tu pale kama ngazi ya maisha, mtu unamuajiri hajaanza kazi hata siku moja anatoka anakwenda kujiunga kwenye Chuo, unayemuajiri anayetakiwa akae pale miaka 2 aende akasome hakai pale miaka kusoma, akifika anageuza anakwenda kwenye Chuo chengine. Kwa hivyo wanashindwa kufuata taratibu zilizowekwa. Wanashindwa wao na wale ambao wanaowasaidia. Maana hata kama tukiwakatalia, kuna watu wana nguvu za kuweza kuwatoa pale wakaenda wakasoma. Kwa hiyo hilo kwa kweli linatuvunja moyo.

Mimi naomba tufuateni taratibu zilizowekwa. Sio hivyo tu sisi Wizara ya Afya tuna kada zetu ambazo tungependa watu wazifuate, kama umekuja kama nesi kuna mambo mengi yanayohitajika kwa manesi kuyasoma mpaka kufikia kwenye Masters Degree. Lakini mtu anakuja pale anaanza kuwa nesi akisha anatoka anakwenda kwenye *human resources* kitu ambacho hakitusaidii na kurudi hataki tena kuwa nesi, wakati nesi sisi wenye pengo nalo.

Kwa hivyo mimi nawaomba watu wakija Wizara ya Afya naomba watufuate vile tunavyotaka, kwa sababu sisi tuna mpango wetu wa miaka 5 tunajikuta kwamba hatufanikiwi, kwa sababu wanaingia wengi kwa utaratibu mwengine na wakifika kule wanakwenda njia ambayo sisi kwetu si sahihi. Na tukijaribu kuwazuia wenye nguvu wanatwambia kwamba ooo kusoma mtu anaweza akaanzia popote akisha akamalizia popote, hiyo kweli kwa kwetu haitusaidii.

Kwa hivyo ninaomba jamani ushirikiano wa wale ambao wanatufanyia hivi watuachie, kwa sababu tuna mipango tumeshapanga na tuna shida kuajiri. Kwa hivyo naomba watu wakija pale wajue kwamba wanakuja kusoma, na wakisoma mambo ya afya wabaki kwenye afya. Kwa sababu hizo kada nyengine wanazozisoma zimejaa tele sokoni, kwa hivyo tukitaka tutaajiri hao wengine.

Lakini pia nataka niseme wanapoingia Chuo cha Afya Mbweni. Wanapoingia Chuo cha Afya Mbweni tunasema kwamba tunataka watu wenye *credit* 2, kwanza biology na ya pili nyengine yoyote ambayo ni ya *science*. Hao wapo tele wenye *credit* hizo. Lakini pia wapo wenye *credit* kubwa zaidi ya hizi unaweza ukamkuta mtu ana C tatu mpaka nne, anakuja Wizara ya Afya wale wanawapa *first priority* Chuoni wanawaingiza lakini watu wale wale wanaweza kuingia form V na VI, wanakuja pale huku wanajiunga Chuo cha Afya huku wanasoma form VI. Matokeo yake anazuia nafasi kwa wengine hawaingii ha-*perform* vizuri anaendelea kusoma kwengine. Anaomba Chuo cha Afya anaomba na vyuo vyengine anazuia nafasi kwa wengine, yeye Chuoni kwetu haji halafu wale wengine wamekosa nafasi.

Sasa mimi ningewaomba kwa sababu hili nalo linaleta athari kwa skuli zetu za sekondari. Siku hizi Zanzibar pameingia dhana moja na wazee na watoto wameichukulia kasi, kwamba ukifika form IV uende Chuoni, form V na form VI ukiingia hutoki na *credit* matokeo yake Skuli za Sekondari zinabakia hazina watu na watu wote wanakuja kwenye vyuo lakini pale wanapita njia; wakimaliza hapo wanakwenda kwenye Vyuo na wale wanaostahiki wanakosa nafasi za kusoma.

Kwa sasa hivi Wizara ya Afya tayari Chuo kimeanza kudahili watoto, tungependa wale ambao wana *credit* 2, ambapo hawawezi kwenda vyuo wale ndio waje wajisajili na wale ndio tutawapa *priority* kwa sababu ndio wale ambao wanaobaki baada ya kwisha kusoma. Kwa sababu ili waweze kwenda vyuo vyengine inabidi wafanye kazi miaka 2 halafu ndio waende kwenye vyuo vyengine. Kwa hivyo tukipata mfanyakazi angalau miaka 2 halafu sheria inamruhusu inakuwa kwetu ni rahisi.

Kwa hivyo tukipata wengi hao ndio tutakaowachukua. Kwa hivyo msije mkatuona wabaya kwa sababu tumeshaiona athari ya kuwachukua watu wenye *credit* nyingi lakini baadae hawafuati taratibu.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho kinaudhi ni hao ambao wanaoingia halafu wakabadilisha kada. Kuna wanafunzi hao ambao wao maisha ni wanafunzi wanaingia Wizara ya Afya wakitoka *course* hii wanakwenda *course* nyengine, ukiwakataza ndiyo hao wenye ma-*god father*, lakini wanawaruhusu, maisha analipwa mshahara na kazi hafanyi na anaongezewa vyeo pamoja na mshahara kazi hafanyi. Nasema hivi, msitutafutie shari jamani, tunataka sheria zifuatwe. Sasa yule atakayeshindwa kufuata sheria tukiona kama anaendelea na utaratibu na huo tutaomba, sasa sheria ichukue mkondo wake kwa sababu haiwezi mtu miaka kumi anapokea mshahara na haifanyii kazi Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda kumpongeza waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya na Mungu atakusaidia bajeti itapita tuko hapa pamoja na wewe kwa sababu matatizo yaliyopo mengine hayako kwenye uwezo wake na mengine yako kwenye mchakato, *Inshaallah* mambo yatakuwa mazuri na sote tutafaidika. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi yha Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii ya leo na mimi kupata fursa ya kuichangia hotuba ya bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, na mimi nimuombee kwa Mwenyezi Mungu Mhe. Haroun Ali Suleiman amzidishie afya njema ili aendelee kulitumikia Taifa letu na vile vile aweze kuendelea kuwatumia wananchi wake wa Jimbo la Makunduchi.

Mhe. Spika, pili, nikupongeze na mimi kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa maoni machache kuhusiana na masuala mbali mbali yanayohusu hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, mimi kwanza nimpongeze na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Waziri kwa umahiri wake na umakini wake wakuweza kuwasilisha hotuba yake na kutusomea yeye mwenyewe kuonesha hali ya Mwenyezi Mungu aliyomjaalia ya kumuwezesha kuwa na afya nzuri.

Mhe. Spika, lakini kabla sijasahau ningependa niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia 100 kwamba tuweze kuruhusu Baraza lako tukufu tuungane tumruhusu baada ya kwisha kuichangia ili aweze kutekeleza majukumu yake kama maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wengine walivyosema na wale ambao wamedhamiria kumuondeshea shilingi ningeomba wakamrejeshea shilingi yake ili akaweza kutekeleza majukumu yake vizuri na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma si mgumu kupokea maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sasa moja kwa moja baada ya utangulizi huo, ningependa nianze kwenye mchango, wako Wajumbe ambao wamesema hawaungi mkono kitabu hiki kuanzia nje ya gamba mpaka ndani na kwa sababu tu ya picha pengine iliyopo mbele na kusema kwamba mwenye punda atawekwa mkiani.

Mhe. Spika, mimi nadhani Waheshimiwa tukubali kwamba hii Ofisi inaitwa Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, mwenye punda yuko mbele Dk. Ali Mohammed Shein na hii picha ni ya tukio miongoni mwa matukio mwa *function* za Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma. Tukio hili ni la siku ya *May Day* wafanyakazi Jumuiya ya Wafanyakazi (*ZATU*) sheria zao zinasimamiwa na Wizara ya Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, kwa sababu hili ni tukio ililazimika lazima hili tukio lioneshwe katika hotuba hii. Kwa hiyo, isiwe tabu pengine inawezekana kaonekana mtu mwengine hapa, lakini nae huyu alikuwa katika majukumu yakukaimu nafasi ya Waziri wa Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, na kwa wakati ule Waheshimiwa waliokuwa wakiniuliza masuala ya kazi hawakuhoji suala la kuwekwa mwenye punda kuwekwa mkiani, kwa sababu nilikuwa nakaimu. Sasa mimi nadhani isiwe sababu hii yakutoa shilingi na kutokuikubali, ni utaratibu tu wa kikazi ndiyo ambao umefanya picha hii iwepo hapa na mwenye punda hayuko mkiani, maana Rais wa Zanzibar ndiyo yuko hapa mbele.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, nataka na mimi niseme kwa ridhaa ya Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma nataka nichukue nafasi hii kueleza mambo machache sana.
Mhe. Spika, limezungumzwa sana suala la miundo ya utumishi (*Scheme of service*). Nataka nichukue nafasi hii kulichangia eneo hili na kusema yafuatayo;

Mhe. Spika, mara nyingi sana suala *la Scheme of service* inalinganishwa unapoidhinisha muundo wa utumishi, basi uidhinishe na viwango vya mishahara ya watumishi. Ni kweli ni vitu viwili vinavyotegemeana kwamba saa nyengine mshahara unategemea *Scheme of service*, lakini siyo sahihi kwamba unapoidhinisha muundo wa utumishi ndipo wakati huo huo unatakiwa uidhinishe kiwango cha mshahara mpya.

Mhe. Spika, sasa mimi nataka niseme kwamba karibu taasisi zote, mihimili yote ya dola na taasisi nyengine za serikali, taasisi nyengine za Idara Maalum Miundo ya Utumishi imeshaidhinishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Tatizo linakuja pale unapopeleka muundo wa utumishi ukapeleka na mapendekezo ya fedha yatekelezwe ndani ya ule muundo wa utumishi.

Mhe. Spika, lakini nataka nithibitishe hapa na Mhe. Waziri atakuja kuniunga mkono kwamba suala la *Scheme of service* za taasisi zote tayari zimeshaidhinishwa mpaka *Scheme of service* ya Baraza lako tukufu muundo wake umeshaidhinishwa, kilichobakia sasa ni kuwa *fitting*, watumishi katika daraja zao na kuwaweka kila mmoja na daraja yake na hatimae suala la viwango vya mishahara vitaendana na viwango vya viwango vya mishahara vilivyoidhinishwa na serikali kwa mujibu wa *scheme* hiyo na pale ambapo mfanyakazi kapunjwa kwa lugha nyepesi, anatakiwa afanyiwe marekebisho ili mshahara wake ulingane na *scheme* ilivyo.

Mhe. Spika, sasa mimi niendelee kushirikiana na Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma kuwaomba viongozi wa taasisi kwamba walishughulikie hili suala la kuwaweka watumishi kwa mujibu wa miundo ya watumishi kwenye daraja zao na ngazi zao ili litakapokuja suala la kuwapandisha mishahara iwe rahisi kuweza kufanya hivyo.

Mhe. Spika, na hili limezungumzwa katika Ofisi hii na hapa nataka nitumie fursa vile vile ya kuzungumzia suala la viongozi wa Baraza kwa maana ya Wakurugenzi.

Mhe. Spika, Wakurugenzi wa Baraza la Wawakilishi ni kweli mwaka jana lilijitokeza suala hili, lakini mara tu baada ya kumaliza bajeti hapa suala hili lilirekebishwa na Wakurugenzi wote wa Baraza waliweza kurekebishiwa mishahara yao sawa na wakurugenzi wengine wa taasisi nyengine na hili lilikuja tu kwa sababu ya mazungumzo na muwala mzuri kati ya mihimili hii, muhimili wa serikali na muhimili wa Baraza la Wawakilishi na hilo jambo lilitekelezwa.

Mhe. Spika, tunakubali kwamba ilitokea kasoro baada ya marekebisho ya mwezi wa kumi, kasoro hii ilitokezea baada ya serikali kutoa *circular* kwa taasisi zote za serikali, Wakurugenzi wa Baraza la Wawakilishi walichelewa kurekebishiwa ile tofauti kati ya Wakurugenzi wa nje na Wakurugenzi wa Baraza la Wawakilishi na hili nalo nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma kwamba hili jambo tayari sasa limeshamalizika.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya suala la mikataba ya watumishi wanaomaliza muda wa kufanya kazi. Ni kweli mkiangalia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama watakumbuka vizuri kwenye sheria yetu ile ya utumishi wa umma…

Mhe. Spika: Mhe. Rashid hebu mkutano umalizike.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Kama tutakumbuka vizuri sheria yetu ile ya utumishi wa umma, sheria Nam. 2 ya mwaka 2011 kwa mujibu wa sheria ile inaruhusu kumuajiri mfanyakazi kwa mkataba. Ndani ya sheria ile inaruhusu kumuajiri mfanyakazi kwa mkataba na inaruhusu kumuajiri mfanyakazi kwa mkataba siyo kila mfanyakazi anaweza akaajiriwa kwa mkataba, lakini mkataba huu siyo huu ule mnaoupigia makofi, ni mkataba wa utumishi serikalini au kwenye taasisi ya umma.

Mhe. Spika, inaruhusu kumuajiri mfanyakazi kwa mujibu wa sheria, kumuongezea muda wa miaka miwili na kumalizia muda wa mwaka mmoja na masharti yake ni kwamba inatakiwa unapomuajiri kutumia kifungu kile asichukue maslahi yake yale ya mwisho ya kiinua cha mgongo ili aunganishe na muda ambao ataajiriwa kwa mkataba maalum wa utumishi wake wa miaka miwili au miaka mitatu.

Mhe. Spika, na haiku wazi, yaani haiko kwamba kila mtumishi anaweza akaajiriwa, hapana inaangaliwa katika taasisi ile fani ambayo anayo yule mtumishi kama hakuna mtu mwengine au wapo wenye *qualification* zile, lakini wanahitaji kuandaliwa. Serikali au taasisi inaweza ikaomba kibali maalum kupitia Tume ya Utumishi husika na hatimae kupata ridhaa ya mkuu wa utumishi serikalini (Katibu Mkuu Kiongozi) hilo jambo linaweza likafanyika.

Mhe. Spika, lakini kama tutakumbuka vile vile Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kwenye mwaka 2012 tumeleta marekebisho madogo na hapa kwa ridhaa ya Mhe. Waziri nataka nilizungumzie suala la *Rare profession*. Ile sheria tulileta marekebisho ya sheria kuruhusu kuajiri watu kwa utaratibu huu wa *Rare profession* na inampa mamlaka Mhe. Waziri kutangaza kwenye gazeti rasmi la serikali, pindipo inapoonekana kwamba kwenye taasisi fulani kunahitajika mtaalamu fulani ambaye hayupo katika taasisi ile, lakini yuko nje ya ajira za serikali kuitangaza nafasi hii katika gazeti rasmi la serikali na hatimae kumuajiri mtaalamu yule.

Mhe. Spika, na kwenye mikutano mengine iliyopita niliwahi kusema kwamba ilitokezea siku moja kwenye Wizara ya Afya kuna uchache wa madaktari hasa waliokuwa na *profession* fulani hawapo, lakini serikali inawahitaji pamoja na kwamba hawa hawako serikalini, basi waziri ana nafasi ya kuweza kutangaza nafasi ile ili mtumishi yule aweze kuajiriwa na kuweza kulisaidia Taifa.

Mhe. Spika, pia, iliwahi kutokea katika Wizara ya Kilimo kulikuwa na mtaalamu mmoja tu wa udongo na mtaalamu yule akawa ameshamaliza muda wake wa kazi na bahati mbaya akawa hakupata nafasi ya kupewa ajira ya mkataba wa muda. Kwa hiyo, inabidi nafasi ile lazima waziri aitangaze kwenye gazeti rasmi ili mtaalamu yule serikali iweze kumuajiri kwa njia hiyo ya *Rare profession* au kwa mkataba maalum.

Mhe. Spika, jengine ambalo kwa ridhaa ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ambalo limejitokeza kuzungumzwa na ningependa nilichangie, ni suala zima la wafanyakazi kupewa muda maalum

wa kuangaliwa baada ya mkataba wa awali wa uwajiri ambao wenyewe wataalamu wanaita *Under probation* anakuwa kwenye kipindi maalum cha kuangaliwa. Utaratibu huo upo bado serikalini wakutizamwa mfanyakazi katika kipindi cha miezi sita, halafu anathibitishwa kazini.

Mhe. Spika, tunakiri kwamba lipo tatizo saa nyengine mfanyakazi akiwepo katika kipindi hiki anachukua muda mrefu hajathibitishwa kazi. Katika uhakiki ambao ulifanyika katika miaka ya hivi karibuni ilibainika baadhi ya taasisi wanapompa *probation*, mfanyakazi basi ndiyo inakuwa *probation* anaendelea kufanya kazi bila ya kupata barua ya kuthibitishwa kwamba huyu atakuwa ni mfanyakazi muajiriwa katika serikali baada ya kuangaliwa uwezo wake wa kuweza kufanya kazi sehemu ya kazi.

Mhe. Spika, nataka nirejee lile eneo la *Scheme of service* ambalo limezungumzwa sana na hasa kuhusu suala zima la *Scheme of service* ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, nalo hili liko katika *package* ile ile ya *scheme* zote za taasisi zote za serikali kwamba zimeidhinishwa na hivi sasa serikali ilichoahidi katika eneo hili kwamba hawa wakaguzi wa hesabu za serikali, yaani wale ma-*auditors* wanaofanya kazi katika Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Mkuu wa Serikali na wao watapata *special treatment* au watakuwa *conceded* kama walivyokuwa wafanyakazi wa *State Attorney*, wafanyakazi wa *DPP* na wafanyakazi wengine wa taasisi nyengine wafanyakazi wa afya kuangaliwa maslahi yao ili na wao waweze ku-*benefit* katika utumishi wao.

Mhe. Spika, na hili jambo litafanyika kabla ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015, yaani watazingatiwa katika bajeti hii inayomalizia sasa, hivi sasa kinachofanyika ni *Internal consultation* hili jambo liweze kumalizika na waweze kuingia katika bajeti hii ambayo inamalizika tarehe 30, mwezi wa Juni na wao wawe wame-*benefit* katika kupata maslahi yao.

Mhe. Spika, najua jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wangependa kulisikia ni suala la kuwalinganisha *Auditors* na mishahara ya ma-*chief accountants.*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kuna tofauti ya mshahara wa mkuu wa idara na mshahara wa mfanyakazi anayelipwa kwa mujibu wa *profession*, kwa mujibu wa *qualification* na kwa mujibu wa ngazi yake ya kazi anayoifanya. Sasa hili nalo nataka tulielewe vizuri, lakini kwa maana ya serikali kuelewa umuhimu wa wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama alivyosema Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora na Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma kweli hili jambo imelishughulikia na hivi sasa inalikamisha ili kabla ya tarehe 30, June hawa wawe wame-*benefit* kama walivyo-*benefit* wafanyakazi wa kada nyengine kama afya, *State Attorney* na maeneo mengine ambayo yame-*benefit* katika kupata maslahi mazuri.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilitaka nilizungumze ni suala zima lile alilozungumza rafiki yangu muasisi pale na mimi nilifurahi sana alipozungumzia mfano wa *Administrator* ambao wanatoka Vitongoji, Tumbatu na kwengineko, lakini alipofika sasa kuwa mfyeka majani akenda kwa Mtumbatu moja kwa moja hakutoa mfano kwa watu kutoka Vitongoji. Sasa Mheshimiwa angekuwa *fair* kwa kuwa kaanza na ma-*administrators* ambao ni wasomi wenye fani tofauti kwa watu wa Vitongoji, Tumbatu na kwengineko, ama na kule kwa wafyeka majani angekwenda kwa watu wa Vitongoji na kwengineko asingewabakisha Watumbatu peke yao. Sasa hapa kidogo naona hakunitendea haki mimi Mtumbatu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini kama angesema mfano wake angeutoa kwamba wafyeka majani atoke Kitongoji, lakini watalii pia kupelekwa baharini, lakini manahodha wa boti wa kuwatembeza watalii wakatoka Tumbatu hapo ningemuunga mkono kwa asilimia mia moja. Kwa sababu huo ndio ukweli wenyewe, lakini unapomnasibisha *Administrator* na Mtumbatu, halafu baadae unapokuja kwenye *field* ukamuweka Mtumbatu ndio mfyeka majani, nadhani sio sahihi. Sasa najua hili atakuwa kalisema kwa sababu pengine atakuwa hakuliangalia vizuri. Nataka nimwambie rafiki yangu kwamba *treatment* ambazo zinafanywa kwa Wazanzibari zifanyike kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, sasa Mhe. Waziri atakapopata nafasi atakuja kusema sisi kama serikali, hili jambo tumelizingatia na tumeliangalia na ndio maana hata juzi tu ulifanyika mkutano wa vijana unaozungumzia suala la mikakati ya ajira. Mjue Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali sio kwamba tupo tupo tu, lakini haya mambo tunayafanyia kazi na mkutano ule aliufungua mwenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar ila na mimi nataka niungane na Mhe. Asha Bakari Makame pale aliposema kwamba Wazanzibari sasa tuwe na tabia ya kutokuchagua

kazi, kwamba kazi tunahisi ni ile ya kuajiriwa serikalini au kuajiriwa pahala pa kwenda kuchukua mshahara na ndio maana hapa leo nimewasikia Wajumbe wana *element* ya kuuliza, eti anayeuza chaza sokoni sio ajira?

Mhe. Spika, Ajira ni kitu chochote kile ambacho kinampa mtu riski halali ya kuweza kuendesha maisha yake, ndio maana vile vile kuna watu wanaweza wakahoji uchomaji chokaa ni kiwanda, uchomaji mikate ni kiwanda, kwa mujibu wa vigezo vya Kimataifa, uchimbaji wa mawe nao ni kiwanda, susagaji wa kokoto nao ni kiwanda. Kwa hiyo, ajira ni jambo lolote lile ambalo linaweza kumpatia mtu maslahi na riski halali ikaweza kumuendeshea maisha yake na ndio maana vigezo vya ajira vinasema kuwe na ajira za staha, kuwe na ajira nyengine. Sasa ajira ambayo inakupa riski halali hiyo ni ajira ya staha, sasa ikiwa unauza chaza, ikiwa unachokoa chaza, ikiwa unafanya nini, madhali hiyo inakupa maslahi na kupata riski halali, hiyo ni ajira tayari. Sasa atakapokuja Mhe. Waziri yeye ni mtaalamu zaidi wa masuala haya, atakuja kuongezea nyama katika kutoa ufafanuzi mzuri juu ya suala hili.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo mdogo sana, naomba nirejee kusema naunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu, hotuba hii ya bajeit ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa tokea jana nimekuwa mtulivu sana kama kawaida yangu na nimekuwa nikiwasikiliza Waheshimiwa wote waliochangia kwa *study* mbali mbali.

Mhe. Spika, bahati mbaya wakati nikiwasilisha bajeti yangu wewe ulikuwa hupo, lakini Naibu Spika, alifanya kazi nzuri sana hapa na nilimpa salamu zangu kwa niaba yangu kukushukuru wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoendelea kufanya, nikatoa mfano tokea kule Dodoma mpaka hapa bado unaendelea kufanya kazi nzuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakusaidia.

Mhe. Spika, lakini jengine niliwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza, niliona ni vizuri kulisema hapa katika kipindi chote ambacho Mwenyezi Mungu alinipa mitihani walishirikiana na mimi kwa asilimia mia moja. Nawashukuru sana na bado wanaendelea kuniombea Mwenyezi Mungu na *Inshaallah* naomba vile vile, Mwenyezi Mungu awajaalie wapate imani wakumbuke kwamba nilikuwa kwenye homa wasiendelee kuniwekea vikwazo katika bajeti yangu hii na dua ikiombwa na mgonjwa, basi hairudi inakubaliwa tu na mimi nawaombe kheri *Inshaallah. (Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu sasa kwanza niwataje wale wote waliochangia hotuba yangu hii, jumla ya waliochangia kwa kusema ni 23 na waliochangia kwa maandishi ni 5. Kwa ruhusa yako naomba kuwataja:

1. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Ali Salum Haji
6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
7. Mhe. Mussa Ali Hassan
8. Mhe. Hija Hassan Hija
10. Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa
11. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
12. Mhe. Saleh Nassor Juma
13. Mhe. Mohammed Haji Khalid
14. Mhe. Subeit Khamis Faki
15. Mhe. Asha Bakari Makame
16. Mhe. Amina Idd Mabrouk
17. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
18. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
19. Mhe. Rufai Said Rufai
20. Mhe. Fatma Mbarouk Said
21. Mhe. Salma Mohammed Ali
22. Mhe. Salim Abdalla Hamad

Wengine;
Mhe. Naibu Waziri wa Afya
Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum

Waliochangia kwa Maandishi ni;
Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Marina Joel Thomas na
Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

Mhe. Spika, kwa sababu maalum na kwa aina ya kipekee namshukuru sana Kaimu Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati wote nikiwa nje ya Ofisi na bado anaendelea kuifanya. Kwa kweli kwa hapa amenisaidia sana leo kunijibia masuala mengi mazito ambayo yangenipa muda kuyajibu na watu wakanielewa, lakini nashukuru sana amenisaidia.

Mhe. Spika, pia, sikufanya dhambi hata kidogo kwenye kitabu changu cha bajeti kumuweka ukurasa wa mbele. Nilifanya hivyo, mimi sikumuangalia yeye, nimemuangalia Rais wangu wa nchi ambaye nampenda sana anatufanyia mengi na alihudhuria kwenye sherehe muhimu sana ya wafanyakazi na mimi wizara yangu inahusiana na wafanyakazi wote wakiwemo Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi nawashughulikia mimi, mambo yao mbali mbali na *Inshaallah* bado mambo ni mazuri tutazidi kuyashughulikia.

Mhe. Spika, lakini pia, ni kuonesha kwamba sina upendeleo na mtu, haki yake apewe. Sikujiweka nyuma kwa sababu sijipendi mimi, najipenda kweli kweli na ndio maana najitahidi kujiangalia afya yangu sasa hivi. Kwa hivyo, picha ile ya juu ilikuwa na umuhimu wa kueleza siku ya *May Day* na ile picha ya nyuma ilikuwa inazungumzia masuala ya ajira kwa vijana. Kwa hiyo, hakukuwa na tatizo lolote.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, basi kitabu kizima aseme hakiungi mkono! Hamna chochote! Unaniomba radhi mimi mwalimu wako nikusamehe, nasema nitakusamehe, lakini kauli kama zile zisituvunje moyo sisi. Lakini ndio ulezi, bado nahitajia kukulea na nitazidi kukulea *Inshaallah,* lakini ulikuwa waziri, ukawa mwanafunzi wangu na bado unaendelea kuwa kiongozi unawakilisha wananchi wa Jimbo la Kwamtipura. Wananchi wa jimbo langu la Makunduchi wamesikia wananambia Mhe. Hamza Hassan Juma kile kitabu chako chote kakiona hakina maana, nikawaambia nitakupelekeeni salamu leo hii zitafika na mtasikia, lakini nimejitahidi kutengeneza kitabu na nawashukuru wale wote waliokisifu na wale ambao kwa bahati mbaya hawakuridhika akiwemo Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, nashukuru wengine walitoa shilingi zao, sio kwa sababu ya kitabu kibaya, kwa sababu zao za kimsingi na wala sina tatizo nao, lakini Mhe. Hamza Hssan Juma moja kwa moja yeye alisema kitabu kile hakifai kabisa na hakiungi mkono kuanzia mbele mpaka nyuma. Sasa nikasema hii kazi itakuwa kubwa sana, lakini hata hivyo, ndio ulezi bado tutaendelea kuleana.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na napenda nikiri kwamba Waheshimiwa Wajumbe wametusaidia sana. Mimi mwenyewe kipindi cha miezi mitatu nilikuwa sipo ofisini, lakini wamenielimisha mambo mengi sana na leo mchana baada ya kuakhirisha, nilikwenda ofisini nimekaa na watendaji na nimepata taarifa nzuri ambazo zimenisaidia na nyengine nilikuwa sizijui baada ya Waheshimiwa hawa kuchangia. Nashukuru sana nimepata taarifa nitajitahidi kadiri nitakavyoweza kujibu yale mambo ambayo nitaweza kuyajibu.

Mhe. Spika, lakini namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kama nilivyosema amenisaidia sana. Naibu Waziri wa Afya nae amenisaidia kujibu suala la Bima ya Afya na mambo mengine ambayo amenisaidia hata nilipopata mtihani huu, yeye kule Hospitali ya Mnazi Mmoja alifanya kazi saa 24 kusema kweli mpaka akahakikisha kwamba naingizwa kwenye ndege na vifaa vya kusaidia pumzi (*Oxygen*) alihakikisha kwamba vifaa hivyo tunavyo kwenye ndege. Kwa hivyo, atakayemlipa ni Mwenyezi Mungu *Inshaallah.(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile, nawashukuru Waheshimiwa wote walioniombea dua na waendelee kutuombea dua, Mwenyezi Mungu atatupa afya njema na tutakuwa wazima kama kawaida.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye baadhi ya hoja muhimu za kimsingi. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nianze naye rafiki yangu na naanza naye si kwa sababu nyengine yoyote, lakini nataka nimpe taarifa nzuri tu. Baada ya kufuatilia suala alilolizungumza la yule mtu anayemwita "Muhindi mkorofi", kwa sababu Wahindi wote siwakorofi, lakini yule mkorofi na inaelekea ni kweli, kwa sababu ukorofi hauna kabila wala hauna rangi.

Mhe. Spika, nitajitahidi kutoa ufafanuzi na anielewe rafiki yangu kwa sababu sitaki aendelee kujenga nyumba ambayo italeta matatizo baadae. Mwaka jana aliniwekea vikwazo vizito sana tukang'ang'anua, hata mwisho *Alhamdulillah* tukaelewana na bado amesimama tena kwa suala lile lile.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nitampa hadithi kwanza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Kuna mtu mmoja alikwenda kumtembelea jamaa fulani Makunduchi huko, basi baada ya kufika tu akamuuliza ndio kwanza unafika? Akamwambia si ndo umeniona, akamuuliza safari lini? Sasa hebu tutizame wewe mgeni umekwenda mahala kufika tu unaulizwa safari lini, ndio panakalika hapo? Hapo hapakaliki. Sasa huyu jamaa alifanya makosa mwaka jana akafanya kosa la kwanza akaitwa wizarani kwangu akapewa na onyo na akaambiwa kwamba ukiendelea kufanya hivi tutachukua hatua zaidi za kisheria.

Mhe. Spika, maafisa wangu walichukua jitihada hizo na bahati nzuri na nampongeza sana Mhe. Makame Mshimba kwa kufuatilia kwake alikwenda naye Afisa wangu yule kule na wakapata taarifa rasmi kwamba, vile vitendo bado anaendelea navyo kwa kuwanyanyasa wafanyakazi wa Zanzibar. Mimi ni mtu mmoja ambaye sitokubali Wazanzibari kunyanyaswa katika taasisi zetu. Niliwafukuza si mara moja, wala mbili wafanyakazi tena wakubwa Mameneja wa Hoteli na wakapewa masaa 24 tu, kuna moja Lagema na Mhe. Asha Bakari Makame ni shahidi. Nilikwenda katika Hoteli fulani nikanyanyaswa na mfanyakazi meneja fulani pale na siku ya pili tu akahama, hatutothubutu kuachia mambo kama hayo.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kuna taarifa nimezipata za uhakika kwamba yule bwana na yule mgeni aliyemuuliza unaondoka lini. Sasa na yeye kaamua mwenyewe kuandika barua ya kuacha kazi. Kwa hivyo, *Inshaallah* ataondoka na kama hakuondoka kwa hiari, ataondoka kwa lazima kwa sababu nitalisimamia mimi mwenyewe. Hivyo, tuvute subira *Inshaallah* mambo yatakaa sawa, nadhani mmeridhika sana, makofi yaashiria hivyo na mimi nakubali kwamba kuna uelewa mkubwa sana wa masuala haya hasa kwa sababu nafuatilia vizuri.

Mhe. Spika, kwenye hoja nyengine zilizojitokeza ni kukamilisha sera za malipo ya mishahara. Wizara inaendelea na uandishi wa sera ya malipo ya watumishi wa umma na rasimu ya awali inatarajiwa kukamilika mwezi wa Julai. Kwa hivyo, masuala haya yatakamilika ikifika Julai tukijaaliwa.

Mhe. Spika, maslahi duni wanayolipwa watendaji hasa katika ngazi ya utaalamu. Serikali inaendelea kuinua maslahi ya watumishi kadiri ya hali ya uchumi itavyokuwa inaruhusu, tutajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu Mfuko wa Bima, nashukuru sana Naibu Waziri wa Afya amenisaidia, amejibu vizuri sana. Ukweli Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008, Idara ya Nyaraka inaitambua kama ile ni taasisi kamili, ni masuala ya mazowea tu, tunaita idara, lakini ile ni Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, ndivyo inavyoitwa rasmi. Nashukuru sana kwa michango kuhusiana na jengo la nyaraka au Taasisi ya Nyaraka. Mambo yaliyotokea pale ya wizi ni kweli yametokezea wala hatuwezi kuyaficha na yamejadiliwa kwenye vikao vikubwa sana serikalini na serikali ikaunda Tume ikapeleka kule na tayari taarifa zote zishapatikana na wahusika wamekiri kwamba wamefanya makosa yale. Mimi mwenyewe nimewaita bahati mbaya wakati ule kabla sijapata mtihani ilikuwa tayari masuala haya yashatokea.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nikawaita wakakiri kwamba yametendeka na bahati nzuri yule mhusika naye nikamwita pamoja na Afisa wa Ubalozi wa Oman, kumbe yule alikuwa si mfanyakazi wa Ubalozi, isipokuwa alikuja na jukumu la kusimamia ukarabati wa jengo la Beit - El- Ajaib, kapewa kama dhamana ya kusimamia, lakini kwa vile anatokea kule, ndio maana yake mara nyingi alikuwa anakwenda Ubalozi wa Oman. Hata sisi tunaposafiri nje ya nchi wakati mwengine madhali tunatokea Tanzania au Zanzibar kama kuna Ofisi yetu ya Tanzania huwa mara nyingi tunakwenda kusalimia salimia. Ni jambo zuri la kawaida tu kama utamaduni.

Mhe. Spika, sasa na huyu kijana alikuwa anatumia nafasi ile na kukamilisha taratibu, alikataa, lakini bahati nzuri tulifuatilia kwa makini sana hata simu zilizopigwa zote kuanzia siku ya kwanza aliyoanza mawasiliano na wale vijana mpaka walipokuwa wanakutana, simu zilizokuwa zinajibishana zote tumezipata. Kwa hivyo, hakukuwa na njia ya kukataa suala lile. Serikali imeshachukua hatua zaidi sasa hivi na wale vijana wamechukuliwa hatua na hatua inayofuata sasa hivi kwa taarifa ni kwamba tunataka tuhakikishe zile *documents* zilizochukuliwa zinarejeshwa hapa Zanzibar. Kwa sababu ile ni mali yetu na lazima irejeshwe na kwa kweli tulikuwa na makubaliano na wenzetu wa Oman ilikuwa tu-*sign.*

Mhe. Spika, lakini tukazuia kwanza saini ile mpaka hapo tutakapokamilisha taratibu zetu hizi za ufuatiliaji wa *documents* hizi. Kwa sababu ile ni hazina yetu na haiwezi kupotea hivi hivi tu. Mheshimiwa yamefanyika mambo hayo na yamethibitishwa kwamba ni kweli na hatuwezi kuficha kweli yamefanyika, pametokea uzembe mkubwa pale, vijana wetu walighilibiwa na shilingi hamsini elfu na laki moja tu basi.

Mhe. Spika, hii ni hatari sana, *documents* za serikali kuchukuliwa au kuibiwa. Tunaziuza *documents* hizi hata shilingi milioni ishirini au thalathini huzipati popote duniani, kwa sababu zile zilikuwa zinapatikana hapa hapa Zanzibar tu. Leo vijana wetu kwa tamaa ile wamezitoa, lakini serikali imelivalia njuga jambo hilo na imelichukulia *very seriously* na hatutoliacha tutaliendeleza mpaka tujue mwisho wake tukijaaliwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe tujue tu kwamba masuala hayo tunayafanyia kazi na tunayafuatilia kwa makini kabisa.

Mhe. Spika, suala la *CCTV cameras*, ni kweli limechelewa na serikali imeshatoa maelekezo tununuliwe *CCTV*. Tumeshaomba pesa Wizara ya Fedha, wakatulipia pesa kwanza milioni ishirini, bei yake ni *fourty five millions*. Tumepata awamu ya pili milioni ishirini na tano. Kwa hiyo, tunatarajia milioni arubaini na tano, zikipatikana *Inshaallah* hivi karibuni tutaweka ile kamera kama Waheshimiwa Wajumbe wengi walivyosema ni muhimu sana. Ingekuwepo tokea mapema ile kamera, wale wezi tungewaona, lakini sasa bahati mbaya haipo. Kwa hiyo, kuonekana yenyewe wameonekana kwa utaratibu mwengine, lakini wanajulikana na kama nilivyosema tumewakamata na wameshughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa hiyo, tukijaaliwa kamera ile itapatikana na tusiwe na mashaka yoyote tutabandika na tutaiweka mnamohusika, isipokuwa sasa hivi ilikuwa ina sehemu nyengine nyeti zaidi zinawekwa zile kamera, wakimaliza kazi watakuja kutuwekea na sisi vile vile.

Mhe. Spika, suala la ajira limezungumzwa kwa wingi sana na Waheshimiwa wengi. Ajira kwa wazalendo tumesema ndio *priority*. Mimi niliwahi kuwaita mameneja wa mahoteli yote, nikawaambia kuanzia sasa hivi kwa kazi zote ambazo zina uwezo wa kufanywa na Wazanzibari sitoruhusu wala sitotoa mkataba mpya kuwapa wageni na msimamo huo ninao na sitoubadilisha. Wageni kokote wanakotoka nje ya Zanzibar, huyo ni mgeni. Tunachotaka sisi tuhakikishe kwamba Wazanzibari wanazo sifa zile ambazo zinahitajika kwa nafasi ile.

Mhe. Spika, wakati mwengine hatuna budi ndio tunatangaza hizo nafasi nyengine kwa sababu hakuna watu wenye utaalamu ule, lakini kwa kweli tungefurahi. Bahati nzuri tumefanya *survey* yetu, tumegundua hoteli nyingi sana Wazanzibari au wazalendo ni wengi zaidi kuliko wageni, isipokuwa sasa unakuta mahali, unakuta mfagiaji, unajua wakati mwengine hawa wanapewa hawana mikataba, wanawachukua kienyeji huko huko. Sasa na hiyo tunaifuatilia. Wale wote ambao wamepewa ajira bila ya kupewa mikataba tutawafuatilia na tutachukua hatua za kufaa.

Mhe. Spika, lakini haiwezekani kufagia na kutandika kitanda, kwani hata kutandika kitanda kunataka Kiengereza, huhitaji kuzungumza Kizungu, Kiswahili kinatosha. Ukenda China na Japan wanazungumzia lugha zao tu wale na kama umo chumbani anakusemesha Kichina au Kijapan, ukitaka utatoka, hutaki utatoka tu, kwa sababu ameshazungumza.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala zima hapa na Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu Muundo wa Utumishi wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Haji Omar Kheir kalitolea ufafanuzi kwa kina, lakini wakati nipo hapa Mhe. Hamza pamoja na mchango wake akaniletea michango ya maandishi ya nyongeza na akasisitiza kwenye barua zake kwamba nitaendelea kuzuia shilingi yako. Heee! Mhe. Hamza, kuna mmoja kanitania hapa anasema hawa Waheshimiwa wanavyochangia kama ulikwenda Al-Rahma, sasa utapelekwa Kidongo Chekundu.

Mhe. Spika, namna wanavyochangia hawa hawana huruma na wewe, wana nia gani hawa. Nikawaambia hapana ni haki yao na ndio demokrasia. Sasa Mhe. Hamza Hassan Juma umeniandikia kwenye barua ile au taarifa ile ya

nyongeza ile kwamba endapo imekwama kweli kwangu mimi na umesema kama uwezo ninao. Mimi ni Waziri kweli na Kamisheni ipo chini yangu na kama limekwama Wizarani kwangu, mimi ninakuhakikishia wiki hii hii litakwamuka tukijaaliwa hakuna matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini taarifa nilizokuwa nazo na nilizozipata kwamba hapa hapa Barazani zimeshaletwa taarifa hizo, maelekezo yameshatolewa utaratibu wa kutumia na kama marekebisho hayo yafanyike vipi. Kama alivyoeleza Mhe. Haji Omar Kheir na kwenye kada ni hivyo hivyo. Sasa ni kupanga zile *level* na *grade* mbali mbali za kuwarekebishia mambo yao.

Mhe. Spika, ninawapenda sana nyinyi wafanyakazi wote wa serikali. Ninashukuru sana wafanyakazi kwa jinsi ya mashirikiano tunavyoyapata na naomba sana Mhe. Hamza Hassan Juma wewe ni hodari wa kufuatilia. Sasa nikushauri tu wewe pamoja na rafiki yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk manung'uniko kama haya yakija usingoje kwenye vikao hapa, tuleteeni Ofisini kwetu moja kwa moja, njooni. Kama wafanyakazi wa Baraza wana matatizo na Waziri wa Utumishi wanamjua, kweli nilikuwa mgonjwa mimi, lakini Kaimu Waziri alikuwepo.

Mhe. Spika, kama kuna tatizo mitaani huko, sasa wale wananchi wafanyakazi wanakuja kwenu nyinyi, nyinyi hamji kwetu kutuona mpaka mnangojea vikao kama hivi. Jamani hamtutendei haki hivyo. Mimi Mhe. Hamza Hassan Juma nakupenda sana na nitaendelea kwa sababu ulinisaidia hata joho langu la ukamanda wa vijana ulinishonea wewe. Sitosahau hisani zako kwa mambo mazuri uliyonifanyia, lakini nitazidi kukuelimisha mpaka unielewe tukijaaliwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, vibali nimeshasema nishawaambia kwa wazalendo, kwa vile ambavyo vimetoka ndio vimeshatoka. Vikimalizika muda wake hakuna ku-*renew* kwa wageni, watapewa wazalendo na hilo naomba tusaidiane inapotokezea matatizo popote, njooni mara moja na mimi hatua kali za kisheria nitachukua. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna tatizo limejitokeza hapa na naomba nikiri ilikuwaje na Waheshimiwa wengi wamelizungumza hilo kwamba tulisema tutakusanya shilingi milioni mia nane na ishirini kama hivi sikosei. Kwa bahati mbaya tumekusanya shilingi mia moja na hamsini na saba. Tatizo ilikuwa ni nini. Mhe. Hamza Hassan Juma analijua suala hili na Waheshimiwa wengine walilizungumza sana. Tatizo ni hili mwaka jana tulikuwa na nia, si kuwakomoa wageni, lakini ni kuchunguza idadi ya wale wageni kufanya kazi katika mahoteli na taasisi zetu, tukasema tupandishe ada kutoka dola mia moja na hamsini, tuweke elfu mbili ili wavunjike moyo.

Mhe. Spika, sasa taarifa zile zilikuwa ni siri ndani ya kikao chetu cha ndani cha Wizara. Zilitokatokaje mpaka zikawafika wale watu wa *ZAT*, Mhe. Hamza Hasan Juma nakumbuka alinipigia simu mara nyingi, anasema mmepandisha ada wageni hawatokuja, watalii watakimbia. Kibali kile cha kufanyia kazi tukasema kutoka mia moja na hamsini tukipandishe elfu mbili na kwa bahati mbaya sana kilichojitokeza Wizarani kwangu walipokwenda Wizara ya Fedha wakaripoti kile kiwango cha dola elfu mbili.

Mhe. Spika, sasa Wizara ya Fedha wakafurahi kwamba tutapata mapato mengi zaidi, lakini ilikuwa maamuzi hayajapitishwa hata Waziri hajaidhinisha. Kwa hiyo, naomba radhi kwa makosa yaliyotendeka yalikuwa nje ya uwezo wetu, sio kama ya makusudi, ndio maana yake mwaka huu tukasema tutakusanya mia mbili na thamanini tumeshajipima, kwa sababu sasa hivi tunachofanya ni nini. Mimi nimewaita *ZAT* wale, nikawaita nikakaa nao vizuri, nikawaambia jamani kakaeni wenyewe muamue mtatuongezea shilingi ngapi, serikali inataka mapato.

Mhe. Spika, wakenda wakakaa wenyewe badala ya dola mia moja na hamsini wakaja na pendekezo la dola mia tatu. Kwa hiyo, sasa hivi wanalipa dola mia tatu wakitaka *permit* yao ya kufanyia kazi na watakao-*renew* wanalipa mia mbili na hamsini, pesa zitaongezeka serikalini na tumefanya mahesabu kwa mujibu wa kipato chetu cha sasa hivi tutakachokuwa tunakipata. Kwa hiyo, yalitokea matatizo, sio kwamba watu wangu walikuwa wavivu kukusanya zile pesa hapana, isipokuwa kulikuwa na masuala ya kimsingi, haya ndio nimeyazungumza kwa makosa ile bajeti ilipelekwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha wakatia kwenye mabuku yao kama ni sehemu ya mapato, ndio maana ikajitokeza milioni 800 na sitoweza kudanganya kwa sababu ndio ukweli wenyewe ulivyokuwa kwenye vitabu vya hesabu na ndio maana hii bajeti nikaandika vile vile 820.

Mhe. Spika, Ajira za nje, nawashukuru sana Waheshimiwa waliopongeza kwa ajira zilizopatikana nje ya nchi na tunaendelea kuhangaika. Tukisafiri kwenda nje wakati mwengine tunatumia pesa, lakini tukifika kule tunafanya mazungumzo na wenzetu na *Alhamdulillah* tunatarajia wiki hii wakati wowote kuna ujumbe utakwenda Qatar

kwenda kukamilisha baadhi ya taratibu na baadae vile vile *Inshaallah* kuna na nchi nyengine kama Saudia na nyengine nazo tunakusudia kuingia nao mikataba kwa ajili vijana waende wakafanye kazi kule.

Mhe. Spika, wengine wamerejeshwa, kuna kesi za kurejeshwa wafanyakazi, mmoja karejeshwa kwa sababu kaonekana ana matatizo ya UKIMWI, kwa bahati mbaya sana hawawezi kumkubali yule, mmoja karejeshwa kwa sababu anasema ananyanyaswa, yeye mwenyewe kaamua kurudi tu. Mmoja karejea kwa sababu unajua mtu akiwa hajaondoka hapa kama hajenda nje ana hamu sana ya kufika kule nje, lakini akishafika kule nje anatamani siku ya pili arudi hapa hapa, kuna tabu kweli huko nje.

Mhe. Spika, wengine zile kazi wanazopewa hawana uwezo nazo, wametudanganya wamekwenda na vyeti vya udanganyifu, sasa huwezi kukaa tu kule ukawafanyisha kazi kama huna uwezo nazo. Mambo ya kwenda na vyeti feki sasa hivi yameshapitwa na wakati, sawasawa na lile suala la Mheshimiwa Muasisi yule mwalimu anasema ana *masters*, lakini hajarekebishiwa mshahara wake mpaka leo anadhalilishwa. Yule kafanya masomo yake na mitihani yake kwa *online*, sasa cheti chake hakijatambuliwa sio rasmi. Hatusemi haitambuliwi *online*, inatambuliwa, lakini cheti chenyewe bado hakijafika mahali kwa kiwango cha kutambulikana, lakini *Inshaallah* tutafanya utaratibu ili na yeye tumjaalie chochote.

Mhe. Spika, suala la *project* wale walimu wa *TAP*. *TAP* kama hamjui wengi nakupeni taarifa, *TAP is my baby*. Mimi wakati nikiwa Waziri wa Elimu na kabla sijawa Waziri wa Elimu kulikuwa na miradi mitatu ilianzishwa pale Wizara ya Elimu, kulikuwa na mradi unaitwa *PILOC*, maana yake ni *Form I English Language Orientation Course*, ndio lile darasa ambalo linaitwa *Form One Zero*, kama mliwahi kulisikia. Baada ya kuondoka *PILOC*, ukaingia mradi mwengine ukaitwa *SELOC, Secondary Orientation Classes*, yaani unaingia darasa la nane au mwaka wa nane kwa *orientation* kuingia kwenye sekondari na masomo ya sayansi yanafundishwa pale. Kwa hiyo, ujiandae na masomo mengine ya sekondari.

Mhe. Spika, baadae tukasema sasa tumeshawasomesha wanafunzi tuanzishe *program* za walimu tukaziita *TAP*. *TAP* maana yake ni *Teachers Advancement Programme* na tulikubaliana na tulitia saini kwamba Agakhan wata-*finance* ule mradi wa *TAP*, lakini hawa walimu wakimaliza masomo yao, basi wapatiwe nyongeza. Kwa bahati mbaya imechelewa na kwanza zile *Certificates* zenyewe zilichelewa kufika katika vyombo vinavyohusika kwa ajili ya kupata ithibati. Nina furaha kusema kwamba masuala yao walimu wale tumeyapeleka Wizara ya Elimu tayari sasa hivi na tumeamua tuwapandishe daraja *level* kati ya *form IV* na *form VI*, yaani daraja kidogo ya juu zaidi kuliko walipokuwepo pale mwanzo. Kwa hiyo, mambo yao ya *TAP* sasa hivi yatakuwa mazuri na nawaomba walimu waendelee kufanya kazi wasiwe na wasiwasi, *Inshaallah* lile lengo lililokusudiwa litakamilika.

Mhe. Spika, wengi wamelilia bajeti yangu kwamba ilikuwa kidogo, lakini ndio hali halisi wakati mwengine tusiwe na mashaka.

Mhe. Spika, kuhusu *E-Government*, watu wengi wamesema iko wapi hasa hii. *E-Government* ipo kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ipo Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, ipo Wizara ya Fedha au ipo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kote ipo, lakini sasa hivi Wizara yetu ndio dhamana wa kusimamia masuala yale na taasisi zote sasa hivi zimeshaunganishwa na mkonga ule wa Taifa, ndio maana yake tukasema sasa hivi tunataka tuunganishe na *E-Service*, yaani sasa zipatikane huduma ndani ya taasisi zenyewe.

Mhe. Spika, kwa hiyo, kwa ufupi *E-Government* mkonga wa Taifa ule unasimamiwa na Wizara yangu, lakini kwenye mambo ya kitaalam ni watu wa Mawasiliano, katika mambo ya malipo ya fedha zinatoka Wizara ya Fedha moja kwa moja wao, ndio wanasimamia. Kwa hiyo, Wizara zote tatu zinahusika na watakapokuja wenyewe Wizara ya Fedha mtakuja kuwauliza.

Mhe. Spika, nimejitahidi kuongeza ajira soko la Jumapili la Chake Chake, nimesema lime-*create* ajira 112. Mheshimiwa ananambia Waziri asitudanganye hapa, ajira gani zile zipo na nani walioajiriwa pale. Mhe. Haji Omar Kheir katoa ufafanuzi ajira ni kazi ambayo unapata mapato halali, hata kama anauza ubuyu ni ajira. Ajira sio kuvaa tai na suti ukenda kazini. Sisi tunaovaa tai na masuti ndio tunaopata mshahara mdogo kuliko hao wengine wanaofanya kazi zao binafsi. Sasa nimethibitisha kwamba pale Chake Chake ndio kwenye soko lenyewe, kule ndani wanajaa na nje wanafurika pale tena wananchi wamefurahia sana kwamba tumefungua njia ya kuuza biashara zao pale. Kwa hiyo, Mhe. Salma ajira zipo na tuendelee kuunga mkono juhudi zile za serikali.

Mhe. Spika, na kwa kusema kweli imesaidia sana, soko letu la Jumapili la hapa Michenzani hatukufanya vizuri, pana mambo yamekosewa kidogo na kweli taratibu za pale hazijenda vizuri. Wanakwenda, lakini hawaendi vizuri, lakini masuala haya sasa hivi hayapo Wizarani kwangu tena ya Uwezeshaji, haya yapo Wizara nyengine, lakini bado tunashirikiana kwa pamoja. Bi Zainab anasikia atajitahidi. Soko hili la Jumapili la pale Chake Chake lilileta msisimko sana.

Mhe. Spika, Mhe. Mussa Ali Hassan amesema anaondosha shilingi kwa sababu mambo ya makumbusho haya hatuyashughulikii vizuri. Mhe. Mussa makumbusho anayo Mhe. Said Ali Mbarouk, ngoja afikishe bajeti yake hapa, halafu umzuie shilingi. Sasa unaposema unanizuilia mimi kwa kitu ambacho hakipo kwenye mamlaka yangu unanionea. Mimi ni mambo ya nyaraka na kumbukumbu, mambo ya makumbusho na mambo mengine haya ya magofu hayapo kwangu.

Mhe. Spika, lakini hata Mhe. Said Ali Mbarouk utakuwa unamuonea huyu kwa sababu utamzuilia kwa mantiki gani. Kwa sababu tatizo lililojitokeza Mhe. Mussa pale kwenye eneo lako la Unguja Ukuu tulijenga lile kumbusho Serikali ya Sweden ilitusaidia pale, tukajenga pale, pale pale karibu yake ukenda ukajenga hoteli yako kitega uchumi, sasa matokeo yake tukakuzuia ndio ghasia zote hizo mpaka leo Mheshimiwa. Sasa si yamekwisha tena tumeshakubaliana huko na wewe unaendelea na shughuli zako kama kawaida. Sasa usizuie shilingi kwa sababu hiyo haitosaidia kitu.

Mhe. Spika, hivi sasa tunafanya kazi moja ya kukusanya takwimu za kujua hasa kila hoteli kuna wafanyakazi wangapi, wageni wangapi na wazalendo wangapi na naomba tupewe muda kidogo Mungu akipenda siku si nyingi takwimu nitazipata, nitakuja kuziwasilisha hapa Barazani tukijaaliwa.

Mhe. Spika, Uliuliza suala la bilioni 17, bilioni 17 hizi zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, naomba nizitolee ufafanuzi kidogo namna zilivyogawiwa. Ni vizuri tukaelewa, serikali ilitenga bilioni 17 kwa ajili ya mishahara na kiasi gani kinatumika na nani hasa aliyefaidika. Naomba wanisikilize vizuri Waheshimiwa.Wafanyakazi wote wa serikali mpaka Disemba 13 thalathini na nane elfu mia nne na thalathini na tisa walifaidika, kati ya hao wateule walikuwa ni mia moja na thalathini, yaani walifaidika na pesa hizo, lakini pia, kwa wafanyakazi wote hao thalathini na nane elfu, kila mmoja alipata shilingi ishirini na tano elfu muda wa miezi kumi, karibu bilioni 9 zilitumika.

Mhe. Spika, lakini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi thamanini na moja ambapo mabadiliko ya mshahara kwa upande wao yalianzia Julai 2013. Kwa hivyo, miongoni mwa watu waliofaidika katika hizi bilioni 17 ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na sisi tumo. Sasa tunazihoji pesa ambazo na sisi wenyewe tumefaidika nazo. Ninadhani sina haja tena ya kuendelea kutoa *breakdown,* lakini ikihitajika ninayo hapa, kwa sababu ya muda vile vile na sitaki kuchukua muda mrefu sana yasije yakatokezea mengine hapa, ikaja kuwa kazi.

Mhe. Spika, ninajua mengine sitoweza kuyajibu yote hapa na watakuwa na huruma ya kunionea huruma kwa yale mambo ambayo sikuweza kuyajibu, lakini nimejitahidi yale ya kimsingi kuyajibu yote. Ajira tutajitahidi kuongeza, tutaendelea kutafuta ajira mpya, ndio kazi yetu na mwisho kwenye kitabu changu nimesema kile kitabu ambacho Mhe. Hamza Hassan Juma amesema hakiungi mkono, lakini mwisho nimesema tutaendelea ku-*create* ajira na kutafuta njia gani tufanye tuwasaidie wazalendo kupata ajira nzuri zaidi.

Mhe. Spika, Waheshimiwa nakushukurani sana tuendelee kushirikiana, huruma zenu za kupitisha bajeti hii, ndio itakayonifanya kwenda kufuatilia yale yote muliyosema tuyafuatilie.Vyenginevyo mukicheleweshe na nyinyi munajicheleweshe.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kuendelea kuwa na imani na mimi na niwashukuru kwa kipindi chote ambacho nilipata mtihani karibu kila siku walikuwa wanakuja kuniangalia, lakini nimshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataalla* kwa sababu yeye tu ndiye mwenye uwezo wa kutuponyesha.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe mwenyewe umekuja si mara moja, si mara mbili umekuja kuniona na Waheshimiwa wengine wote waliopata bahati ya kuja kuniona na wale waliokuwa hawakubahatika, nimewasamehe wala wasiwe na matatizo yoyote. Ninajua nia yao ilikuwa ni nzuri na wameniombea kwa Mwenyezi Mungu na dalili zimeonekana hapa Barazani kila aliyesimama kaniombea Mungu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu na wao atawapa

uzima, atawaepushie na kila balaa na aina ya maradhi. Maradhi haya yaliyotupa mimi ninasema hata adui wako usimuombee. Shida yake ninaijua mimi na Dr. Sira Ubwa Mamboya alishuhudia.

Mhe. Spika, kwa hivyo, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akuepushieni, lakini nakuhakikishieni kwamba juzi nilikwenda Afrika ya Kusini, nimekwenda kufanya *checking*, ninasema hivi sasa nimerudi katika hali yangu ya kawaida. Kwa hivyo, *Inshaallah* nipo *fit* na nimeamua kuja kuisoma bajeti yangu, si kwa sababu sikutaka kumpa nafasi Mhe. Haji Omar Kheir, kuthibitisha kwamba nimepata uzima *Alhamdulillah.* (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa nadhani kwa leo itoshe hapa, si haba, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuja kufanya majumuisho haya na sidhani kama wataendelea kunikwamisha kwamisha wakaja kunipatia yale mambo mengine tena. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninakushukuru sana, ninakutakia kila la kheri na ninawatakia Wajumbe wachangia bajeti yangu pale ambapo *Inshaallah* watanipa maelekezo nitafuata *Inshaallah.* (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma kwa ufafanuzi na sasa Waheshimiwa Wajumbe basi niwahoji, wale wanaokubaliana na hoja hii na makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 27 - WIZARA YA NCHI (OR) KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu 0601 Idara ya Ajira -	Shs.25,000,000.00
Kifungu 0801 Kamisheni ya Kazi -	Shs.211,000,000.00
Jumla ya Fungu -	**Shs.251,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu na Kamati ya Matumizi zimepitishwa bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0111 Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Utumishi Shs.

Mhe. Mwenyekiti: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tugonge kwa utaratibu. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninataka nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Kaimu Waziri, ingawa pamoja na ibaji nyingi walionieleza, lakini bado sura ya kitabu hichi. Kwa sababu nimejaribu hapa nimechukua vitabu vyote vya bajeti Mhe. Mwenyekiti, kila kitabu kina sura ya Waziri katika ukurasa wa mbele. Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri kakiri kwamba mara nyengine, basi sura yake itakuwepo mwanzo na kwa bahati nzuri nina kitabu mpaka cha alipokuwa Waziri wa wizara nyengine, amejiweka mbele na nyuma.

Kwa hivyo, hili mimi ninafikiri limeshapata ufumbuzi sina tatizo nalo sana. Lakini hoja yangu inakuja katika hii Idara ya Miundo ya Utumishi. Nimesikia maelezo mengi ya Waheshimiwa Mawaziri wote wawili na kimsingi nilikuwa nimekusudia zaidi kwenye hili fungu lenye la Kamisheni, lakini naona bora nizungumzie hapa kwa sababu majukumu yenyewe yanalingana katika miundo ya taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, na alilalamika sana kwamba taasisi hizi hasa zinazosimamia serikali, basi Kamisheni inatakiwa iziangalie kwa umakini mkubwa kama Mataifa yanavyotaka, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, unatupa mafunzo mengi sasa hivi. Hivyo, tunapata kujifunza mambo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ninashukuru kuambiwa kwamba Ofisi ya *CAG*, sasa hivi mambo yao ndani ya bajeti hii, ninafikiri *once* tukimaliza tu hapa mambo yatakuwa mazuri. Ninaamini na wao sasa hivi wanapiga makofi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi mara nyingi hapa tunawasema watendaji wa serikali hawafanyi vizuri, wanatafuna, lakini mpaka pale, basi tunapowatakia mema, basi pia tuwaone wakorofi. Sasa mimi ninadhani kwa kuwa wanafanya kazi vizuri katika bajeti hii ya wizara hii tunawatakia mema maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuna moja tu Mhe. Waziri, hili kidogo pamoja na maelezo yote niliyoyataja, ninashukuru kwa ngazi ya Wakurugenzi wa Baraza sasa hivi kuanzia mwezi nimefanya *research* tukaambiwa kuwa mambo yapo vizuri, tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo moja mimi safari hii nilitaka kuzuia bajeti ya Baraza la Wawakilishi na nilitaka kuzuia kwa sababu kuna fedha kama alivyoeleza Mhe. Hamad Masoud Hamad juzi. Mhe. Hamad Masoud aliuliza leo inakuwaje mwaka uliopita vifungu la mishahara la Baraza la Wawakilishi lilikuwa kubwa, bajeti ya mwaka huu limekuwa dogo.

Mhe. Mwenyekiti, na ikaonekana kwamba labda Ofisi yako haipo makini, haikufanya uchambuzi labda wa zile fedha zilirushwa tu bila ya kufanyiwa utaratibu, lakini fedha zile ziliekwa kwa makusudi na ilikuwa katika kutekeleza ile *Scheme of service* ya Baraza la Wawakilishi na safari hii fedha zile mimi nikiwa kama Mwenyekiti, nimezi-*surrender* kuzirejesha serikalini wakati huku tayari miundo ya utumishi imeshakuwa tayari na ndio hili ambalo Mhe. Haji Omar Kheir pale Kaimu Waziri alipokuwa akilitolea maelezo, ndio nikasema inaonesha kuna *certain information* pengine labda Mhe. Kaimu Waziri alikuwa hana.

Mhe. Mwenyekiti, na hili lilikuwa halihitaji uwezo wa ziada wa serikali, tayari ndani ya bajeti ya mwaka uliopita ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti, tulidhiinisha fedha zile za *Scheme of service* na yale madaraja hapa Baraza la Wawakilishi tulikwisha kukamilisha.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa bahati, sasa hivi tunapata *support* kubwa ya wenzetu wa Kenya na Uganda ambao tumeajiri kuja kutufanyia mafunzo mbali mbali. Kimsingi wao ndio wanatuelimisha mambo mengi sana. Kwa hivyo, ile *Scheme of service* ilikuwa imeshakuwa tayari na zile fedha zilikwisha kuingizwa, lakini kwa kuwa Kamisheni ya Utumishi ya Umma waliukubali muundo, wakakataa yale maslahi yaliyokuwemo katika muundo kwa shingo upande, niliamua kuzi-*surrender* fedha zile nikazirejesha serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ninamshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu hata kwenye bajeti kuu ya serikali nilikuwa mgumu sana na nikasema kwamba fedha zile zirudi. Mhe. Waziri wa Fedha alichonihakikishia kwamba fedha zile zimerejeshwa ili Kamisheni ya Utumishi wa Umma wakishakubali ile *Scheme of service*, fedha zile zinatoka kwenye mfuko mkuu wa serikali, zinaingia kwenye Ofisi yetu ya Baraza la Wawakilishi nje ya bajeti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hili mimi ninafikiri Mhe. Waziri ninadhani ndio ambalo zaidi nimekuwa nimelizuia na kwa kweli nilikuwa mgumu sana, kwa sababu sio kwamba labda serikali haina uwezo, serikali tayari ilikuwa na uwezo na fedha tuliingiziwa, tumekaa nazo mwaka mzima tumezirejesha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimejaribu kutoa maelezo mengi ili Mhe. Waziri apate kunifahamu, lakini kimsingi ninawashukuru kwa jitihada zao kwamba muundo umekubalika. Sasa basi na yale mafao sasa hivi nadhani wakati umefika yaweze kurejeshwa ili hawa watendaji wetu waweze kufanya kazi zao kwa utulivu na umakini mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, na ndio maana Mhe. Waziri kwenye ki-*memo* changu kile nilijaribu kumuandikia, naamini kwa hili kwa wewe, linaweza kumalizika ndani ya muda mfupi. Kwa sababu ni suala ambalo ni la msingi na lina mantiki.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nadhani labda kama kutakuwa kuna maelezo ya ziada ya Mhe. Waziri labda nipate maelezo, halafu niangalie kama hili fungu niendelee kunyanyua mikono.
Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana na nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kunielewa vizuri na tokea zamani hakuwa mkaidi.

Mhe. Mwenyekiti, na sasa hivi kazidi kwamba ni laini zaidi na kwa sababu haya aliyozungumza yote, ndio serikali na ndio nia yake. Ninapenda niwatoe wasi wasi *Inshaallah* tukijaaliwa kinachofuatia sasa hivi ni kwamba serikali kimsingi imeshakubali kufanya haya marekebisho yote. Ni kuwaweka katika *grade* zao mbali mbali na *level* zao mbali mbali kwa mujibu wa zile kada zao zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata mara moja serikali haiwezi kudhulumu au haiwezi kwamba ikate mishahara au kwamba isiwalipe haki zao. Ni suala la *time* tu iliyobaki. Kwa hivyo, ni suala zima la kuvuta subira kidogo wakati serikali inafanya utaratibu, lakini masuala mengine wakati mwengine sio kwamba upande wa upande wa Tume ya Utumishi au Kamisheni, pengine ndani ya taasisi yenyewe kunatakiwa vile vile kunatakiwa tuharakishe kidogo hali masuala yasichelewe sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, yakiharakishwa hapa na kule yatatupa uharaka wa kuweza kuyatoa. Mimi ninapenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kwa vile kishaniambia kuwa nina uwezo nao kuyafanya, basi tutayafanya hayo asiwe na wasi wasi *Inshaallah* tutayavalia njuga ili tuweze kuyatekeleza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninaendelea tena kumshukuru mwalimu wangu Mhe. Waziri kwa kukiri, lakini kimsingi unajua kwamba hii wizara ndio kwanza umeipata, lakini suala hili la maslahi ya watumishi wa Baraza, Kamati ya Uongozi mbele ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tumelizungumza sana sana suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sitaki turejee hayo yaliyopita, lakini kwa sababu Waswahili wanasema kwamba; "Ukali wa nyuki ndio utamu wa asali yake". Sasa mimi nadhani ile sauti kali niliyokuwe nimeitoa na nikakitoa kitabu hichi moja kwa moja na nilikaribia kukichana, kwa sababu nilihisi Mhe. Waziri angelikuwa mkaidi wa kukataa haya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kuwa Mhe. Waziri amekuwa laini sana na ameyakubali yote na yatatekelezwa ndani ya kipindi hichi, lakini tu kuna jambo moja labda Mhe. Waziri ambalo nililizungumza mpaka kwenye Kamati ya Wenyeviti na Mhe. Waziri wa Fedha, kwamba haya maslahi yamechukua muda mrefu baada ya wenziwao kufaidika. Je, Mhe. Waziri kwa huruma yake, hichi kipindi tangu wenziwao waliporekebishiwa maslahi yao mpaka leo Mhe. Waziri anakubali baada ya mwaka mmoja, tutawaangalia vipi hawa watumishi. Kwanza sio wengi, wala hawatoitikisa bajeti ya serikali, ni wachache sana ambao serikali wala haitotikisika, wala kujua labda ngapi zilitoka kule.

Mhe. Mwenyekiti, na zaidi kwa sababu ninasema hili Mhe. Waziri, fedha hizi kama nilivyosema tulizihifadhi na ninakushukuru sana, wewe ni mtu wa imani sana, maana yake fedha zile hukutaka kuzihaulisha, ulisema hizi ninazibakisha wakati wowote Mhe. Waziri atakaposema muundo nimeukubali, basi haya maslahi moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa hii bajeti mpaka sasa hivi fedha hazijarudishwa serikalini, zimo bado katika ndani ya mkoba wetu wa Baraza la Wawakilishi, basi Mheshimiwa sema tu. Aseme tu, basi fedha hizi zisirudi serikalini na *figures* yake zinajulikana na Mhe. Hamad Masoud Hamad juzi aling'ang'ana sana na kwa bahati mbaya ulikuwa hupo, lakini aliitoa maanani Ofisi yetu kwamba hatupo makini, lakini kumbe tulikuwa tupo makini kwa sababu tunajua hizi ni fedha za watu, tumezihifadhi na kabla ya kupita bajeti hii tutaambiwa, basi zitumieni walipeni wenyewe, ili bajeti inayokuja isiwe na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, nasubiri kauli ya waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hebu kaa hapo hapo, kisogeze hicho kipaza sauti kama kuna maelezo kidogo utowe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Ehee! Wewe kaa hapo hapo bila ya kusimama.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Haah! bora nisimame tu, hakuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Kweli eeh! Haya.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, najua unanihurumia sana na ni lazima unihurumie kwa sababu nyingi tu, lakini sisemi Mhe. Hamza hanihurumii, hapana, anatekeleza wajibu wake.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kama nilivyosema, imeshasema kwamba haina pingamizi na marekebisho yatakayofanywa, lakini kuna taratibu za kisera, sera zikubalike kwanza na hivi sasa kwa mujibu wa muundo wa utumishi, hajafanyiwa mtu yeyote marekebisho yale, kwa sababu hatuwezi kufanya kwa taasisi moja na nyengine tukaziwacha. Tukifanya marekebisho yale, basi tufanye kwa serikali nzima, tuvute subira, madamu serikali imeshatoa ruhusa kwa maelekezo mengine, basi tuvute subira na hili jambo litakuwa tukijaaliwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea au bado. Haya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo kidogo kalizungumza Mhe. Waziri, ndio nataka niweke sawa. Mhe. Mwenyekiti, suala lilikuwa limeshakwenda vizuri sana, lakini Mhe. Waziri kalirudisha kidogo na ndio maana hapa nilikuwa nataka nipate maelezi ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, hii sera ambayo Mhe. Waziri anasema bado, ndio yale yale niliyosema jana kwamba tunaukubali muundo, lakini yale maslahi hayajakubaliwa, lakini maelezo ya Mhe. Kaimu Waziri alieleza kwamba wao wenyewe kazi iliyobakia ni kutengeneza zile kada na zile stahili zao, wakati huku kwenye Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti, kazi hiyo ilikwisha kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tukubali kwamba utaratibu wa Baraza la Wawakilishi na utaratibu wa serikalini, hauwezi kwenda sambamba kwa sababu Baraza la Wawakilishi ndio linaisimamia serikali. Kwa hivyo, Baraza la Wawakilishi walitakiwa wao waandae utaratibu wa kuwajenga watu wao vizuri mapema, ili waisimamie serikali. Sasa tukisema kwamba tusubiri mpaka sera huko ya serikali nzima, Mhe. Waziri huku bado tutaendelea kudumaa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani juzi kwa bahati mbaya tulipokuwa katika mkutano wa kujenga uwezo wa Baraza. Kwa bahati wewe ulipata maadhura kidogo ukawa hupo, lakini wenzetu sasa hivi hatua ambayo wamefikia, wao wanaajiri mpaka watu wa nje ya serikali, wanatafuta watu waliobobea kwa sababu *scheme* zao ziko vizuri. Sasa leo serikali kuizuwia *scheme* yetu, kwa sababu wao hawajaandaa sera, sisi huku kwetu tumeshakamilisha kila kitu. Tunataka kujenga uwezo wa taasisi yetu, kuwalipa vizuri watendaji wetu ili watusaidie vizuri kuisimamia serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa huko serikalini wacha waendelee kusubiri sera zao, lakini kwa upande wa Baraza la Wawakilishi ni vitu tofauti *Operation of power* na ndio maana hata kwenye Ofisi ya *CAG*, ingawa kule bado serikalini, lakini bado *CAG* na Baraza la Wawakilishi hizi ni taasisi ambazo zinaisimamia serikali kuichunguza na kuisimamia. Sasa utakaposubiri mlolongo mrefu wa serikali itujenge uwezo ili tuwasimamie.

Mhe. Mwenyekiti, hayo yatakuwa ni yao wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani huku kwetu masuala haya yalikuwa yameshamaliza na ndio maana nikasema kwamba hatuombi pesa mpya katika muundo wa utumishi wa Baraza, huku kwetu tulikwisha kukamilisha. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo tuelewane vizuri. Baraza la Wawakilishi na nafikiri tulipokwenda katika ziara Maalim Haroun tulimchukua. Katika mawaziri ambao tuliwachukua katika ziara zetu, kwenda kwenye Mabunge ya nchi yengine, ili kuangalia *treatments* za Bunge ziko *separate* na serikali. Sasa hili mimi nadhani...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, usijadili tena upya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sawa sijadili. Unajua ninamrejesha Mhe. Waziri mpaka katika ile ziara, nafikiria tulikwenda naye India kama sikosei, aliona ni namna gani India ilivyokuwa *treated* na serikali inavyokuwa *treated* vile vile. Sasa tukisubiri sera ya serikali, wakisema mwaka huu mzima hawakukamilisha, ina maana huku sisi tushindwe kutengeneza nani hii.

Mhe. Mwenyekiti: Haya ishia hapo. Kuna maelezo zaidi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikutaka ku-*intervene* kwa sababu sikupenda ionekane kwamba mimi ndio mkorofi yule yule, hapana. Ninachotaka kuzungumza hapa ni kitu ambacho kinaweza kutekelezeka na ili hili jambo liweze kutekelezeka, basi sote tunatakiwa tuambizane ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe uliongoza msafara wa kwenda kwa Mhe. Rais pamoja na timu yako, suala hili mulilizungumza kwa mapana yake na mkafikia pahala. Mimi nadhani imefikia pahala wewe sasa utusaidie kutoa muongozo juu ya suala hili. Kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma. Serikali hatuna matatizo na jambo hili, kinachofuata sasa ni kufuata ule utaratibu na Mhe. Hamza Hassan Juma, mimi nakubaliana na yeye na hata juzi niliposaidia ile hoja aliyoitoa Mhe. Hija Hassan Hija, nilikuwa na maana hiyo. Hayo anayoyazungumza ni lazima yawe katika utaratibu wa kisheria na ndio maana serikali imekubali ile sheria ya Utawala wa Baraza iweze kuletwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunazungumzia suala la *Scheme of service,* muundo wa utumishi serikali imeidhinisha, lakini kwa serikali nzima kwa taasisi zote mihimili yote ya dola, tumesema kwanza tuwa-*fit* watumishi katika *Scheme of service* kuwapa ngazi zao za kiutumishi kila mmoja. Hilo jambo hata Baraza la Wawakilishi halijafanya, akiwauliza watumishi wa Baraza la Wawakilishi, nani anaijua daraja yake ya kiutumishi ni kwamba inatakiwa sasa taasisi yenyewe iweze kuwapanga, ikisha kuwapanga serikali baadaye itakuja kuona uwezekano sasa wa kuowanisha na ukishapangwa kwenye hiyo *scheme* sasa hivi, kwa mfano kwa mujibu wa *scheme* ilivyo na mshahara unavyolipika, sasa kwa mujibu wa daraja iliyo, kama umepunjwa serikali saa yoyote itaweza kurekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili suala la kuweka mishahara na *scheme* na mapendekezo mapya kwa nchi nzima, hili halijafanyika. Sasa mimi nadhani, najua mbinu aliyokuwa anaifanya Mhe. Hamza Hassan Juma ya kumuweka Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma aseme anakubali, ili baadaye hili jambo lisiweze kutekelezeka, pawe na mzozo ionekane kama kuna mzozo kati ya serikali na muhimili huu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba muhimili wa Baraza la Wawakilishi, muhimili wa serikali na muhimili wa Mahakama ni vyombo vinavyotegemeana, vinafanyakazi kwa pamoja. Kwa vyovyote vile vyombo vyote hivi vinategemea Hazina moja. Sasa mimi nadhani Mhe. Mjumbe angeturuhusu akatukubalia, vyenginevyo tutasema maneno haya ya kutoa tamaa kwa jambo ambalo haliwezekani kulisema. Kwa hivyo, mimi nadhani tukubaliane kwamba Baraza lenyewe kupitia Tume ya Utumishi na *Management* yake, iwaweke wafanyakazi kwa mujibu wa *Scheme of service* na daraja zao, masuala ya mshahara, nadhani mmezungumza sana mlipokwenda kumuona Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nadhani suala hili mwenzetu Mhe. Hamza Hassan Juma, aelewe kwamba serikali haina nia mbaya kwa watumishi wa Baraza la Wawakilishi. Tumesikia na litaendelea kufanyiwa kazi kama serikali ilivyokwisha kuamua.

Mhe. Mwenyekiti, alivyosema suala la sera ni kwamba sera ya malipo ya mishahara yanakwenda kwa nchi nzima, kwa taasisi zote za dola, huwezi kuwa taasisi hii ukaipa upendeleo na taasisi nyengine ukaiwacha huo ndio msimamo wa serikali. Sasa mimi nadhani tusikae hapa, tukapakana mafuta kwa nyuma ya chupa, mimi nataka kuwa muwazi. Maamuzi ya serikali ni hayo na hii haisababishi kwamba ndio serikali kitu chengine. Kwa hivyo, inawapangia, ndio utaratibu uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, itakapokuja hiyo Sheria ya Utawala wa Baraza, haya mambo sasa yatakuwa yanafanywa kwa mujibu wa hiyo sheria, lakini kwa sasa Sheria ya Utawala wa Baraza haipo ni vizuri tukaendelea kutumia sheria ambazo zipo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba utuongoze.

Mhe. Mwenyekiti: Muongozo ambao natoa ni mmoja tu. Tunashukuru kwanza kwa maelezo hayo mazuri na ndio maelezo ambayo mimi niliyatoa wakati ule tunapitisha kasma za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, jambo hii lilijitokeza kwenye hoja, tukaamua na Wajumbe nyinyi mlipiga kura ya kupitisha na ndio hoja hii hii inakuja hivi sasa, jambo hili tumeshaliamua. Kwa hivyo, ni kwamba tunasubiri jambo hili ili serikali iandae kwa serikali nzima kufanya marekebisho kwa mujibu wa miundo hiyo ya utumishi kutoka taasisi mbali mbali. Tuendelee.

Kifungu 0111	Idara ya Miundo ya Taasisi Utumishi na Maslahi ya Watumishi -	162,286,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba -	427,035,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti-	156,753,000

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba fungu 0201 hukulihoji mara ya mwisho ukaniambia tuendelee, lakini...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, endelea na hoja hapa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, haya, lakini naamini unayo nafasi kubwa, kwa kuwa Mhe. Waziri keshapoa atapata nafasi nalo. Nakuja katika Idara ya Mipango ambalo nilizungumzia suala zima la wafanyakazi wetu, hasa wanaofanyakazi katika sekta binafsi kuwa ni wafanyakazi ambao wanaishi katika maisha ya kubahatisha na wanaishi katika maisha ya kubahatisha kwa sababu kila mwaka inabidi waombe ajira, hasa katika sekta ambayo serikali yetu imejitahidi kutoa ajira nyingi kwa vijana wake, sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa wengine hawana mikataba wanafanyakazi, lakini wengine wanafanyakazi, lakini mikataba yao ni ya mwaka mmoja mmoja. Kwa hivyo, hapa inatuhakikishia kwamba hawa wataendelea kuishi kwa muda mrefu na hatimaye hata kiinua mgongo hawana. Kwa hivyo, kwa kiasi fulani wanafanyakazi kama hawana uhakika. Ikishamaliza *season* kama sasa hivi tuko mwezi wa Mei. Kuanzia mwezi wa Juni vijana wetu wanakwenda kuhangaika kuomba tena kazi katika sehemu ambazo walikuwa wakifanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa namtaka Mhe. Waziri anisaidie labda ana utaratibu gani wa kuangalia hawa wafanyakazi wetu, hasa katika hizi sekta binafsi angalau kuwa na mikataba ya muda mrefu na ikawa na hifadhi ya maisha yao, wasiwe na maisha ya kubahatisha na wengi wao wana wake na watoto, wanakuwa baadaye watoto wao wanayumba.

Mhe. Mwenyekiti, nataka maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuhakikishie Mhe. Hamza Hassan Juma suala lake leo hii tumelizungumza juu ya kuangalia mikataba upya ya wafanyakazi wetu, lakini tuna tatizo moja ambalo linatusibu wakati mwengine hasa kwenye mahoteli. Siku kama *season* za kipindi hiki wanasema iko chini kibiashara, yaani wageni hawapo. Kwa hivyo, mikataba yao na wao inabidi wengine wapewe likizo bila malipo au pengine warejeshwe kwanza mpaka wageni watakapoanza kuingia tena.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tunataka tuweke utaratibu kwamba hata wakati ule wa *low season*, basi wale wafanyakazi waendelee kufaidika na kupata chochote pale, kwa sababu *it is unfair* kwa mfanyakazi ukamuhitajia kwa wakati fulani tu na wakati fulani usimuhitajie, lakini hawa watu wa sekta binafsi tujuwe kwamba wanafanyabiashara na wao wanataka wapate faida, sasa hatuwezi tukawafunga sana, kwa sababu masuala ya utalii, haya ukifanya mchezo mwenzako jirani yako anawachukua, ukimuwekea masharti sana, anahama itakuja kuwa matatizo. Kwa hivyo, ni lazima tuletee mikataba yao, tutaifuatilia tujuwe mikataba yao iko vipi na ile yenye mushkeli, tutajaribu kuzungumza nao na wenye taasisi hizo ili turekebishe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hilo suala tumelizungumza na tunaifuatilia mikataba kuona kwamba haiwadhalilishi wafanyakazi wale tukijaaliwa katika maisha yao ya kila siku. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema Mhe. Waziri bado ni mpya katika wizara hii, naamini hili suala nimpe nafasi alifanyie kazi, lakini nitamuomba kitu kimoja, tutapitisha fungu hili la mipango sera na tutakupitishia fungu la safari za nje. Nitakuomba sana hebu tafuta hizi nchi ambazo zaidi uchumi wao unategemea utalii, wala mimi usinichukuwe. Wewe nenda ukafanye *research*, halafu uangalie wale wenye mahoteli au wale wawekezaji, zile ajira zao kwa wale wananchi wa pale, kuna *condition* gani ambazo wanazowekewa wakati wa *low season*?

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa kuwa suala hili mtakwenda kukaa kulijadili na wawekezaji. Mimi nadhani naweza kujaribu kutoa ushauri ambao pengine na wawekezaji wanaweza wakauzingatia. Katika hiki kipindi mfano hapa Zanzibar kuna miezi mitatu hii inakuwa *low season*, basi angalau japo nusu ya mshahara katika ile mikataba hao wale wafanyakazi wakawa wanapata, ambapo mtu ataweza ndani ya miezi mitatu angalau kuweza kununua sabuni na mama watoto nyumbani. Sasa hili mimi sitaki kumlazimisha, lakini ajaribu kuangalia Mhe. Waziri atakapokuwa katika *negotiation*, lakini bado nilikuwa namuomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, mwakani naomba hasa akija aje aniambie Mhe. Hamza Hassan kwamba nilikwenda, aidha, Maldivu au kwengineko nikawaangalia wale wawekezaji na wale wananchi wa pale katika ile *low season*, je, wanazingatiwa vipi maslahi yao? Ahsante.

Kifungu 0401

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nilitamka na kwenye *Hansard* limeandikwa kuwa fungu hili nitalizuwia, lakini kwa kuwa Mhe. Waziri wangu na hasa nilipata mawaidha leo makali sana kwa kupitia Mhe. Ali Mzee Ali ya kuniambia kutokana na hali alivyo Mheshimiwa wangu na alisema kuwa tutazungumza na yeye ili kidogo niwe aste aste.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa kunijibu vizuri sana, nimeridhika na *messages* zimeingia nyingi sana na kwa taarifa tu nimealikwa nikale ng'ombe mzima, kutokana na taarifa yako ilivyokuwa nzuri sana. Umesifiwa umeambiwa huo ndio ujasiri wa kizalendo wa Kizanzibari ulivyofanya huku hiyo. Hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, ni dogo tu. Kuna Kampuni ya Vespa ambayo ya ulinzi imeajiri vijana wengi, hatimaye wameingia mitini na mpaka sasa hivi *cheque* ninavyosikia iko *Millenia* pale ambapo ni Kempiski ya zamani na hili nililisema, lakini hukulitolea hoja kutokana na hali yako. Sikupigii buti, lakini nakuomba hili nalo ulishikilie bango ili wale wazalendo wako wapewe zile fedha ile *cheque* isitoke mpaka walipwe kama ni kweli. Kama ni uongo tuwatafute tuwakamate, kwa sababu hawa wamewadanganya, wamewaambia subirini *cheque* iko *Millenia* pale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba suala hili hukulisema, najua hukusema kwa nia mbaya binadamu imo mtafaruku imo dunia, kuumwa dunia imo. Kwa sababu mimi naitwa Makame Mshimba Mbarouk, uliniita Makame na nihii, hiyo sikulaumu nilijua ni moja katika kupitikiwa mwalimu wangu, naomba na hili nijibu kwa lugha fasaha kabisa ili tuliruhusu hili fungu. Sikukusudii kukupigia buti kwa maneno matamu, lakini naomba nipe kidogo muruwa wa maneno na hasa kwa mzee wangu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Makame Mshimba kesho aje Ofisini kwangu asubuhi kama saa 4:00 namuombea ruhusa kabisa hapa, *Inshaallah*,basi aje tuyamalize haya mara moja tu wala hakuna matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali, naomba tuendelee, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ambarikie kila la kheri na yeye. Ahsante sana.

Kifun gu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti-	154,753,000
Kifungu 0403 Chuo cha Utawala wa Umma-	555,100,000
Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi-	981,873,000
Kifungu 0601 Idara ya Ajira-	126,204,000
Kifungu 0701 Idara ya Usalama na Afya Kazini-	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ndio ninampa afya mwalimu wangu, wala asiwe na wasiwasi. Hapa nilizungumzia suala la Bima ya Afya kwa wafanyakazi wetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mhe. Waziri alieleza kwenye maelezo yake kwamba wanaandaa huo utaratibu na ninajua Wizara ya Afya kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri katika maelezo yake wao wanahusika zaidi. Sasa wafanyakazi wetu kwa kweli kwa muda mrefu wanakuwa wanatulalamikia jinsi wanavyoona hasa wenzao wa upande wa pili wa Muungano wanavyofaidika na hizi Bima za Afya.

Mhe. Mwenyekiti, basi labda ningelipata tu maelezo labda utaratibu kwa serikali mategemeo ndani ya mwaka huu wa bajeti hii ambayo tuliyokuwa nayo tutegemee labda wafanyakazi wetu wataweza kufaidika na bima hii. Kwa sababu mara nyingi wananchi wetu ikifika tarehe 10 mfukoni anakuwa hana kitu na yanapotokezea maradhi aidha yeye au ndani ya familia inabidi sasa hodi hodi na wale anaowapigia hodi ni sawa sawa na wao vile vile. Kwa hivyo, tunaishi katika maisha ambayo mazingira magumu sana. Sasa labda Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Afya labda wameshafikia *stage* gani kuhakikisha kwamba alau ndani ya mwaka huu tunaweza tuka-*take off.*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mhe. Hamza kwa kuliulizia suala hili ili kutaka undani wake. Mhe. Mwenyekiti, kama angelijua Mhe. Hamza jinsi gani sisi tunavyopata tabu ya kupata matumizi kwa ajili ya kununua vifaa na dawa, ninafikiri angetuonea huruma kwa sababu tegemeo letu kubwa tunategemea kwamba mchango wa Bima ya Afya ndio mchango unaofanya mambo makubwa kuliko hata mchango wa serikalini. Kwa sababu pesa zinachangwa, lakini Bima za Afya ziko aina nyingi kulingana na hii tofauti na uwezo tofauti wa serikali na wale wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu uwezo wa serikali yetu, kama tunavyofahamu mishahara ya watu wetu na mikato tuliyonayo. Tunatakiwa *ZSSF*, tunatakiwa Bima tunatakiwa na mikato mingi tu na wafanyakazi wetu hao hao siku hizi katika maisha yao mikopo ni mingi. Kwa hivyo, unakuja unamkuta mtu mwisho wa mwezi hata kile cha kukila hana, anakopa anasomesha watoto, anakopa kwa sababu yake mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hayo yote lazima serikali iangalie na ione utaratibu gani utakaowezesha wale watu kukatwa, lakini wakati huo huo maisha yao yende vizuri. Wanaoandaa mpango wamefikia mipango mingi kuangalia ambayo wanajaribu kutafuta uwezekano wa ule mpango ambao kwa kweli utawasaidia watu. Hatuwezi tukajilinganisha na mipango kama hiyo ya Bima ya Bara, mishahara yao ni tofauti. Kwa hivyo, mshauri muelekezi aliyepo ndie anaendelea na hiyo hali na si kazi nyepesi na rahisi kama tunavyofikiria. Sisi tunafikiri maelekezo tutakayoyapata, Makatibu Wakuu wananisikia na baadae itapitishwa kunakostahiki na baadae tutapata jawabu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Naibu Waziri hapa kwa maelezo yake mazuri, sasa nadhani wewe mwenyewe shahidi mfano kama wenzetu Uganda au Kenya wale Waheshimiwa wana kadi tatu za Bima ya Afya. Kuna Hospitali za pale pale, Hospitali za Mikoa na Hospitali za nje. Sasa mimi ushauri wangu kwa kuwa hapa Zanzibar kuna Wizara na taasisi mbali mbali ambao kuna baadhi ya taasisi wao kidogo maslahi yao...

Mhe. Spika: Kwa kifupi lakini.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sawa, wao maslahi kidogo yako vizuri, basi nadhani *at least* wangelianzia kwa wao. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ile Bima ya Afya ikianza itaisaidia hata Hospitali yetu, kwa sababu wale ambao watakuwa na uwezo wa kuanza, kama mfano Mashirika, Mashirika yetu kidogo mimi naamini waka-*afford, at least* wale wakaanza alau ile Hospitali yetu ikaanza kutotonoka kupata fedha za kununulia vifaa na za kuendeshea kazi, halafu hizi taasisi nyengine zikafuata baadae.

Mhe. Mwenyekiti, huu *just* ulikuwa ni ushauri wangu au sijui wamejaribu kuangalia vipi, mfano hata katika taasisi yetu, hapa mimi nadhani ni pahala ambapo yapo maeneo kama nilivyosema wanaweza wakaanzia, tusisubiri lazima labda serikali nzima iingie katika hii Bima ya Afya. Kwa sababu moja ni lengo la kuisaidia mpaka Hospitali yetu kuu ya Mnazimmoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Naibu wangu pamoja na ushauri mzuri wa Mhe. Hamza, naomba kutoa taarifa tu kwamba kazi hii tunajitahidi italetwa hapa, Mungu *Inshaallah* akituweka hai kabla ya Kikao cha Januari ili tupate kitu kamili *Inshaallah* Mungu akitujaalia.

Mhe. Spika: Nadhani ushauri huo umepokelewa na taarifa italetwa hapa. Tuendelee.

Kifungu 0701 Idara ya Usalama na Afya Kazini- 126,235,000
Kifungu 0801 Kamisheni ya Kazi-

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ukifanya kazi sana na wananchi matokeo yake ndio yanakuwa kama haya, kwa sababu kila mmoja anakupa lake ulipeleke na kwa sababu hapa ndio uwanja ambao wananchi wanapata kusikia Wawakilishi wao wanawatumikia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili la Kamisheni ya Kazi, ninaamini bila shaka linahusu mpaka katika sekta ya uwekezaji na hata vibali vya kazi vinatoka katika kupitia Idara hii, nadhani Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi. Kwanza namshukuru kwa lile moja alilosema kwamba kwa safari hii hawezi kutoa kibali kwa mgeni kama kazi ile inawezekana na mzalendo. Kwa hivyo, hilo kwa kweli namshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sasa naomba moja Mhe. Waziri alifanyie kazi hivi sasa, hawa wawekezaji wanatumia manyanyaso makubwa kwa kuchukua bidhaa kwa wananchi wanyonge wale ma-*supplier*. Kuna vijana mfano kama pale Nungwi wao wamesha-*supply* bidhaa mbali mbali kwa mahoteli karibu matatu, manne, lakini kimsingi katika suala zima la malipo yao kwa kweli inachukua zaidi ya miaka 2, 3 na kwa kweli wameshafika mpaka kwa Makamu wa Pili wa Rais, nadhani idara yake ya uratibu wa shughuli za serikali wanashughulikia masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili pamoja kwamba haliendi moja kwa moja, lakini kwa kuwa wao ndio wanaotoa vibali vya kazi, nadhani Mhe. Waziri na hili tunaomba atusaidie ili wale sasa wanapochukua bidhaa za waanchi wanyonge, waje vile vile kuwa zile bidhaa huwa wanakopeshwa na maeneo mbali mbali. Sasa hili sijui Mhe. Waziri ataweza kutusaidia vipi ili hawa vijana wetu ingawa moja kwa moja hapa wanakusudia Kamisheni na *supplier* vitu viwili tofauti, lakini wao ndio wanaotoa vibali vya kazi kwa wale wageni ambao wanochukua bidhaa za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, nafikiri amelielewa, nafikiri atanisaidia maelezo ya kutosha na wenyewe wananisikia huko Nungwi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kuna haja ya kumfungulia darasa la nyongeza kama lile la elimu mbadala Mhe. Hamza, kwa sababu naomba atafautishe juu ya mambo mawili. Wizara yangu inatoa vibali vya kazi, lakini sichagui *suppliers* wa kupeleka vyakula kwenye mahoteli. Sasa kama kuna *any delay* ni kati ya yule *supplier* na hoteli yenyewe. Sasa kuna vyombo vya kisheria, Mahakama waanze huko Wilayani wende Mkoani. Sasa mimi ninacho chombo changu cha Mahakama kinaitwa *DHU* kweli, lakini kutatua migogoro ya kazi, sio migogoro kwamba watu wanadaiana aa, hayo hayako kwangu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Hamza, nitendee haki mwalimu wako, mimi nishayabeba, basi hata haya ya kwamba mtu ana-*supply* kuku anachelewa kulipwa, unataka nayo pia Wizara yangu ya kazi ingie kati aa, *free*. Ninachoomba Mhe. Mwenyekiti, afafanue kati ya majukumu yanayohusiana katika sekta zetu nay ale yanayohusiana na yale ambayo yanahusiana na sekta nyengine. Kwa hivyo, Mhe. Hamza, sijui kama utawaambia wanaohusika, lakini mimi nasema hao wafanyabiashara wana *chamber* yao ya mambo ya biashara. Mimi nadhani ungeelekeza masuala yao wakenda wakalalamika kwenye chombo chao cha biashara ikiwa vizuri zaidi ni ushauri tu ninakupa, lakini Wizara yangu haihusiki kabisa wala hilo nisijaribu kulijibu kwa sababu nitakuja ku-*create* tatizo ambalo mimi ndio nitakuwa *responsible*. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, alipokuwa akitoa ufafanuzi wa kazi mpaka wauza chaza pia, waliitwa wafanyakazi, sasa na hawa vile vile ni sehemu ya wafanyakazi. Sasa mimi hapa hoja yangu ninafikiri Mhe. Waziri, ndio maana nikamwambia ajaribu kuliunganisha, kwa sababu hawa ambao wanaotoa hizi kazi ni wageni. Leo mtu anakuja kuomba kibali cha mwaka mwengine cha kazi, wakati huku kuna msururu wa watu ambao keshawachukulia vitu vyao hajawalipa, leo huyu anakuja kupewa kibali cha kazi hapo, ndio nilipopakusudia, lakini naomba hili liache, mimi nitamfata na mwisho atagundua kuwa pia lilikuwa linamhusu.

Mhe. Mwenyekiti, Ahsante tuendelee.

Kifungu 0801	Kamisheni ya Kazi-	286,444,000
Kifungu 0002	Idara ya Tekonolojia ya Habari na Mawasiliano	700,880,000
Kifungu 1003	Idara ya Mipango ya Raslimali Watu-	157,669,000
Kifungu 1201	Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu-	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo kwa Mhe. Waziri, nilipozungumzia Idara ya Nyaraka nilizungumzia suala la wizi uliofanyika, lakini vile vile, aliyekuwa anakaimu kiti chako. Pia, nilijaribu kumtaka atusaidie maelezo kwa sababu Baraza lililopita tuliunda Kamati Teule ya kwenda kufuatilia wizi ule,lakini leo Mhe. Waziri katika maelezo yake alitueleza kwamba serikali wameshafanya uchunguzi, sasa hili kidogo lilinipa tabu na bahati wamefanya uchunguzi na ripoti imeshafika serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa taratibu za kisheria Baraza kwa kuwa liliibua hii hoja. Kwa hivyo, ilikuwa nadhani ilikuwa lifanye kazi yake, halafu ile ripoti iwasilishwe serikalini, lakini sasa, je, kama serikali wao ndio waliofanya uchunguzi sasa Baraza litafanya nini? Je, ile Kamati Teule itakuwa imefutika, sasa hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo ya kisheria kwa sababu chombo hiki kikishatoa utaratibu serikali inakwenda kuchunguzwa, sasa serikali ikaamua kujichuguza wao wenyewe, hapa kidogo tulikuwa tunataka maelezo, maana tulikuwa tunaulizana ulizana sasa vipi ile Kamati ndio kidogo Mheshimiwa hapa nataka maelezo ya kisheria zaidi. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, suala hili lilikuwa na utata tangu mwanzo na tutakumbuka kwamba ilipokuja hoja hii ya kuunda Kamati Teule, serikali kwa upande wake nayo ilikuwa inachukua hatua. Kwa hivyo, ni mambo mawili yaliyokuwa yanakwenda kwa pamoja na katika Baraza hili tukaelezwa kwamba mambo haya hayatogongana na hoja ikapita ile ya kuunda Kamati Teule. Ila tatizo limekuja ni kwamba kipindi kile kilikuwa kimekuwa na shughuli nyingi sana. Kwa sababu mara baada ya kumaliza kikao kile ambacho kiliamua kuundwa Kamati Teule, basi tulikwenda katika Bunge Maalum na tumerudi kwenye Bunge Maalum tumeingia katika shughuli za Kamati, baada ya kumaliza shughuli za Kamati, tumeingia katika Baraza la Bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nilikumbushia kwamba kazi hiyo ifanyike, lakini kweli kibali cha mwisho kwamba kazi ifanywe, sikuruhusu kwa sababu tunaelewa kwamba mara nyingi tunakosa *quorum* hapa ndani ya ukumbi. Ningeitoa Kamati kwenda kazini, huko kuna hatari ya shughuli zetu kukwama kabisa, lakini nakumbuka hata Mhe. Mjumbe Jecha Simai yuko wapi, ni mmoja wapo kati ya Wajumbe ambao waifanye kazi hiyo. Tatizo ni kwamba bado hatujawa sawa katika kuhakikisha kwamba tuna *quorum* ya kutosha, lakini kimsingi hili jambo nalikumbuka na ilikuwa kama vile ambavyo tuliamua, basi liendelee.

Waheshimiwa Wajumbe, lakini kimsingi kama mtakumbuka vizuri ilikuwa kuna hoja kubwa sana kwamba kunafanyika kazi ya kidiplomasia na serikali ya Oman, ndio jibu ambalo limetoka sasa hivi, sasa itakuwaje kuja kwenda Kamati Teule pale, lakini maamuzi ya Baraza hili ikawa ni kwamba hilo jambo linaweza likenda sambambakila upande ukafanya shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo, nadhani tuone hapo baade kama itakuwa bado kuna haja na hasa hasa katika eneo lile la wale waliosababisha uzembe mpaka yakatokea hayo, basi Kamati ile itafanya kazi kama vile ambavyo tumeamua katika Baraza hili, lakini wakati huo huo tuzingatie sana kwamba kuwepo kwetu humu kwa wingi, ndio itasaidia Kamati ile ikaweza kufanya kazi, maana kuiruhusu Kamati ikafanye kazi wakati huku Baraza linasita na shughuli hii muhimu na ambayo ni shughuli ya kipaumbele kuliko jambo jengine lolote, nayo kidogo itakuwa inatupeleka pahala sipo.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo, uamuzi wa Baraza kwamba Kamati ifanye kazi, bado upo na tutaona na hatua ya serikali nini kimefikiwa, lakini hasa kwa upande wa ule uhalifu wenyewe, tena nao ulikuwa unafanyiwa kazi vile vile, ninakumbuka kwamba uchunguzi ulikuwa unafanywa na vyombo vinavyohusika juu ya wale ambao wanatuhumiwa kufanya makosa hayo ya uzembe, labda niishie na tuone hatua za baadae hapo usoni.

Kifungu 1201	Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu-	375,656,000
Kifungu 1301	Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi-	124,362,000
	Jumla ya Fungu-	4,180,500,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi
Bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0201	Utawala Unguja-	853,700,000
	Jumla ya Fungu-	853,700,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi
Bila ya mabadiliko yoyote)

Kijifungu 0201

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sisi uheshimiwa wetu tumeitwa kutokana na wananchi na wananchi ndio waliotutuma hapa kuja kuwafanyia kazi yao, la sivyo na hiki ndio chombo chao. Hoja zangu zilikuwa mbili, wakati nilipokuwa nikichangia; moja itakuwa kidogo kubwa na moja itakuwa ni ndogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu wazee umri wao kurejeshwa tena kazini kupewa mikataba na tukiwaacha watoto wenye *degree* na diploma mitaani, mifano hiyo ipo. Leo nilikuwa nataka serikali itoe kauli kwa suala hili tunawaacha watoto wetu wenye *degree* kuongezwa wazee wetu mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, hii Wizara ya Afya, ninajua Wizara ya Afya pengine wataleta wenyewe barua kuja kuomba kwako kibali kuhusu ajira ya daktari wa mifupa. Daktari aliyekuwepo Mnazimmoja ni mmoja tu wa mifupa kwa kipindi kirefu, lakini hii itakuja katika Wizara ya Afya, nafikiri wataomba wenyewe. Hoja yangu kubwa ni hii kuhusu ajira kuongezewa wazee wakati wengine wako juu ya vitanda wanaongezwa muda.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, ninachomwambia Mhe. Jaku, wazee wanaongezewa muda kwa sababu maalum kama hao tunawaita *Rare profession* wale ambao wanaongezewa muda wanakuwa na kada maalum, sio kama tunawaongezea tu na kama mtu anahitajika hata kama ni daktari ana *degree* ya kwanza, ya pili, lakini kama yuko mwengine ana *experience* keshatumikia miaka 30, anaweza akapewa *priority* yule, kwa yule *experience* yake na tunamuhitajia na Wizara wanayo haki hiyo ya kusema kwa mfano wanataka mtaalam, kwa nini wao watasema fulani anatufaa, fulani anatufaa, wanayo haki ya kutuletea na sisi tukawaruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili suala la vijana kwamba hawaajiriwi, kuna vijana zaidi ya elfu tano, hivi sasa wamemaliza diploma, wamemaliza *degree* ya kwanza, kweli hawajapata ajira, lakini ajira kama alivyosema Mhe. Asha, hapa si lazima serikalini, lakini hali itaporuhusu na tumeshasema wangapi wataajiriwa mwaka huu. Kwa hivyo, tutizame bajeti inayokuja fursa itakapopatikana tutawachukua. Kwa hivyo, Mhe. Jaku, yeye kaletwa na wananchi na sisi tumeletwa na wananchi vile vile, lakini pia, tumeteuliwa na serikali, kuilinda serikali yetu katika kuhakikisha kwamba na maslahi yanapatikana kwa serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, watu wako juu ya vitanda wanaongezwa muda na ni wagonjwa na huku wanataka utumishi wawatumikie wananchi, bado kitandawili hiki kingali vile vile, bado na mifano iko hai na mmoja ninafikiri katika Wizara yake kama sikosei Idara ya Nyaraka bado nataka kauli yako nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku aseme kitu ambacho ana uhakika nacho, lakini mtu gani wa Nyaraka ambaye amelazwa kitandani amepewa mkataba athibitishe hilo. Hiki ni chombo kikubwa unapotoa kauli kama hizo lazima uwe na uhakika wanachokizungumza ni kweli. Kama anazungumzia Mkurugenzi Maalim Hamad, Maalim Hamad sasa hivi yuko kwenye likizo la kustaafu na hajaongezewa muda, lakini tukimuhitajia Mheshimiwa tutampa, wa kitandani sio kwa sababu umekufa tu, mimi nilikuwa kitandani miezi mingapi na yeye anajua Mheshimiwa na *Alhamdulillahi*.

Mhe. Mwenyekiti, leo nikisimama leo, nazungumza natoa kauli hizi. Namshukuru Mwenyezi Mungu, sasa tuwe na huruma ya wananchi wetu hawa wameshatumikia nchi yetu miaka mingi. Sasa si kwa sababu ya Maalim Hamad au mtu mwengine yoyote, serikali hii haitomuonea mtu yoyote akiwa na haki atapata na kama huyu tutamhitajia Mhe. Jaku, namhakikishia tutamchukua yuko kitandani Mungu kamjaalia akipona *Inashaallah* tutamchukua. Kama hakupona Mwenyezi Mungu kamchukua, basi ndio uwezo wake Mwenyezi Mungu hatuwezi kumuingilia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kama ana uhakika kuna mwengine zaidi ya huyo aje atwambie, lakini sasa hivi Maalim Hamad yuko likizo ya kustaafu hata hayupo hakuna na hawezi kuja kwa sababu yuko likizo la kustaafu kuna Kaimu pale. Sasa kama huyo Kaimu ndio yuko kitandani na tumempa mkataba itakuwa suala jengine. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubali ulimi hauna mfupa, nimeteleza. Alivyokusudia Mhe. Waziri sahihi kabisa, Mhe. Hamad niombe radhi kwa hilo. Tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala Unguja -	510,900,000
	Jumla ya Fungu -	510,900,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti-	285,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Ajira -	

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa kupata nafasi hii nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu kiambatanisho nambari 6(a), ikiwa kinahusiana na ajira zilizopatikana katika nchi za nje. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuhangaika mpaka vijana wetu waliokuwa hawapungui 859 wakapata ajira huko nje, lakini hapa mimi nataka ufafanuzi wa mambo mawili ambayo kwa bahati mbaya sikuyasikia.

(a) Ni kuwa hapo zamani yalitokea mambo kama haya, lakini serikali ikakataa kutokana na sababu zao za msingi, lakini hivi sasa utekelezaji ndio kama tulivyouona, nikitaka kujua kuwa ni sababu zipi zilizofanywa zamani hili suala likakataliwa na hivi sasa ikawa linakua na muitikio mzuri kama huu?

Halafu la pili, likiwa kutokana na ajira ilivyo tukiangalia mfano kama Qatar kuna jumla ya wanaume 55, lakini wanawake ni 6 tu, lakini Oman kuja jumla ya wanaume 174 tu, lakini wanawake ni 401, ikiwa ni asilimia haipungui 64. Nikitaka kujua ni sababu gani kwengine wanawake ni wengi sana, lakini wanaume ni kidogo sana kinyume yake.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, sijui kama ni sahihi kwenye fedha za maendeleo kwa sababu hizo hoja zilikuwa ziko kwenye matumizi ya kawaida. Kule kwenye matumizi ya kawaida ndio inayofanya kazi hizo unazozitaja. Sasa mimi nadhani tufanye hivi nikuelekeze tu kwamba hebu nenda kwa Waziri Ofisini mlizungumze hilo. Kwa sababu kuhusu masuala yale ya Kamisheni ya Kazi, kuhusu utaratibu wa shughuli zenyewe kiidara ya sera ni kule kule kwenye matumizi ya kawaida, sio kwenye maendeleo. Kwa hivyo, onana na Mhe. Waziri ili upate maelezo juu ya jambo hilo. Tuendelee.

Kifungu 0601	Idara ya Ajira -	43,000,000
	Jumla ya Fungu-	328,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)
(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu, bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataaa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa mashirikiano makubw, Katibu anatueleza kwamba shughuli za leo zote mmezimaliza. Nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mhe. Waziri, pamoja na Wajumbe wote kwa kazi kubwa mlioifanya na kwa kuwa muda wenyewe umebakia kidogo tu, basi tusitishe shughuli zetu na niahirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 30/05/2014 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 1.34 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 30/05/2014 saa 3.00 asubuhi)